# MIKONO WA HOJA YA MUNGU

## *Nguzo za Agano*



*Dunstan Ruta*

# MIKONO WA HOJA
# YA MUNGU
***Nguzo Za Agano***

*Mwangaza na utukufu, salaam na sifa ziwe juu ya Mikono ya Hoja Yake, ambao kupitia kwao mwangaza wa uwezo umechomoza na ukweli umesitawishwa kwamba mamlaka ya kuchagua yamo katika mikono ya Mungu, Mwenye Uwezo, Mwenye Nguvu, Asiyezuilika, ambaye kupitia Kwake bahari ya ukarimu imefurika na manukato ya majaaliwa yenye neema ya Mungu, Bwana wa wanadamu, yametawanywa. Tunamsihi Yeye —Ametukuka Yeye —kuwakinga wao kupitia uwezo wa Majeshi Yake, kuwalinda kupitia nguvu za Mamlaka Yake, na kuwasaidia kupitia nguvu Zake zisizoshindwa ambazo hutawala juu ya vitu vyote vilivyoumbwa. Mamlaka ni ya Mungu, Muumba wa mbingu na Bwana wa Ufalme wa Majina.*

***—Bahá'u'lláh***

*© Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabaha'i wa Tanzania*

Uhakiki wa Tafsiri ya Kiswahili:

Kamati ya Uhakiki wa Tafsiri ya Kiswahili ya Kitaifa
ya Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabaha'i wa Tanzania

Kimechapishwa mwaka 2023 na Baraza la Kiroho la Kitaifa

S.L.P 585
Dar Es Salaam, Tanzania
secretariet@bahai.or.tz

## *Yaliyomo*


Utangulizi 1

1. Asili ya Asasi ya Mikono wa Hoja 3
2. Mikono wa Hoja katika Kipindi cha Baha'u'lláh 7
3. Mikono wa Hoja katika Kipindi cha 'Abdu'l-Bahá 13
4. Mikono wa Hoja katika Kipindi cha Shoghi Effendi 19
5. Mikono wa Hoja Walioteuliwa kwa Makundi 35
6. Huduma ya Mikono wa Hoja Baada ya Shoghi Effendi 91
7. Huduma ya Mikono wakati a Nyumba ya Haki ya Ulimwengu 105
8. Simulizi za Baadhi ya Mikono wa Hoja 111

## *Utangulizi*

Utawala wa Imani ya Kibahá'i kama ulivyoasisiwa na Baha'u'lláh hutiririka kuwafikia waumini kupitia mikondo miwili ya asasi zenye mwingiliano wenye kukamilishana ambao kwa pamoja hufuma mfumo thabiti wa utawala. Mkondo mmoja huundwa na asasi za watawala na wa pili huundwa na asasi za washauri au wasomi. Asasi ya juu kabisa ya kiutawala ni Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ambayo chini yake kuna Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa ambayo ni asasi ya kiutawala ya juu katika kila nchi. Chini ya Mabaraza ya Kitaifa kuna Mabaraza ya Kiroho ya Mahali ambayo ndiyo asasi za kiutawala katika kila kijiji au mji wenye Wabahá'i watu wazima tisa au zaidi.

Kwa upande wa asasi za washauri, chini ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kuna Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa. Chini yake kuna asasi ya Halmashauri za Washauri wa Bara ambazo chini yake kuna asasi ya Washauri Wasaidizi na wasaidizi wao. Wajumbe wa asasi za kiutawala huchaguliwa na waumini katika maeneo husika kwa utaratibu maalum uliowekwa na Baha'u'lláh. Wajumbe wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu huchaguliwa na wawakilishi wa nchi zote zenye Mabaraza ya Kitaifa kila baada ya kipindi cha miaka mitano. Lakini wajumbe wa Mabaraza ya Kitaifa huchaguliwa kila mwaka na wawakilishi wa waumini kutoka sehemu zote za nchi husika. Na pia wajumbe wa Mabaraza ya Mahali huchaguliwa na waumini watu wazima wakazi wa kijiji au mji husika. Kwa upande mwingine wajumbe wote wa asasi zote za washauri huteuliwa. Wajumbe wa Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa pamoja na wajumbe wa Halmashauri za Washauri wa Bara huteuliwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu lakini Washauri wasaidizi huteuliwa na Halmashauri za Washauri wa Bara.

Na pia washauri wasaidizi huteua wasaidizi wao wajulikanao kama Wasaidizi wa Washauri wasaidizi au kwa kifupi Wasaidizi. Mkondo wa ushauri ulianzishwa na Baha'u'lláh Mwenyewe, kwa kuteua Mikono wa Hoja. Utaratibu huu ukaendelezwa na 'Abdu'l-Bahá na baada yake Shoghi Effendi. Nyumba ya Haki ikaendeleza mkondo huu kwa kuanzisha Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa na Halmashauri za washauri wa bara. Kitabu hiki kitakusaidia kuelewa jinsi mfumo huu wa utawala wa Kibahá'i ulivyotokea hatua kwa hatua toka/tangu wakati wa uongozi wa Mwasisi wake hadi wakati huu wa zama za utungo/ujenzi.

Kadiri tunavyoendelea kujifunza mada kadhaa katika Imani ya Kibahá'i aghalabu tumeendelea kukutana au pengine kusikia matumizi ya msamiati Mkono wa Hoja ya Mungu. Mara nyingi tunapata maelezo machache tu kuhusu roho hizi zilizojulikana kama Mikono wa Hoja, walakini huwa tunabaki na hamu ya kujua zaidi juu ya maisha yao pamoja na asasi waliyoitumikia na vile vile mchango wao katika historia ya maendeleo ya Hoja. Hili hapa ni jaribio mojawapo la kukidhi kiu hii, na kwa vyovyote vile kitabu hiki hakiwezi kutosheleza kukupa kila kitu kuweza kupata uelewa kamili uhitajikao kuhusu asasi hii na kiwango kisichopimika cha mchango wao katika ukunjukaji wa maendeleo ya Hoja toka/tangu siku zake za mwanzoni hadi katika kipindi hiki. Ni matumaini yetu kuwa umaizi utakaoupata kutokana na usomaji wako juu ya mchango wa waumini hawa, upendo wao kwa Hoja na uthabiti wao katika Agano la Mungu utakusaidia kuongeza utambuzi wako juu ya nguvu ya Agano la Baha'u'lláh. Tukitambua kuwa huu ni ufupisho tu wa kile kilichotekelezwa na roho hizi zilizojitoa wakfu, tunakushauri kuendelea kuchunguza vyanzo vingine ili kupata uvuvio zaidi juu ya huduma yao iliyotukuka kwa hoja ya Mungu.

Kitabu hiki kinakupa vionjo juu ya maisha ya kila mmojawapo wa roho hizi pamoja na huduma yao kwa hoja wakiwa wajumbe wa asasi muhimu katika ukunjukaji wa Utaratibu wa Utawala wa Baha'u'lláh. Kipindi cha kati ya 1957 hadi 1963 kimeangaziwa mahsusi kuonesha uthabiti wa asasi ya Mikono wa Hoja wakati ilipolazimika kuongoza Hoja ya Baha'u'lláh baada ya kunyang'anywa ghafla kiongozi wao mpendwa.

Mwishoni utaweza kuona kiwango chao cha utiifu kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na jinsi walivyoshiriki kusimamia mchakato wa uundwaji wake kwa kufuata maandiko ya Baha'u'lláh. Kwa uamuzi na maelekezo ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu utagundua jinsi asasi ya Mikono wa Hoja ilivyokuwa mbegu iliyoota na kuchipuka kuwa shirika la washauri. Hivyo, utagundua kuwa majukumu yaliyokuwa yakitekelezwa na Mikono wa Hoja, kwa sasa yanaendelea kubebwa na asasi ya Washauri. Kama nyongeza, mwishoni kuna simulizi chache kutoka kwa baadhi ya Mikono wa Hoja ambazo zitaweza kuvuvia roho zetu ili kujitoa wakfu maisha yetu kwa ajili ya huduma kwa Hoja.

# 1

## ASILI YA ASASI YA MIKONO WA HOJA

Ni mara nyingi umesikia au kusoma msamiati ‘Mkono wa Hoja ya Mungu’ au ‘Mkono wa Imani’ au kwa kifupi ‘Mkono wa Hoja’ au ‘Mkono’ na hivyo sio maneno mageni kwako. Mikono wa Hoja walikuwa ni waumini thabiti katika historia ya Imani ya Kibahá’i walioteuliwa na kupewa hadhi hiyo na Baha’u’lláh Mwenyewe na baadaye ‘Abdu’l-Bahá na Shoghi Effendi wakati wa vipindi vyao wakiwa Wakuu wa Imani ya Kibahá’i. Baada ya kifo cha Mlinzi Shoghi Effendi hapakuwa tena na uteuzi wa Mikono wa Hoja. Hivyo, kwa sasa hakuna Mkono wa Hoja yeyote aliye hai hapa duniani. Wote walikwishatangulia kwenye ufalme wa Abhá. Baha’u’lláh Mwenyewe ndiye alikuwa mwanzilishi wa asasi hii ya Mikono wa Hoja ya Mungu. Katika kipindi Chake akiwa hapa duniani aliteua wachache kati ya wafuasi Wake waaminifu waliokuwa wanaitumikia Hoja Yake kwa uthabiti na akawaita Mikono wa Hoja ya Mungu. Hiki kilikuwa ni kipindi cha kuelekea mwisho wa maisha Yake hapa duniani, kati ya mwaka 1887 hadi 1892. Hawa wote walikuwa ni waumini waliokuwa wanaishi nchini Iran kwa wakati huo. Bila shaka ni kwa sababu Hoja Yake ilianzia huko na idadi kubwa ya waumini wa mwanzoni walikuwa nchini humo. Ilikuwa ni mnamo mwaka 1887 ndipo kwa mara ya kwanza alilitaja hilo jina la Mikono wa Hoja ya Mungu (kwa kiarabu “Ayadi’ Amru’llah”). Katika waraka aliomwandikia Ibn Asdaq, ambaye baadaye alimteua kuwa Mkono wa Hoja, Baha’u’lláh alikuwa anamuomba Mungu ***“kuwathibitisha wateule hawa, roho hizi ambazo ni Mikono wa Hoja ambao wamepambwa kwa joho la ufundishaji na wameinuka kuihudumia Hoja”***. (1)

Pia katika “Waraka wa Dunia” Alieleza daraja la huduma ya Mikono wa Hoja:

*“Mwangaza na utukufu, salaam na sifa viwe juu ya Mikono wa Hoja Yake, ambao kupitia kwao mwangaza wa stahamala unang’aa na ukweli umesitawishwa kwamba mamlaka ya kuteua yanakuwa ni kwa Mungu,*

*Mwenye uwezo, Mwenye nguvu, Asiyezuilika, ambao kupitia kwao bahari ya fadhili imesukumwa na manukato ya upendeleo wenye neema ya Mungu, Bwana wa jamii ya binadamu, yamesambazwa. Tunamsihi Yeye- Ametukuka Yeye – kuwakinga wao kupitia nguvu ya majeshi Yake, kuwalinda kupitia uwezo wa utawala Wake na kuwasaidia kupitia nguvu Yake isiyoshindwa ambayo hushinda vitu vyote vilivyoumbwa. Mamlaka yote ni ya Mungu, Muumba wa mbingu na Bwana wa Ufalme wa Majina."* *(2)*

Na katika Maandiko mengine Baha'u'lláh anawarejelea Mikono wa Hoja kuwa watainuliwa ili kumsaidia katika kuendeleza Hoja Yake na pia anataja majukumu yao katika kuunganisha na kuilinda Imani ya Kibahá'i. Vile vile kama uthibitisho na mwendelezo wa asasi hii, katika Wasia na Agano la 'Abdu'l- Bahá kuna aya nyingi zinazohusu Mikono wa Hoja ambazo huweka wazi daraja lao, majukumu yao, pamoja na nasaha kadhaa kuhusu utendaji wao na mwenendo wao. Pia katika hati hiyo, kwa uwazi 'Abdu'l –Bahá anampa mrithi Wake mamlaka ya kuteua na kuwaongoza Mikono wa Hoja ya Mungu.

*"Heshima na sifa, Baraka na utukufu…viwe juu ya Mikono wa Hoja ya Mungu ambao wametawanya mbali Manukato Matakatifu, wametamka Uthibitisho Wake, wametangaza Imani Yake, wamechapisha Sheria Yake nchi za ng'ambo, wakijitenga wenyewe kutoka vitu vyote isipokuwa Yeye, wakisimama kwa haki katika hii dunia, na kuwasha Moto wa Upendo wa Mungu ndani ya mioyo na roho za watumishi Wake; ….Mikono wa Hoja ya Mungu lazima wakati wote wawe macho na wakikuta yeyote anaanza kwenda kinyume na kumpinga Mlinzi wa Imani ya Mungu ni kumuondoa haraka kutoka kwenye kundi la watu wa Bahá na kamwe wasikubali kisingizio chochote kutoka kwake ….*

*Majukumu ya Mikono wa Hoja ya Mungu ni kusambaza Manukato Matakatifu, kuadilisha roho za watu, kuendeleza ujifunzaji, kuboresha tabia za watu wote na kuwa, wakati wote na katika hali zote waliotakasika na waliojitenga kutoka vitu vya kidunia. Lazima wadhihirishe hofu/kicho cha Mungu kwa mwenendo wao, tabia zao, vitendo vyao na maneno yao. Asasi hii ya Mikono wa Hoja ya Mungu ipo chini ya uongozi wa Mlinzi wa Imani ya Mungu. Lazima bila kukoma awahimize wajaribu na kujitahidi*

*kadiri ya uwezo wao kutawanya ladha tamu ya Mungu, na kuongoza watu wote wa dunia, kwa kuwa ni mwanga wa Uongozi Mtakatifu ambao husababisha ulimwengu mzima kuangaziwa. Kupuuzia, japo kwa kitambo, amri hii kamilifu ambayo inamfunga kila mmoja hairuhusiwi kabisa, kwamba uso wa dunia uweze kuwa wa kimbingu, kwamba kushindana na ugomvi miongoni mwa watu, ndugu, mataifa na serikali vitatoweka, kwamba wakazi wote wa duniani watakuwa ukoo mmoja na mbari moja na kwamba dunia itakuwa kama vile nyumba moja.* (3)

Katika kipindi cha miongo mitatu ya uongozi wa Shoghi Effendi kama Mlinzi wa Imani, yeye, licha ya kuteua idadi kubwa ya Mikono wa Hoja lakini pia aliinua huduma ya waumini hawa kuwa ya muundo wa asasi kamili. Kati ya mwaka 1951 na 1957 alifanya mambo manne makubwa ili kuimarisha asasi hii. Kwanza, aliteua Mikono wa Hoja wengi. Katika kipindi hicho tu aliteua Mikono wa Hoja 32. Lakini hadi kufika mwaka 1957 wakati wa kifo chake idadi ya Mikono waliokuwa hai na wakihudumu ilikuwa 27. Pili, kila Mkono wa Hoja alipangiwa eneo la huduma katika mojawapo ya mabara matano ya dunia. Kila bara lilipata idadi kadhaa ya Mikono wa Hoja waliokaa na kuhudumia humo. Mikono waliokuwa katika bara moja walianza kutoa huduma kwa ushirikiano wakijiona kama wajumbe wa asasi moja. Tatu, aliwateua wanne kati yao kukaa Makao Makuu ili kumsaidia kazi ya kuratibu shughuli za Mikono waliokuwa wakihudumu katika kila bara. Utaratibu huu ulirahisisha sana mawasiliano kati ya Mlinzi wa Hoja na Mikono waliokuwa sehemu mbalimbali za dunia. Pia walianza kupata ufahamu wa maendeleo na uratibu wa shughuli za Imani kidunia. Nne, aliwaelekeza Mikono wa Hoja kuteua bodi mbili za usaidizi kwa kila bara, moja ya ulinzi na nyingine ya uenezaji, ili kuwasaidia Mikono wa Hoja waliokuwa wakihudumia kwenye mabara hayo. Wajumbe wa bodi hizi wakawa ndio wasaidizi wa Mikono wa Hoja katika maeneo yao ya huduma na wakajulikana kama Washauri Wasaidizi. Zaidi ya hayo, alianzisha mifuko ya bara kwa ajili ya kugharamia shughuli za Mikono wa Hoja na wasaidizi wao, na kwa kila bara akamteua mmoja wa Mikono wa Hoja katika bara hilo kuwa mdhamini wa mfuko huo. Hatua hizi ziliimarisha sana utendaji wa Mikono wa Hoja na ukawa wa kiasasi. Katika ujumbe wa kuwateua Mikono 8 wa mwisho, Oktoba 1957, aliwatambulisha Mikono wa Hoja kama "Wasimamizi Wakuu wa Jumuiya Changa ya Ulimwengu ya Baha'u'lláh''. Lakini huduma muhimu kabisa na ya kihistoria ya Mikono wa Hoja ilikuwa ni wakati wa kipindi cha miaka

takribani mitano na nusu baada ya kifo cha ghafla cha Mlinzi Shoghi Effendi. Hii ilikuwa ni kati ya Novemba, 1957 hadi Aprili 1963. Huduma yao ilijumuisha mambo makuu matatu ya kihistoria: i) kuwa wasimamizi wakuu wa Imani ii) kuukamilisha mpango wa miaka kumi wa ufundishaji ulioanzishwa na Mlinzi na iii) kusimamia uchaguzi na kuisimika Nyumba ya Haki ya Ulimwengu mwaka 1963. Wakiwa watawala, waliilinda Imani dhidi ya maadui na kudumisha umoja wa Wabahá'i duniani kote, waliongoza juhudi za ufundishaji na uundaji wa mabaraza ya kiroho ya vijiji na kitaifa katika mabara yote na mwishowe wakasimamia mchakato wa uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kama ilivyokuwa imeamriwa na Baha'u'llah katika Maandiko Yake miaka kadhaa kabla. Katika kutimiza majukumu haya, walichagua tisa kati yao kukaa na kusimamia kazi za kiutawala huko Makao Makuu ya Imani mjini Haifa kama zilivyokuwa zikifanywa na Mlinzi; na wengine wakiendelea kuongoza juhudi za ufundishaji katika mabara yote ili kukamilisha Mpango wa Miaka Kumi. Japo kwa ujumla Mikono wa Hoja walioteuliwa idadi yao ni hamsini, lakini Shoghi Effendi na hata baadaye Nyumba ya Haki imesema kuwa kuna uwezekano wa kuwa zaidi ya hao, lakini kwa sasa wanaojulikana ni hao kwani mazingira ya Iran hayajaruhusu kufanyika kwa utafiti wa kina zaidi wa historia ya Imani nchini humo

# 2

## MIKONO WA HOJA KATIKA KIPINDI CHA BAHA'U'LLÁH

Katika kipindi cha utume Wake akiishi hapa duniani Baha'ulláh aliteua Mikono wa Hoja wanne. Hawa walikuwa ni kati ya waumini wa miaka hiyo ya mwanzoni waliofanya kazi kubwa ya kusimamisha Imani Yake, hasa katika nchi ya Iran. Hawa ni waumini ambao Alikuwa Anawapa majukumu kadhaa maalum katika kipindi hicho kigumu. Na waliendelea kuhudumia Hoja hadi wakati wa uongozi wa 'Abdu'l-Bahá na hata mmoja wao alihudumu mpaka kipindi cha uongozi wa Shoghi Effendi kwa miaka kama saba hivi. Majina yao ni:

1. Haji Mulla 'Ali-Akbar-i-Shahmirzadi, alijulikana pia kama Haji Akhund
2. Haji Mirza Muhammad Taqiy-i-Abhari, alijulikana pia kama Ibn-i-Abhar
3. Mirza Muhammad-Hasan, au Adibu'l-'Ulama, alijulikana pia kama Adib, na
4. Mirza 'Alí-Muhammad, alijulikana pia kama Ibn-i-Asdaq

### 1. Ali-Akbar-i-Shahmirzadi (Hájí Ákhund) (1842- 1910)



Alizaliwa mwaka 1842 huko Shahmírzád, Iran. Alipata elimu ya dini ya kiislamu katika vyuo mbalimbali nchini Iran na alitambulika na kuheshimika

kwa usomi wake katika dini. Aliamini na kuikubali Imani baada tu ya kusoma **Kitabu Yakini** mnamo mwaka 1861. Haji Akhund alifungwa mara tano kwa ajili ya Imani katika vipindi tofauti tofauti na alikuwa mmoja wa waumini waliofundisha na kuwezesha idadi kubwa ya watu kuwa Wabahá'i nchini Iran katika kipindi hicho kigumu. Alisafiri kwenda Nchi Takatifu na kukutana na Baha'u'lláh mara tatu – mwaka 1871, 1882 na 1889. Na kutokana na uaminifu wake mkubwa, Bahá'u'lláh alimpa jukumu kubwa na nyeti la kutunza na kuhamisha mabaki ya Mwili Mtakatifu wa Báb. Aliteuliwa na Bahá'u'lláh kuwa Mkono wa Hoja baada ya kukutana Naye mara ya mwisho. Mara ya mwisho alikwenda 'Akká kukutana na 'Abdu'lBahá mwaka 1894 na kwa ruhusa Yake alijaribu bila mafanikio kumshawishi mvunja- Agano mkuu Mirza Muhammad Ali kuacha uasi wake dhidi ya 'Abdu'l-Bahá. Alifariki mnamo mwaka 1910 mjini Tihrán baada ya yeye na Mikono wa Hoja wenzake kufanikisha kuunda Baraza la kwanza la mji wa Tihrán mwaka 1899.

## 2. Hájí Mírzá Muhammad-Taqíy-i-Abharí—(Ibn-i-Abhar) (1854-1917)




Alizaliwa mnamo mwaka 1854 kule Abhar. Aliamini na kuwa mfuasi wa Baha'u'lláh mwaka 1868, baada ya kuwa Mbabi kwa miaka kadhaa. Kuna sehemu fulani katika Maandiko, ambapo Bahá'u'lláh humtaja Hájí Mírzá Muhammad-Taqíy-i- Abharí kuwa aliumbwa kutukuza Sifa na Utukufu wa Mungu. Baha'u'lláh alimteua kuwa Mkono wa Hoja mnamo mwaka 1886**.** Kwa miaka minne (1890-1894) alipata baraka ya kufungwa ndani ya gereza la Siyal-Chal akifungwa kwa minyororo ile ile aliyofungwa Bahá'u'lláh mwaka 1852. Katika kipindi cha 'Abdu'l-Bahá alitumwa kwenda kufundisha Imani katika nchi za Uturuki na India, na kwa ruhusa ya 'Abdu'l-Bahá alifanya safari 11 kwenda Nchi Takatifu. Ibn-i- Abhar alikuwa kati ya waumini waliopokea nyaraka nyingi kutoka kwa Baha'u'lláh zikiwapa miongozo mbalimbali. Wakati fulani alimuomba Baha'u'lláh ampe

mwongozo wa sehemu gani akaishi nchini Iran. Baha'u'lláh kwa kutaka kumfundisha umuhimu wa ushauriano alimjibu kuwa aende akashauriane jambo hilo na waumini wenzake walio thabiti na jibu litakalotokana na ushauriano huo ndilo alitekeleze. Huduma yake kubwa ilikuwa ni juhudi yake ya kuendeleza elimu ya wanawake. Yeye na mke wake walikuwa na mchango mkubwa katika kuinua elimu ya wanawake katika jamii ya Waajemi. Hájí Mírzá Muhammad-Taqíy-i-Abhari alifariki mwaka 1917.



*Mírzá Muhammad-Taqíy-i- Abhari akiwa amefungwa minyororo akipelekwa gerezani*

### 3. Haji Mírzá Hasan, (Adib) (1848- 1919)



Alizaliwa Talaqán, Iran, mwaka 1848. Alipata elimu ya dini ya kiislam mjini Tehran na Mashhad. Wakati akiwa kijana alipewa kazi ya kuwa mwandishi wa vitabu wa mwana mfalme. Na kwa kuwa alikuwa msomi wa dini ya kiislamu wakati fulani alipewa nafasi ya kuwa imam wa msikiti wa Ijumaa mjini Tehran. Aliikubali Imani na kuwa Mbahá'i mnamo mwaka 1889 baada ya kufundishwa imani na kuitafiti kwa kusaidiwa na Nabil-i-Akbar. Baada ya hapo alifukuzwa kazi yake ya uandishi kwa mwana mfalme. Bahá'u'lláh

alimteua kuwa Mkono wa Hoja ya Mungu ndani ya kipindi cha mwaka mmoja tangu alipoikubali imani Yake. Tofauti na Mikono wa Imani wengine wa kipindi hicho yeye hakupata baraka ya kukutana na Baha'ulláh katika maisha yake bali baadaye alipata bahati ya kukutana na 'Abdu'l-Bahá huko 'Akká. Alijishughulisha sana na kufundisha elimu ya dini kwa vijana na pia alikuwa mmoja wa waanzilishi wa shule za Tarbiyat mjini Tihrán, shule ambazo zilikuja kuwa maarufu na kuenea katika nchi nzima ya Iran kwa miaka hiyo. Vile vile aliandika machapisho na vitabu kadhaa vya historia na uthibitisho wa Imani. Wakati wa kipindi cha 'Abdu'l-Bahá alishughulika sana kuzima upinzani wa wavunja- Agano na juhudi zake za ufundishaji zilipelekea uanzishwaji wa Baraza la Kiroho la Wabahá'i wa Iran (la kwanza) ambalo alichaguliwa kuwa mjumbe. Alifariki tarehe 2 Septemba, 1919 mjini Tihrán baada ya kurejea kutoka safari ndefu ya ufundishaji huko India na Burma kwa maelekezo ya 'Abdu'l-Bahá. (4)

## 4. Aqá Mírzá 'Alí-Muhammad (Ibn-i-Asdaq) - Shahíd Ibn-i-Shahíd (1850- 1928)



'Mfa kishahidi, mwana wa Mfa kishahidi' aliyezaliwa Mashhad mwaka 1850. Baba yake alikuwa Mullá Sádiq-i- Muqaddas au Ismu'llahu'-Asdaq ambaye aliifia kishahidi Imani ya Báb (ambaye baadaye naye alikuja kupewa daraja la Mkono wa Hoja na 'Abdu'l-Bahá akiwa amekwishafariki). Akiwa bado mdogo alifungwa gerezani pamoja na baba yake katika gereza la Siyah-Chal mjini Tihrán kwa sababu ya kuwa wafuasi wa Báb. Akiwa bado kijana mdogo aliambatana na baba yake kwa safari ndefu ya kwenda Baghdád ambako alipata baraka ya kufika mbele ya Baha'u'lláh. Ni kutoka wakati huo ndipo alivutiwa mno na wajihi Wake na kujenga imani thabiti kwa Baha'u'lláh. Miaka kadhaa baadaye akiwa mfuasi thabiti wa Baha'u'lláh alimuomba mara

nyingi awe kifo cha kishahidikama baba yake. Baha'u'lláh alimjibu kuwa ''**katika kipindi hiki kitendo kikuu kuliko vyote ni huduma kwa Imani... na ufia dini hauna maana ya mtu kujitolea kufa na kumwaga damu kwa ajili ya dini tu, bali hata mtu ambaye anapata baraka ya kuishi akifurahia maisha ya huduma anaweza kuwa na daraja la ufia dini**''.

Baadaye kutokana na huduma yake kubwa kwa Imani mwaka 1882 Baha'u'lláh alimpa daraja la mfia dini akamuita mfa kishahidi, mwana wa mfa kishahidi yaani 'shahid bin Shahid' (kwa Kiarabu). Vile vile Ibn-i-Asdaq alikuwa mtu wa kwanza kupewa daraja la Mkono wa Hoja ya Mungu na Baha'u'lláh mwaka 1887. Ni katika waraka mmojawapo Aliomwandikia Ibni-Asdaq, ndimo Baha'u'lláh alipofunua sala maarufu ya *'Heri pahali, na nyumba, na mahali ……..*'' Hii ilikuwa ni majibu baada ya yeye kumjulisha Baha'u'lláh kuwa waumini wa Tihrán walikuwa wanataka kutekeleza sheria ya Mashriqu'l-Adhkar lakini hawakuwa na Nyumba za Ibada. (Baha'u'lláh alikuwa amewaagiza waumini kwenda kwenye Nyumba za Ibada na kufanya sala za alfajiri; lakini kwa kuwa wakati huo hakukuwa na Nyumba za Ibada za Kibahá'i walikusanyika katika nyumba za waumini wenzao na kufanya ibada pamoja kila alfajiri). Baada ya kupokea waraka huo kutoka kwa Baha'u'lláh, Ibn-i-Asdaq aliupeleka kwa waumini wenzake wa Tihrán na walifurahi na kuzidisha mikusanyiko hiyo ya sala za alfajiri. Kwa hiyo, na wao wakaonekana kuwa walikuwa ni watu wanaofanya ibada kama walivyokuwa wenzao waislamu. Wakati wa kipindi cha 'Abdu'l-Bahá alipewa kazi maalum ya kufundisha watu mashuhuri na watawala. Licha ya kufundisha kada hiyo nchini Iran, alisafiri hadi India, Burma naTurkistan na mnamo mwaka 1920 'Abdu'l-Bahá alimpa yeye na Ahmad Yazdani waraka maalum ulioitwa '*'Waraka wa the Hague''* kuuwasilisha kwa 'Shirika la kuleta Amani ya Kudumu' huko mjini The Hague, Uholanzi. Na pia alihusika kwa kiasi kikubwa katika mipango ya ujenzi wa Nyumba ya Ibada ya kwanza ya Kibahá'i ya Ishqábád. Alikuwa ni mmoja wa Mikono wa Hoja wa mwanzoni aliyeishi na kuhudumia Imani tangu wakati wa Baha'u'lláh hadi wakati wa Mlinzi Shoghi Effendi. Alifariki na kuzikwa mjini Tihrán mwaka 1928. (5)


# 3

## MIKONO WA HOJA KATIKA KIPINDI CHA 'ABDU'L-BAHÁ

Baada ya 'Abdu'l-Bahá kuachiwa uongozi wa Imani, Aliongoza shughuli za Mikono waliokuwa wameteuliwa na Baba Yake. Kwa maelekezo Yake walifanya kazi kubwa ya kuzilinda jumuiya za Wabahá'i wa Iran dhidi ya uasi wa Mirza Muhammad Ali na wavunja-agano wenzake waliojaribu kuleta mifarakano. Pia walifanya kazi kubwa kuwezesha uundwaji wa asasi ya kuchaguliwa. Mwaka 1897 'Abdu'l-Bahá aliwaelekeza Mikono wa Hoja (ambao wote walikuwa wanaishi Iran) kuunda asasi ya ushauriano miongoni mwao pamoja na walimu wengine mashuhuri waliokuwa wanaishi Tihrán wakati huo. Mnamo 1899 walifanikiwa kuunda asasi ya kwanza kabisa ya kuchaguliwa ya Kibahá'i duniani ambapo Mikono wote walikuwa wajumbe. Asasi hii ilijulikana kama 'Baraza Kuu la Tihrán' na huchukuliwa kama Baraza la kwanza la Mahali kuundwa, japo wakati huo halikujulikana kwa jina hilo. Kama mwendelezo wa jukumu aliloachiwa na Baba yake, baadaye 'Abdu'l-Bahá pia Aliwataja Mikono wa Hoja. Aliwapa heshima na kuwataja kama Mikono wa Hoja baadhi ya Wabahá'i waliokuwa thabiti na walimu mashuhuri katika kipindi cha Baba Yake wakati wao wenyewe walikuwa wamekwishafariki. Waumini hao ambao 'Abdu-l-Bahá katika Kipidi Chake aliwapa daraja hilo akiwa mkuu wa Imani kati ya mwaka 1892 hadi 1921 walikuwa pia wanne. Hawa wote aliwatangaza kuwa walikuwa Mikono wa Hoja wakati wamekwishafariki na wote walikuwa ni waumini wa Irán. Walikuwa wafuatao:

1. Aqa Muhammad-i-Qa'ini, akijulikana pia kama Nabil-iAkbar
2. Mirza 'Ali-Muhammad-i-Varqa, mfa kishahidi
3. Shaykh Muhammad-Riday-i-Yazdi, na
4. Mulla Sadiq-i-Muqaddas, aliyepewa jina la Ismu'llahu'l-Asdaq

## 1. Aqa Mohammad-i-Qa’ini (Nabil-i-Akbar) (1829- 1892)



Nabil-i-Akbar alizaliwa huko Qa’ini, Irán mnamo mwaka 1829. Alipata elimu ya dini, na ya nyanja zingine za elimu zilizothaminiwa sana kwa wakati huo. Alikuwa msomi aliyeheshimika sana na viongozi wa dini, watawala na watu wa kawaida. Baada ya kupata mwanga wa mafundisho ya Imani mpya ya Báb aliikubali na kuwa muumini thabiti, na baadaye alipata baraka ya kufika mbele ya Baha’u’lláh kipindi kile alipokuwa Baghdád. Alikuwa ni kati ya waumini wachache waliolitambua daraja la Baha’u’lláh baada ya kufika mbele Yake na kusikiliza Mafundisho Yake katika kipindi kile kabla hajajitangaza kuwa ndiye Mdhihirishaji Aliyekuwa anasubiriwa. Wengi waliopata nafasi ya kumsikiliza Nabil-i-Akbar waliamini kuwa hakukuwa na msomi wa dini mwenye uwezo na kipaji kama yeye katika nchi ya Irán wakati huo. Kwa kutumia elimu yake na uwezo wake mkubwa aliweza kufundisha na kuwawezesha watu wengi wa aina tofauti tofauti kuwa wafuasi wa Imani ya Baha’u’lláh. Baha’u’lláh aliandika waraka aliouita ‘*Waraka wa Hekima*’ kwa ajili yake. Alisafiri sehemu mbalimbali ndani ya Irán na Ishqábád na Bhukara ili kueneza ujumbe wa Baha’u’lláh. Alifariki mnamo mwaka 1892 huko Bhukara, Uzbekistan. Alitajwa na ‘Abdu’l-Bahá kama Mkono wa Hoja miaka kadhaa baada ya kuwa amekwishafariki.

## 2. Mirza 'Ali-Muhammad-i-Varqa, kifo cha kishahidi (1855- 1896)




Ali-Muhammad-i-Varqa alizaliwa mwaka 1855 huko Yazd, Irán. Alisomea utaalam wa mashairi na tiba za asili za kiajemi. Alikuwa mmoja wa wafuasi wa mwanzoni wa Baha'u'lláh. Alijaaliwa kupata watoto watatu; Azizu'lláh, Ruhu'lláh na Valliyu'lláh. Mke wake na mama mkwe wake walikuwa waislamu waliokuwa wanaichukia sana Imani ya Kibahá'i, lakini pamoja na hayo aliweza kuwafundisha na kuwafanya watoto wake kuwa Wabaha'i thabiti tena tangu wakiwa bado na umri mdogo. Ruhu'lláh, akiwa mtoto wa miaka 7 hivi alipata baraka ya kufika mbele ya Baha'u'lláh na kuongea Naye akiwa ameambatana na baba yake. Muhammad Varqa alikuwa mmoja wa washairi maarufu nchini Irán na alitumia kipaji hicho na umaarufu wake kueneza Imani ya Baha'u'lláh. Ni kutokana na kipaji hicho cha ushairi na jinsi alivyokitumia kuwaleta watu kwenye Imani, kwamba Baha'u'lláh akampa jina la Varga ambalo humaanisha hua. Alikuwa mmoja wa walimu mashuhuri wa Imani wa wakati huo. Katika kipindi cha uhai wake alikwenda 'Akká mara tatu; mara mbili katika kipindi cha Baha'u'lláh ambapo alipata baraka ya kufika machoni Pake mwaka 1879 na 1891, na safari ya mwisho ilikuwa wakati wa 'Abdu'l-Bahá mwaka 1893. Katika safari zake mbili za mwisho aliandamana na watoto wake wawili wakubwa (Azizu'lláh na Ruhu'lláh) hali ambayo iliwapa watoto hao uthabiti mkubwa sana katika Imani. Aliuawa kifo cha kishahidi pamoja na mtoto wake wa miaka 12, Ruhu'lláh, mwaka 1896 wakiwa wafungwa gerezani mjini Tihrán kwa sababu walikataa kuikana imani yao kwa Baha'u'lláh. Wakati wa kuuawa kwao muuaji aliingia kwenye chumba cha gereza akawatenganisha Muhammad Varqa na mtoto wake Ruhu'lláh kutoka kwenye mnyororo uliokuwa umewafunga; akamuuliza Varqa ''unataka nikuue wewe kwanza au mtoto wako kwanza" Varqa akajibu ''utakavyopenda wewe''. Yule muuaji akachukua nyengo akamchana tumbo na kuvuta utumbo wake nje kwa kutumia nyengo hiyo, na wakati utumbo na damu vikianza kutiririka chini yule muuaji akamwangalia usoni na kumuuliza ''unajisikiaje sasa", Varqa akajibu huku akitabasamu "najisikia vizuri kuliko wewe". Hapo wauaji wote kwa pamoja wakamvamia kwa hasira na kumkatakata vipande vipande mbele ya mtoto wake na baadaye wakamnyonga mtoto wake. Hivyo ndivyo Varqa na mtoto wake Ruhu'lláh walivyokufa kishahidi. Baadaye 'Abdu'lBahá alikuja kumtangaza kuwa Mkono wa Hoja.



*AIi Muhammad Varqa na mtoto wake Ruhu'lláh wakiwa gerezani kabla ya kuuawa*

## 3. Shaykh Muhammad-Riday-i-Yazdi (1814-1897)



Muhammad-Riday-i-Yazdi alizaliwa katika familia maarufu jimboni Yazd mwaka 1814, na alipata elimu ya kidini katika vyuo maarufu vya kidini vya eneo hilo. Alikubali na kuwa mfuasi wa Báb katika siku za mwanzoni za Utume Wake. Alimtambua Baha'u'lláh hata kabla ya kujitangaza mara baada ya kusoma waraka Wake aliouandika akiwa kwenye milima ya Suleimaniya. Alikuwa mwalimu mahiri wa Imani ambaye alitumia kila fursa kufundisha Imani. Kutokana na elimu na ujuzi wake alifanikiwa kuwabadilisha viongozi na walimu kadhaa wa dini ya kiislamu kuwa Wabahá'i. Mara nyingi alitumia vifungu vya maandiko kutoka kitabu cha Qur'án kuwasadikisha wasikilizaji wake. Japo alipata mateso mengi kutoka kwa wapinzani wa Imani lakini hakukata tamaa. Baada ya mateso mengi na kufungwa mara kadhaa, alifariki akiwa gerezani mjini Tihrán mwaka 1897. Alitajwa na 'Abdu'l-Bahá kuwa Mkono wa Hoja wakati akiwa amekwishafariki.

## 4. Mulla Sadiq-i-Muqaddas (Ismu'llahu'l-Asdaq) (haijulikani–1889)



Mulla Sadiq-i-Muqaddas alizaliwa mjini Mashhad nchini Irán lakini mwaka wake wa kuzaliwa haujulikani vizuri. Alikuwa mwanafunzi wa Siyyid Kazim ambaye baadaye mwaka 1843 alikutana na mtukufu Báb. Lakini ilikuwa baadaye alipokutana na Mulla Hussein ndipo alipolitambua daraja la Báb na hivyo akamuamini na kuwa Mbábi. Alihamia Shiráz na kuanza kufundisha Imani mpya kwa nguvu sana, akiwa pamoja na Quddus. Alikuwa mmoja wa Wabábi waliozingirwa kwenye ngome ya Sheikh Tarbasi, lakini mwishowe alifanikiwa kutoroka. Baadaye akiwa Mbábi alipata baraka ya kufika mbele ya Baha'u'lláh mwaka 1860 kule Baghdad na kuamini kuwa huyo ndiye Mungu Alikuwa Amemdhihirisha. Baadaye alikamatwa na kufungwa kwenye gereza la Siyah-chal. Akiwa gerezani humo alimfundisha na kumfanya kuwa muumini wa Imani daktari wa gereza hilo aliyeitwa Hakim Masih, huyu ndiye alikuwa Mbahá'i wa kwanza mwenye asili ya Kiyahudi. Kwa kipindi fulani baada ya kutoka gerezani alipewa jukumu la kutunza mabaki ya mwili wa Mtukufu Báb. Vile vile alimtembelea Baha'u'lláh kule 'Akká mwaka 1874 na baada ya hapo akapewa jukumu la kuwafundisha Imani ndugu zake Báb (Afnan). Alifariki mwaka 1889 kule Hamadan, Irán baada ya kazi kubwa ya kufundisha Imani na mateso mengi kutoka kwa wapinzani wa Imani. Baadaye alitajwa na Abdu'l-Baha kama Mkono wa Hoja wakati amekwishafariki. Huyu ndiye alikuwa baba yake Ibn-i-Asdaq aliyekuwa wa kwanza kupewa daraja la kuwa Mkono wa Hoja na Baha'u'lláh. (6)

# 4

## MIKONO WA HOJA KATIKA KIPINDI CHA SHOGHI EFFENDI

Mamlaka ya Mlinzi ya kuteua Mikono wa Hoja ilitokana na Wosia na Agano la ‘Abdu’l-Bahá:……. ***Mikono wa Hoja ya Mungu lazima wachaguliwe na kuteuliwa na Mlinzi wa Imani ya Mungu.Wote lazima wawe chini ya kivuli chake na watii amri yake…”.*** Vile vile hati hiyo inaendelea kuonesha mamlaka ya Mlinzi juu yao, uhusiano wao pamoja na majukumu yake kwao “***Asasi hii ya Mikono wa Hoja ya Mungu ipo chini ya uongozi wa Mlinzi wa Hoja ya Mungu. Lazima bila kukoma awahimize wajaribu na kujitahidi kadiri ya uwezo wao kutawanya ladha tamu ya Mungu, na kuwaongoza watu wote wa dunia, kwa kuwa ni mwanga wa Uongozi Mtakatifu ambao husababisha ulimwengu mzima kuangaziwa***”. (7)

Hivyo ilikuwa wazi kuwa Mikono wa Hoja wakati wa Mlinzi walipaswa kuwa watiifu na chini ya uangalizi wake na pia walikuwa na wajibu wa kumsaidia kutawanya Mafundisho ya Mungu kwa watu wote. Ni yeye tu aliyekuwa amepewa mamlaka na kuteua Mikono wa Hoja.

Katika kipindi chake kama mkuu wa Imani (1921-1957) Shoghi Efendi aliteua jumla ya Mikono wa Hoja 42. Hawa waliteuliwa kwa nyakati na kwa namna tofauti tofauti. Baadhi aliwatangaza kuwa Mikono wa Hoja wakati wamekwishafariki, wengine aliwateua kwa makundi na wengine aliwateua mmoja mmoja kwa vipindi tofauti tofauti. Miaka michache baada ya kuchukua uongozi wa Imani, Shoghi Effendi kama Babu Yake, aliwatangaza waliokuwa waumini thabiti waliokuwa wametoa huduma kubwa katika maisha yao wakati wa uongozi wa ‘Abdu’l-Bahá, kuwa walikuwa Mikono wa Hoja. Hawa walitangazwa wakati wamekwishafariki kwa vipindi tofauti tofauti kuanzia mwaka 1925 hadi 1952. Idadi yao jumla ilikuwa 10· Kutokana

na Wasia huu, Shoghi Effendi alianza kuteua Mikono wa Hoja mwishoni mwa mwaka 1925. Utaratibu huu uliendelea kwa kuwataja Mikono wa Hoja waliokwishafariki hadi mwaka 1952. Wengi wa hawa walioteuliwa kipindi hicho walikuwa ni kutoka Amerika. Hawa wote 10 walitajwa kwa vipindi tofauti tofauti.

## Waliotangazwa baada ya kuwa wamekwishafariki

| Na | Jina La Mkono wa Hoja | Kuzaliwa | Kufariki | Kutangazwa—Mkono wa Hoja |
|---|---|---|---|---|
| 1 | John E. Esslemont | 1874 | 1925 | 30 Novemba 1925 |
| 2 | Haji Abdu'l-Hasan Amin | 1831 | 1928 | Julai 1928 |
| 3 | Keith Ransom-Kehler | 1876 | 1933 | 28 Oktoba 1933 |
| 4 | Martha Root | 1872 | 1939 | 02 Oktoba 1939 |
| 5 | 'Abdu'l-Jalil Bey Sa'd | H* | 1942 | 25 Juni 1942 |
| 6 | Siyyid Mustafa Rumi | H | 1942 | 14 Julai 1945 |
| 7 | Muhammad Taqi-i-Isfahani | H | 1946 | 15 Desemba 1946 |
| 8 | Louis Gregory | 1874 | 1951 | 05 Agosti 1951 |
| 9 | Roy C. Wilhelm | 1875 | 1951 | 23 Disemba 1951 |
| 10 | John Henry Hyde-Dunn | 1855 | 1941 | 26 Aprili 1952 |

*Tazama Kitabu: Ulimwengu wa Kibahái, cha Kiingereza, Toleo la XIV, 1963-1968, uk. 445-446 (H—maana yake mwaka haujulikani vizuri)


1. **John Esslemont,** (1874 -1925)



John Ebenezer Esslemont alikuwa Mbaha'i mashuhuri wa Scotland aliyezaliwa Aberdeen- Scotland, tarehe 19 Mei, 1874 katika familia mashuhuri ya eneo hilo, na alipata elimu yake hadi chuo kikuu cha Aberdeen ambapo alihitimu kama daktari mwaka 1898. Aliishi kwa muda nchini Australia na Afrika Kusini na baadaye alirudi nchini mwake mwaka 1908. Kwa mara ya kwanza alisikia juu ya Imani ya Kibahá'i kutoka kwa mke wa mfanyakazi mwenzake ambaye alikuwa Mbahá'i, mwaka 1914. Baada ya hapo alisoma vitabu mbalimbali juu ya Imani na ndani ya kipindi cha mwaka mmoja akawa Mbahá'i. Esslemont alikuwa na ujuzi mkubwa wa lugha na alijua lugha za Kifaransa, Kijerumani, Kihispania na Kiesperanto, na baada ya kuwa Mbahá'i alianza kujifunza kwa juhudi Kiajemi na Kiarabu. Ilimlazimu kwenda kuishi Irán kwa mwaka mmoja ili kupata umahiri katika lugha hizo za Kiajemi na Kiarabu.Wakati mmoja alisema kuwa alifanya hivyo ili aweze kutafsiri Maandiko ya Kibahá'i kwa lugha za Ulaya ikiwa ni njia mojawapo ya kueneza Imani katika bara hilo. Mwaka 1916 alianza kuandika kitabu chake maarufu cha 'Baha'u'lláh na Wakati Mpya'. Mwaka 1919 alienda Haifa baada ya 'Abdu'l-Bahá kumuomba aende na muswada wa kitabu hicho alichokuwa anaandika cha utambulisho wa Imani ya Kibahá'i. Alipata baraka ya kukutana na kukaa na 'Abdu'l-Bahá kwa miezi miwili ambapo aliongezewa elimu ya Imani ambayo ilimsaidia kuboresha kitabu chake baada ya 'Abdu'l-Bahá kukipitia na kuhakiki sura kadhaa alizokuwa tayari ameziandika. Aliendelea na kazi hii ya kuandika kitabu hicho hata baada ya kifo cha 'Abdu'l-Bahá. Alipokimaliza alimpelekea Mlinzi ambaye naye aliweka maoni yake na ndipo akakikamilisha na kikaweza kuchapishwa rasmi mwaka 1924. Hii ni mojawapo ya kazi zake za kukumbukwa sana. Kitabu hiki cha ''Baha'u'lláh na Wakati Mpya" kimetumika kuitambulisha Imani kwa watu wengi na kimekwishatafsiriwa katika lugha zaidi ya 60.

Kipindi hicho Esslemont aliishi mjini Bournemouth Uingereza ambapo aliwafundisha Imani watu wengi. Baada ya afya yake kuwa dhaifu Shoghi Effendi alimkaribisha kwenda kuishi Haifa. Alihamia Haifa Novemba 1924 na kutokana na ujuzi wake wa Kiingereza, Kiajemi na Kiarabu akawa anamsaidia Mlinzi kutafsiri kitabu cha "Maneno Yaliyofichwa" na 'Waraka wa Ahmad' kutoka Kiarabu na Kiajemi kwenda Kiingereza. Baadaye aliendelea kuwa msaidizi wa Mlinzi kama mwandishi wake wa lugha ya Kiingereza. Lakini afya yake iliendelea kuzorota na mwishowe mnamo Novemba 1925 alifariki dunia mjini Haifa na kuzikwa kwenye makaburi ya Wabahá'i. Mlinzi Shoghi Effendi katika barua iliyoelezea huduma yake kwa Imani alimtangaza John Esslemont kuwa Mkono wa Hoja. Hii ilikuwa Novemba 1925 akiwa ni muumini wa kwanza kutangazwa na Mlinzi kwa daraja hilo.

## 2. Haji 'Abdu'l-Hasan Amin (Haji Amin-i-llahi) (1831 - 1928)



Haji Amin au Haji 'Abu'l-Hasan Ardikani alizaliwa mnamo mwaka 1831/32 huko Ardikani kaskazini mwa Yazd nchini Irán. Mnamo mwaka 1851 alikutana na Mulla Mohammad Rida akampa mafundisho ya Mtukufu Báb kwa kina, akaamini na tangu hapo akawa Mbábi. Aliendelea kuwa Mbábi na kufundisha Imani hiyo hadi alipomwamini Baha'u'lláh baada ya kusikia habari Zake na kusoma Maandiko Yake. Mwaka 1869 alifanya safari yake ya kwanza kwenda 'Akká akawasilisha fedha na barua kutoka kwa waumini wa Irán kupitia kwa Mirza Aqa Jan (mwandishi wa Baha'u'lláh) kwa kuwa kipindi hicho hakuruhusiwa na walinzi wa gereza kufika mbele ya Baha'u'lláh. Kipindi kifupi baadaye alifanya safari nyingine na akafanikiwa kufika mbele ya Baha'u'lláh akiwa bado mfungwa kwenye gereza la 'Akká. Haji Amin alivutiwa sana na Utukufu wa Baha'u'lláh kiasi kwamba alipigwa na bumbuazi akaanguka chini akazimia na kuumia kwenye paji la

uso. Baadaye aliamua kutoa mali zake zote ziwe mali za Baha'ulláh na hivyo kubaki hana makazi wala mali yoyote. Sasa aliishi kwa kufanya biashara ndogo ndogo na kwa kulipwa ujira kidogo kwa kuwasaidia kuandika barua waumini waliokuwa hawajui kuandika. Baadaye Haji Amin akawa msaidizi wa Haji Shah-Muhammad Manshad ambaye Baha'u'lláh alikuwa amempa jukumu la kukusanya Huqúqu'lláh kutoka kwa waumini. Hii ilisababisha afanye safari nyingi katika mikoa yote nchini Irán. Baada ya kifo cha Haji Shah-Muhammad Manshad mwaka 1880, aliteuliwa na Baha'u'lláh kuwa mdhamini wa Huqúqu'lláh na ndipo akaanza kujulikana kama Haji Amin. Jukumu hili lilijumuisha safari nyingi kutoka mji mmoja hadi mwingine na katika safari hizo alisaidia pia kusambaza nyaraka kutoka kwa Baha'u'lláh kwenda kwa waumini na pia kusaidia kusafirisha barua za waumini walizomwandikia Baha'u'lláh. Mwaka 1891 Haji Amin alikamatwa pamoja na Haji Akhundi na wakafungwa kwa miaka miwili kwa ajili ya Imani. Mnamo mwaka 1916 kutokana na umri kuwa mkubwa alimuomba 'Abdu'l-Bahá awe na msaidizi mwingine na akakubaliwa. Kwa hiyo akamteua Haji GhulamRida kuwa msaidizi wake katika jukumu la kukusanya Huqúqu'lláh. Baada ya kuhudumia Imani kwa muda mrefu hatimaye Haji Amin alifariki mnamo mwaka 1928 mjini Tehrán. Baadaye mwaka huo huo aliofariki Shoghi Effendi alimtaja kuwa Mkono wa Hoja. Baraka yake ya kipekee ni kwamba Haji Amin aliishi tangu kipindi cha Báb hadi kipindi cha Shoghi Effendi na alihudumu kama mdhamini wa Huqúqu'lláh kwa miaka 11 ya mwisho ya kipindi cha Uongozi wa Baha'u'lláh, miaka 29 ya Uongozi wa 'Abdu'l-Bahá na miaka 7 ya mwanzo ya Uongozi wa Shoghi Effendi.

### 3. Keith Ransom-Kehler (1876 - 1933)



Alizaliwa mwaka 1876 huko Kentucky, Marekani. Alisoma hadi ngazi ya shahada ya uzamili katika lugha ya Kiingereza na baadaye akawa mhadhiri

katika vyuo mbalimbali nchini humo. Alikutana na mafundisho ya Baha'u'lláh kwa mara ya kwanza mwaka 1911 akiwa mjini London alipopata baraka ya kukutana na 'Abdu'l-Bahá wakati wa ziara Yake nchini Uingereza. Alijiunga na Imani mwaka 1920 na baada ya hapo akafanya kazi kubwa ya kufundisha Imani katika miji mbalimbali nchini humo na baadaye akarudi nchini Marekani. Kadiri alivyozidi kufundisha Imani akatokea kuwa mzungumzaji mahiri wa Kibahá'i nchini Marekani. Alisafiri sehemu mbali mbali nchini Marekani na Canada kufundisha Imani na baadaye nje ya bara la Amerika ikiwemo Afrika, Asia, Australia, New Zealand, Amerika kusini na baadaye nchini Irán. Mwaka 1932 Mlinzi Shoghi Effendi alimuita Haifa na kumtuma aende Irán kumuomba Sháh (mfalme) aondoe marufuku ya kuchapisha na kusambaza vitabu na machapisho ya Kibahá'i iliyokuwa imewekwa na serikali. Bila kusita Keith-Kehler alikwenda Irán kutekeleza jukumu hilo zito; alifanya juhudi ya kukutana na maofisa wa ngazi za juu serikalini wakiwemo wasaidizi wa Sháh, lakini mtawala huyo alikataa kuondoa marufuku hiyo. Baadaye alifanya safari za kufundisha na kukutana na waumini katika miji kadhaa nchini Irán pamoja na kutembelea maeneo matakatifu ya Kibahá'i. Akiwa mjini Tehrán, baada ya kutembelea miji mbalimbali nchini humo alipata ugonjwa wa ndui na kufariki dunia mjini humo mnamo mwaka 1933. Wiki mbili baadaye mlinzi akiomboleza kifo chake alimtaja Keith Ransom- Kehler kuwa Mkono wa Hoja ya Mungu.

### 4. Martha Root (1872 - 1939)



Martha Louise Root alizaliwa mwaka 1872 katika jimbo la Ohio, nchini Marekani. Alisoma hadi chuo kikuu cha Chicago na kuwa mwalimu baada ya kuhitimu. Kutoka na uwezo wake na mapenzi yake baadaye akawa mwandishi wa magazeti. Mwalimu wake wa kwanza wa Imani alikuwa Roy Wilhem na baadaye alikutana na Wabahá'i wengine wa mwanzoni kama vile Thorton Chase na Arthur Agnew na akajiunga na Imani mjini Pittsburgh mwaka 1909. Lakini kitu kilicholeta msukumo mpya kwa Martha Root

ilikuwa ni ziara ya 'Abdu'l-Bahá kule Amerika mwaka 1911-1912 ambapo Martha alipata baraka ya kukutana na 'Abdu'l-Bahá. Alitumia uwezo wake wa kiuandishi kuandika makala juu ya historia na mafundisho ya Imani kwenye magazeti nchini Marekani. Baada ya kupata na kusoma Nyaraka za Mpango Mtakatifu kwa Amerika alianza safari za ufundishaji katika nchi mbalimbali. Alianza safari za ng'ambo mwaka 1915. Baadhi ya nchi alizotembelea kwa ajili ya kufundisha Imani ni India, China, Canada, Australia, New Zealand, Mexico, Guatemala, Afrika kusini, Misri, Uingereza, Yugoslavia, Ugiriki, Ujerumani, Japan na Uswisi. Martha Root alitamani na kufanya juhudi sana kuufikisha ujumbe wa Baha'u'lláh kwa watawala na watu mashuhuri. Alifanya safari kwa kusudi la kufanya mahojiano na rais wa Guatemala ambaye hata hivyo alipinduliwa siku moja kabla ya tarehe aliyokuwa amepangiwa kumuona. Mwaka 1930 alijaribu kwenda Japan kuonana na mfalme Hirohito ambaye alimpelekea zawadi ya vitabu vya Kibahá'i, hata hivyo alikataliwa na maofisa wa ubalozi nchini humo kukutana naye. Vile vile alijaribu kwenda Irán kwa nia ya kuonana na Sháh Reza Pahravi ingawa hakufanikiwa kukutana naye. Hata hivyo, alifanikiwa kuonana na malkia Marie wa Romania mara kadhaa na kumfundisha Imani. Kwa mara ya kwanza alikutana naye mjini Bucharest mwaka 1926 na kumpa kitabu cha ''Baha'u'lláh na Wakati Mpya". Baadaye malkia Marie alikuja kuikubali Imani ya Kibahá'i, hivyo akawa mtu wa kwanza kutoka familia ya kifalme kuwa Mbahá'i. Malkia Marie alikuwa ni mjukuu wa Malkia Victoria wa Uingereza. Martha Root pia alikutana na rais Masaryk wa
Czechoslovakia, mwana mfalme Paul na mkewe Olga wa Yugoslavia, mfalme Faisal wa Iraq na viongozi wengine mashuhuri katika nchi mbalimbali. Vile vile alikuwa Mbahá'i wa kwanza kufanya kipindi cha mafundisho ya Imani redioni mnamo mwaka 1924 kule Australia. Mwaka 1939 baada ya safari nyingi na ndefu za ufundishaji alifariki dunia huko Hawaii, Marekani. Mwaka huo huo alitangazwa na Mlinzi kuwa Mkono wa Hoja.

## 5. ‘Abdul Jalil Bey Sa’d (H – 1942)




‘Abdul Jalil Bey Sa’ad alizaliwa na kukulia nchini Misri lakini mwaka wake wa kuzaliwa haujulikani vizuri. Alikuwa msomi na mtaalamu mahiri wa sheria, hadi akafikia kuwa jaji wa mahakama kuu nchini humo. Vile vile alikuwa mwandishi na mtetezi wa haki za kiraia. Akiwa tayari ni jaji wa mahakama kuu alifundishwa Imani na akawa Mbahá’i baada ya kukutana na msomi na mwalimu mashuhuri wa Kibahá’i Mirza ‘Abdu’l-Fadl, aliyekuwa ametumwa na ‘Abdu’l-Bahá kufundisha Imani nchini humo mwaka 1895. Aliandika makala nyingi zenye ushawishi wa kisheria juu ya uhuru wa dini na kuabudu. Mwaka 1929 wakati Wabahá’i wa Misri wakiwa katika shida kubwa ya kukosa haki zao za msingi Bey Sa’ad alisaidia sana kwa juhudi zake kupeleka matatizo yao kwa viongozi wa serikali na vyombo vya kisheria na hatimaye matatizo yao yakaanza kutatuliwa. Mara zote alikuwa akipigania haki za kuabudu na kanuni ya kuwa dini zote lazima zipewe haki sawa. Mwaka 1934 katiba ya Baraza la Kitaifa la Misri ilikataliwa kusajiliwa na serikali hivyo kuzuia kutambulika kwa shirika hilo kisheria. Bey Sa’ad alilisimamia suala hilo hadi kwa mwanasheria mkuu wa serikali, akajenga hoja za kisheria hadi zikakubalika na kusajiliwa.

‘Abdu'l-Jalil Bey Sa'ad alitafsiri kitabu cha Wanamapambazuko kwa Kiarabu na kikachapishwa mwaka 1941, lakini mamlaka za kiislamu zilikipinga kwa madai kuwa kilikuwa kinapinga Uislamu na wakafanikiwa kukizuia kisisambazwe na kusomwa. Lakini kwa juhudi kubwa na umahiri wake wa sheria, Bey Sa’d baadaye alifanikiwa kupata ruhusa ya kukisambaza na kuondolewa kwa marufuku hiyo. Vile vile Bey Sa’ad alifanya tafsiri ya kitabu cha ‘Baha’u’lláh na Wakati Mpya’ pamoja na machapisho mengine ya Imani kutoka Kiingereza kwenda Kiarabu. Baadaye mwaka huo huo alifanikisha kupatikana kwa kibali cha serikali cha Wabahá’i wa Misri kujenga makao ya kitaifa (Haziratu'l-Quds) jijini Cairo. Akiwa na hamu kubwa kuona wanapata makao ya kitaifa, alihusika binafsi kutafuta kiwanja na kusimamia ujenzi.

Wakati akiendelea kusimamia kazi ya ujenzi alianza kuugua, akapatiwa matibabu ya upasuaji na siku chache baadaye alifariki ghafla tarehe 25 Mei, 1942. Mwezi mmoja baada ya kifo chake (25 Juni 1942) Shoghi Effendi alimtangaza kuwa Mkono wa Hoja.


### 6. Siyyid Mustafa Rumi (1852 -1945)



Siyyid Mustafa Rumi alizaliwa mwaka 1852 jijini Baghdad, Iraq katika familia ya kiislamu na alilelewa na mjomba wake baada ya mama yake kufariki akiwa bado mtoto mchanga. Alilelewa katika dini na kufuata maadili ya kiislamu kikamilifu. Akiwa kijana alijifunza na kupata ujuzi wa kuongea lugha nyingi yaani Kiarabu, Kiajemi, Kihindi, Kitamil, Gujarat, Urdu, Kiburma na Kiingereza, na ndipo alihamia Madras, India ili kumsaidia baba yake katika biashara ya mchele**.** Muda mfupi kabla hajarejea Iraq mwaka 1876 alikutana na Jamal Effendi-mwalimu wa kwanza wa Imani nchini India aliyekuwa ametumwa na Baha'u'lláh Mwenyewe. Alivutiwa sana na mafundisho yaliyotolewa na Jamal Effendi mpaka akafuta mipango yake ya kurudi Iraq na kuanza kuandamana naye katika safari zake za ufundishaji, na mwaka mmoja baadaye, mwaka 1877 alikiri Imani yake kwa Baha'u'lláh. Kuanzia mwaka 1879 Rumi alianza safari za ufundishaji akiambatana na Jamal Effendi katika miji na nchi mbalimbali za Asia ya kusini ikiwemo Rangoon, Madras, Singapore, Java, Bali, Malay na baadaye alirudi Burma na Jamal Effendi alirudi India. Bila shaka unajua kuwa sanduku lililowekwa mwili wa mtukufu Báb kabla ya kuzikwa lilinakshiwa kwa marumaru nzuri. Hii ilikuwa zawadi iliyotolewa na watu wa Burma, na Mustafa Ruma alikuwa mmoja wa watu walionunua marumaru hiyo na kuipeleka Nchi Takatifu kwa 'Abdu'l-Bahá mwaka 1899. Alikuwa mwandishi na mzungumzaji mzuri na alisaidia kutafsiri katika lugha ya Burma vitabu kadhaa vya Imani vikiwemo *Kitabu Yakini*, *Maneno Yaliyofichwa, Sala za Kibahá'i, na Baadhi ya Maswali Yaliyojibiwa*. Alihudumia Imani katika nyanja za ufundishaji,

tafsiri na utawala kwa kipindi chote cha maisha yake katika Imani na mpendwa Mlinzi alimuelezea kama “mfano wa kweli wa muumini na mtangulizi imara wa Imani aliyetokea katika karne ya kwanza ya uwepo wa Imani”. Mustafa Rumi alikuwa mahiri sana katika kuimarisha waumini na kujenga jumuiya imara za Kibahá’i. Pia alihudumu katika Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabahá’i wa India na Burma. Aliuawa tarehe 13 Machi, 1945 wakati wa vita vya dunia kwa kukatwa mwili wake vipande vipande na wapiganaji wa kikabila waliovamia kijiji cha Daidanaw alikokuwa akiishi. Walichoma nyumba na kuua Wabahá’i kumi na mmoja akiwemo yeye. Baadaye Wabahá’i wa eneo hilo walivikusanya vipande vya mwili wake na kumfanyia maziko stahiki kwenye eneo la Bahá’i senta. Mwezi Julai mwaka huo huo Shoghi Effendi katika ujumbe wa kuomboleza kifo chake alimtaja Mustafa Rumi kama Mkono wa Hoja ya Mungu. Mwaka 1948 akiwaandikia marafiki wa Australia na New Zealand kuwatia moyo kuhudumia Imani yeye alisema “…angalieni mafanikio ya Mustafa Rumi kule Burma, ……………. ni moyo wa kujitoa na dhabihu binafsi ndiyo iletayo matokeo katika huduma ya Imani hii, kuliko nyenzo, uwezo au hali ya ukwasi”.

## 7. Muhammad Taqi-i-Isfahani (H --- 1946)



Muhammad Taqi Isfahani alizaliwa katika kijiji cha Sidih, kule Isfahan eneo lililokuwa maarufu kwa kutoa walimu na washairi mahiri katika Imani ya Kibábi na baadaye Kibahá’i. Mwaka 1875 yeye pamoja na Wabahá’i wenzake kadhaa walikamatwa wakateswa na kufungwa gerezani kwa sababu ya kufundisha Imani kwa watu huko Isfahan. Baadaye mwaka 1878 alihamia Misri na kuendelea na huduma ya ufundishaji Imani. Wakati wa kipindi cha Baha'u'lláh, alitembelea Nchi Takatifu mara 4 ambapo alipata baraka ya kufika mbele ya Baha’u’lláh. Wakati ‘Abdu'l-Bahá alipotembelea Misri kati ya mwaka 1910 na 1913 alikutana na Muhammad Taqi Isfahani kwa sababu nyumba yake ndiyo ilikuwa kitovu cha shughuli za Kibahá’i nchini humo.

Ilikuwa ni nyumbani mwake ambamo Mirza 'Ab'ul-Fadl alifia mwaka 1914 na pia Lua Getsinger mwaka 1916. 'Abdu'l-Bahá alipofariki mwaka 1921, Muhammad Taqi Isfahani alisafiri mara moja kwenda Haifa na alifanikiwa kuwepo wakati Wasia na Agano Lake linasomwa na alisimama imara kulilinda Agano hasa katika nyakati za uasi wa wavunja agano. Mwaka 1924, Muhammad Taqi Isfahani alichaguliwa kwenye Baraza la Kitaifa la kwanza la Misri. Vile vile alijishughulisha na uandishi, tafsiri na uchapishaji wa vitabu na Maandiko ya Imani. Muhammad Taqi Isfahani alikuwa na uwezo mkubwa wa kukariri sala nyingi na nyaraka za Baha'u'lláh na 'Abdu'l-Bahá na pia alikuwa na uwezo mkubwa wa kuelezea kwa ufasaha matukio yote muhimu ya kihistoria katika Imani. Alifariki mwaka 1946 jijini Cairo na kuzikwa kwenye makaburi ya Kibahá'i. Mwezi Desemba mwaka huo huo mpendwa Mlinzi alimtangaza Muhammad Taqi kuwa Mkono wa Hoja.

## 8. Louis Gregory (1874--1951)



Louis George Gregory alizaliwa Chareston, Carolina Kusini, Marekani mwaka 1874, miaka michache baada ya wazazi wake kupewa uhuru kutoka kuwa watumwa. Baba yake mzazi alifariki wakati Louis akiwa mdogo na baadaye mwaka 1881 mama yake aliolewa na George Gregory ambaye alimlea Louis kwa upendo mkubwa na ndipo alipoanza kutumia jina la Louis Gregory. Alisoma hadi chuo kikuu na kuwa mwanasheria na wakili wa mahakama kuu mwaka 1902. Alisikia juu ya Imani mwaka 1907 kutoka kwa mfanyakazi mwenzake ambaye naye hakuwa Mbahá'i bali alikuwa amehudhuria mkutano wa Wabahá'i na kupewa kipeperushi. Louis alivutiwa na kipeperushi hicho na baadaye huyo bwana aliyeleta kipeperushi hicho alimtambulisha kwa Wabahá'i alikokuwa amekipata. Siku chache zilizofuata Wabahá'i walimwalika kwenye mkutano ambao mzungumzaji alikuwa Lua Getsinger. Alipendezwa na mafundisho yale kiasi kwamba alianza kujifunza zaidi juu ya Imani hiyo mpya na mnamo mwaka 1909 alijitangaza kuwa

Mbahá'i. Akiwa mwanasheria mwanaharakati wa kupinga ubaguzi wa watu weusi huko Amerika alivutiwa zaidi na mafundisho ya Baha'u'lláh yanayolenga kuondoa ubaguzi wa aina zote na jinsi alivyoshuhudia jamii ndogo ya Wabahá'i ilivyojitahidi kutoonesha hali ya ubaguzi katika mikutano yao aliyokuwa akialikwa mara kadhaa kuhudhuria ili kujifunza Imani. Aliamini kwamba kwa kuwa Mbahá'i angeendeleza juhudi zake za kupigania ubaguzi wa rangi kwa mtazamo mpana zaidi wa kidunia na kwa njia zilizo bora zaidi na zilizoangaziwa na Maandiko ya Mungu. Alitiwa moyo sana na barua aliyoandikiwa na 'Abdu'l-Bahá akimuhimiza kuendeleza juhudi za kuleta umoja na upatano wa watu wa rangi zote kwa kutumia mafundisho ya Imani. Mnamo mwanzoni mwa mwaka 1911 Louis Gregory alikuwa Mwamerika mweusi wa kwanza kwenda hija Nchi Takatifu kwa mwaliko wa 'Abdu'l-Bahá. Upendo wa Louis Gregory kwa 'Abdu'l-Bahá ulizidi kuongezeka wakati wa ziara ya 'Abdu'l-Bahá kule Amerika mnamo mwaka 1912. Katika hafla mojawapo aliyoandaliwa na viongozi wa kiserikali na watu mashuhuri jijini Washington D.C, 'Abdu'l-Bahá alivunja itifaki na mila za wakati huo kwa kuagiza Louis Gregory akae meza kuu pembeni Yake. Vile vile, 'Abdu'l-Bahá alimtia moyo Louis Gregory kumuoa Louisa Mathew, Mbahá'i wa kizungu kwa kumwambia kuwa muungano huo wa ndoa ungekuwa mzuri kwa wote wawili. Kwa ushauri huo mara moja wakaanzisha uchumba na baadaye Septemba mwaka huo 1912 wakafunga ndoa, ikiwa ni ndoa ya kwanza ya Kibahá'i kati ya mweusi na mzungu nchini Marekani, jambo ambalo halikuwa la kawaida katika kipindi hicho. 'Abdu'l-Bahá aliielezea ndoa hiyo kuwa ni ''utangulizi wa ukamilisho wa utangamano kati ya mbari za watu".

Louis Gregory alihudumia Imani katika Nyanja tatu; ufundishaji wa Imani, kushiriki katika utawala wa Imani na kuendeleza jitihada za kuleta umoja wa mbari za watu. Katika uwanja wa ufundishaji alikuwa mwalimu msafiri wa Imani takribani katika majimbo yote ya Marekani akielekeza juhudi zake zaidi kwa jamii ya Waamerika weusi iliyokuwa ikibaguliwa sana kwa wakati huo. Aliacha kazi yake ya uanasheria na kutumia muda wote kufundisha Imani hasa katika majimbo ya kusini mwa Marekani hasa baada ya kusoma Nyaraka za Mpango Mtakatifu zilizoandikwa na 'Abdu'l-Bahá kwa waumini wa Amerika mwaka 1916. Kwa takribani miongo mitatu kutoka 1917 hadi 1946 alikuwa mwalimu msafiri bila kupumzika huku akisafiri na kuishi katika mazingira magumu. Mara nyingi alisafiri bila mke wake kuepuka

kadhia ambazo zingetokea kutokana na taratibu za kijamii za kibaguzi za wakati huo. Katika Nyanja za utawala wa Imani Louis Gregory alianza kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Bodi ya 'Baha'i Temple Unity' mwaka 1912 katika mkutano mkuu wa kwanza wa Kitaifa uliohudhuriwa na 'Abdu'l-Bahá. Hii ndiyo ilikuwa kama Baraza la Kitaifa kwa wakati huo. Mwaka 1922 wakati Baraza la kwanza la Kitaifa la Marekani lilipochaguliwa, Louis Gregory alichaguliwa kama mjumbe na katibu wa Baraza hilo la kwanza. Alihudumu katika Baraza la Kitaifa la Marekani kwa miaka kumi na nne. Katika uwanja wa juhudi za kutokomeza ubaguzi alikuwa mstari wa mbele kufundisha na kutoa hotuba juu ya uondoaji wa chuki na kujenga umoja kwa jamii mbalimbali. Alihutubia katika makongamano na mihadhara mbalimbali akielezea kanuni ya umoja katika vyuo vikuu, kwa wanaharakati wa kupinga ubaguzi, wanazuoni nk. Vile vile aliongoza kamati ya kitaifa ya Kibahá'i ya kujenga uhusiano wa watu wa rangi mbalimbali. Katika kuendeleza juhudi zote hizo, kilichokuwa kinawashangaza watu ni hali yake ya kutokasirika wakati alipofanyiwa vitendo vya kibaguzi hata kama vilihatarisha maisha yake. Katika miaka mitano ya mwisho wa maisha yake afya yake ilidhoofu na hivyo akawa hawezi kusafiri. Mnamo Julai 1951 alifariki ghafla nyumbani kwake Eliot na kuzikwa na Wabahá'i kwa heshima kubwa. Akiandika ujumbe wa kuomboleza kifo chake tarehe 5 Agosti,1951 Mlinzi Shoghi Effendi alimtangaza Louis Gregory kuwa Mkono wa Hoja.


### 9. Roy C. Wilhelm (1875 – 1951)



Roy Cochran Wilhelm alizaliwa mwaka 1875 huko Ohio, Marekani. Mama yake alijiunga na Imani mwaka 1898 lakini yeye hakuvutiwa na Mafundisho ya Imani. Mwaka 1900 wakati Roy Wilhelm akiwa kijana wa miaka 25, akiwa jijini New York, aliota ndoto ya ajabu. Alimuona mtu mmoja aliyevaa joho, mwenye ndevu ndefu nyeusi, alichukua pete yake akaivika kwenye kidole cha Roy na akachukua pete ya Roy na kuivaa kwenye kidole chake. Roy

alipoamka alishikwa na bumbuazi lakini hakumwambia mtu yeyote juu ya ndoto hiyo. Alipofikia umri wa utu uzima alihamia New York na huko alifanikiwa kuwa mfanya biashara na tajiri mkubwa. Mwaka 1907 mama yake alimuomba Roy waende pamoja kuhiji katika Nchi Takatifu, naye akakubali japo wakati huo yeye hakuwa Mbahá'i. Walipata fursa ya kufika mbele ya 'Abdu'l-Bahá na Roy akakiona chumba kile kile alichokiona kwenye ndoto yake miaka kadhaa iliyopita na akaamua kumsimulia 'Abdu'l-Bahá juu ndoto yake na alichokiona. Na hapo akatangaza kumkubali Baha'u'lláh kama mdhihirishaji wa Mungu. 'Abdu'l-Bahá akamwambia kuwa Baha'u'lláh Mwenyewe ndiye aliyekuwa amemchagua na kumfanya awe Mbahá'i. Aliporejea Marekani alikuwa na shauku kubwa kuendeleza Mafundisho aliyoyapata kwa 'Abdu'l-Bahá na mara moja akaanza kufundisha Imani kwa juhudi kubwa san. Mmojawapo wa watu waliofundishwa naye katika kipindi hicho ni Martha Root, ambaye baadaye alikuja kuwa mwalimu mahiri wa Imani na baadaye kutangazwa kuwa Mkono wa Hoja. Roy alichaguliwa kuwa mjumbe wa 'Bodi ya Bahá'i Temple Unity' ya kwanza mwaka 1909 na baadaye kwenye Baraza la kwanza la Kitaifa la Wabahá'i wa Marekani na Canada na alihudumu kwenye Baraza hilo kwa mfululizo hadi mwaka 1946, mara nyingi akihudumu kama mhazini. Alisifika kwa kuwa mfano kwa maisha ya unyoofu ya Mbahá'i halisi na kutoa mali zake nyingi kwa ajili ya Imani. Alikuwa mfadhili mkubwa wa shughuli za ufundishaji za walimu wasafiri huko Marekani na hata zile safari za Martha Root na Louis Gregory. Wakati wa ziara ya 'Abdu'l-Bahá huko Marekani sehemu aliyofanyiwa karamu ya kukutana na Wabahá'i huko New Jersey ilikuwa ni kwenye bustani ya shamba lake ambalo baadaye Roy alilitoa iwe mali ya Imani. Alifariki huko Maine mwaka 1951 na tarehe 23 Desemba, 1951 Shoghi Effendi akamtangaza kuwa alikuwa Mkono wa Hoja.

## 10. John Hyde-Dunn (1855 –1941)



John Henry Hyde-Dunn alizaliwa mnamo Machi, 1855 jijini London, Uingereza. Akiwa bado kijana alianza kazi ya uwakala wa mauzo wa kampuni ya maziwa nchini Uingereza na Ufaransa na baadaye alihamia nchini Marekani na kuendelea kufanya kazi hiyo hiyo. Mwaka 1905 akiwa mjini Seatle alimsikia mtu mmoja aliyeitwa Ward Fitzgerald akimwambia mtu maneno ambayo alisikia sentensi moja "Dunia ni nchi moja na binadamu ni raia wake, msiangaliane kama wageni". (Maneno ya Baha'u'llah aliyomwambia profesa E.G Browne kule Bahji). Alivutiwa mno na maneno haya na kuanza kumpeleleza ili kujua chanzo cha maneno hayo. Huu ndio ulikuwa mwanzo wake wa kujifunza Imani na baada ya siku chache akawa Mbahá'i. Baadaye alianza kuandamana na Fitzgerald kwenda kufundisha Imani. Hii ilimkutanisha na Wabahá'i thabiti wa wakati huo kama vile Thornton Chase, Lua Getsinger na Ella Cooper ambao walisaidia sana kumuimarisha katika Mafundisho ya Kibahá'i. Mwaka 1907 Hyde-Dunn alikutana na Clara Davis katika mkutano wa Kibahá'i na baada ya kufuatilia Mafundisho, baadaye Clara alijiunga na Imani. Clara aliyezaliwa mwaka 1869 alikuwa mjane aliyekuwa amefiwa na mumewe kutokana na ajali. Hyde-Dunn na Clara wote walipata bahati ya kumuona 'Abdu'l-Bahá mwaka 1912 wakati wa ziara Yake huko Amerika na walihudhuria hotuba Zake nyingi huko California ambazo ziliwaimarisha sana katika Imani. Mwaka 1916 mke wa kwanza wa Hyde-Dunn aliyeitwa Fanny alifariki na mwaka mmoja baadaye alimuoa Clara (aliyekuwa mjane) na kuanzia hapo mama huyo akajulikana kama Clara Dunn. Baada ya kupokea na kusoma 'Nyaraka za Mpango Mtakatifu' Hyde-Dunn na mkewe Clara waliamua kuitikia wito wa 'Abdu'l-Bahá kwa 'kupeleka ujumbe wa Baha'u'lláh huko ambako 'Abdu'lBahá alitamani kuupeleka lakini hakuweza' kwa sababu ya umri – Australia. Wakati baadhi ya marafiki zao walipojaribu kuwashauri kuwa haikuwa busara kwa wao kuwa watangulizi katika bara hilo la mbali katika umri wao mkubwa, Hyde-Dunn aliwajibu kuwa kwake "ni afadhali kufa kuliko kutotimiza tamanio la 'Abdu'l-Bahá". Hivyo tarehe 10, Aprili, 1920 John Hyde-Dunn na mkewe Clara Dunn waliwasili Sydney, Australia wakawa watangulizi wa kwanza kupeleka ujumbe wa Baha'u'lláh nchini Australia na New Zealand. Ili kupata fedha ya kujikimu huku wakifundisha Imani, HydeDunn alipata kazi ya mauzo kwenye kampuni ya maziwa na muda mfupi baadaye alipandishwa cheo kutokana na kufanya vizuri kwenye mauzo, na nafasi hiyo ikampa nafasi ya kusafiri katika miji mingi kufanya

masoko na huku akifundisha ujumbe wa Baha'u'lláh kila alikokwenda. Baada ya miaka 2 ya ufundishaji Imani hatimaye mtu wa kwanza katika bara la Australia alitangaza imani yake kwa Baha'u'lláh, na Desemba 1923 Baraza la kwanza la Mahali liliundwa jijini Melbourne, Australia. Mwaka 1932 Clara Dunn alienda hija, na alipokutana na Mlinzi mjini Haifa, Mlinzi alimwambia kuwa ulikuwa wakati muafaka wa kuunda Baraza la Kitaifa la Australia, na miaka miwili baadaye mwaka 1934, walifanikiwa kuunda Baraza la kwanza la Kitaifa na Hyde-Dunn alikuwa mjumbe. Watu waliokuwa Wabahá'i kwa kufundishwa Imani na Hyde na Clara Dunn moja kwa moja walifikia zaidi ya mia moja na miongoni mwao ni Gretta Lamprill, Bertha Dobbins na Harold na Florence Fitzer waliokuja kupewa hadhi ya kuwa 'Mashujaa wa Baha'u'lláh. Mwaka 1941 John Hyde-Dunn alifariki dunia akiwa na umri miaka 86 baada ya kazi kubwa ya kufundisha Imani. Katika ujumbe wa kutangaza kifo chake, Mlinzi alimuelezea kama 'mkombozi wa kiroho wa Australia'. Hyde na mkewe Clara ni kati ya Wabahá'i wachache walioitikia wito wa 'Abdu'l-Bahá wa Nyaraka za Mpango Mtakatifu na kwenda kupeleka ujumbe kwenye bara jipya, kwa kuhamia na kustawisha Imani Australia. Aprili 26, 1952, Mlinzi alimtangaza John Hyde Dunn kuwa alikuwa Mkono wa Hoja.

Baada ya kifo cha mumewe Clara aliendelea na juhudi za kuhudumia Imani na hasa kuimarisha jamii za Kibahá'i ambazo zilikuwa bado changa nchini Australia. Mnamo Februari 1952 Mlinzi alimteua Clara Dunn kuwa Mkono wa Hoja na kumuelekeza kufanya huduma yake Australia na New Zealand. Tangazo hili lilikuwa ni miezi miwili kabla ya kifo cha mumewe Hyde Dunn. Mnamo Aprili, 1954 Mlinzi alimteua kuwa mdhamini wa Mfuko wa Bara la Australasia na wakati huo huo kumwambia ateue Washauri Wasaidizi wake wawili ili wamsaidie katika majukumu yake. Alimteua Collis Featherstone ambaye baadaye naye aliteuliwa kuwa Mkono wa Hoja na Thelma Perks ambaye baadaye alikuja kuteuliwa kuwa Mshauri wa Bara la Australasia. Pamoja na kuwa dhaifu kiafya na mwenye umri wa miaka 88, Clara Dunn alisafiri kwenda Haifa kuhudhuria mkutano wa Mikono wa Hoja kufuatia kifo cha ghafla cha Shoghi Effendi.

# 5

## MIKONO WA HOJA WALIOTEULIWA KWA MAKUNDI

Ilikuwa ni tarehe 24 Desemba, 1951 Shoghi Effendi alipotangaza kuteua kundi la waumini 12 kuwa Mikono wa Hoja. Ilikuwa mara ya kwanza kuwateua Mikono ambao walikuwa bado hai wakiishi katika maeneo mbalimbali duniani. Ruhiyyih Khanum alidokeza baadaye kuwa alipomuuliza Shoghi Effendi kwa nini hapo kabla Mikono wa Hoja walikuwa wanatajwa wakati wamekwishafariki, alimjibu kuwa Wabahá'i wengi wakati huo walikuwa bado wachanga katika Imani na hivyo ingekuwa vigumu kwao kupokea bila wivu na lawama hali ya muumini mwenzao kupewa hadhi kama hiyo. Bila shaka kwa kuteua waumini hao kuwa Mikono ilikuwa ni ishara kwamba ukomavu wa waumini ulikuwa umeongezeka. Katika ujumbe wake Mlinzi alihusisha uteuzi huu na ujumbe wake wa Novemba 30, ambapo alikuwa ameeleza mpango wa kufanyika kwa mikutano mikubwa ya mabara ya Afrika, Amerika, Ulaya na Asia ambayo ingeweka mipango mahsusi ya maendeleo ya Imani katika mabara hayo. Na miezi miwili baadaye tarehe 29, Februari 1952, Shoghi Effendi aliteua tena kundi lingine la waumini saba kuwa Mikono wa Hoja. Kwa hiyo, sasa kukawa na jumla ya Mikono wa Hoja 19. Hii ilikuwa ni hatua kubwa katika ukunjukaji wa asasi ya Mikono wa Hoja.

### *Kundi la kwanza: Walioteuliwa 24 Desemba, 1951*

| Na | Jina La Mkono wa Hoja | Kuzaliwa | Kufariki |
|---|---|---|---|
| 1 | Dorothy Baker | 1898 | 1954 |
| 2 | Amelia E. Collins | 1873 | 1962 |
| 3 | 'Ali-Akbar Furutan | 1905 | 2003 |
| 4 | Ugo Giachery | 1896 | 1989 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5 | Hermann Grossmann | 1899 | 1968 |
| 6 | Horace Holley | 1887 | 1960 |
| 7 | Leroy Ioas | 1896 | 1965 |
| 8 | William Sutherland Maxwell | 1874 | 1952 |
| 9 | Charles Mason Remey | 1874 | 1974 |
| 10 | Tarazu'lláh Samandari | 1875 | 1968 |
| 11 | George Townshend | 1876 | 1957 |
| 12 | Valiyyu'lláh Varqa | 1884 | 1955 |

## 1. Dorothy Baker (1898 – 1954)



Dorothy Beecher Baker alizaliwa mwaka 1898, New Jersey nchini Marekani. Akiwa binti mdogo wa miaka 13 bibi yake alikwenda naye jijini New York kumuona ‘Abdu’l-Bahá wakati anafanya ziara Yake huko Amerika. Alipofikisha miaka 15 alijitangaza kuwa Mbahá’i. Aliolewa mwaka 1921 na Frank Baker na katika ndoa yao hiyo walibahatika kupata watoto wawili. Mwaka 1926 alichaguliwa kwa mara ya kwanza kuwa mjumbe wa Baraza la Kitaifa la Marekani hadi mwaka 1937. Dorothy Baker alihudumia Imani katika namna mbalimbali; mjumbe wa Baraza la Kitaifa la Marekani kwa miaka 14, alifanya safari za ufundishaji katika nchi takribani 15 za bara la Amerika, nchi 14 za Ulaya na alitoa hotuba katika vyuo 140 nchini Marekani. Dorothy Baker alijulikana kama mmoja wa wazungumzaji mahiri wa Imani huko Marekani wakati huo. Tarehe 24 Desemba, 1951 akiwa njiani kwenda Ulaya aliteuliwa kuwa Mkono wa Hoja pamoja na wengine 11. Mwaka 1953 Mlinzi aliandaa mkutano mkubwa wa mipango ya ufundishaji ya bara la Afrika jijini Kampala, Uganda na alimtuma yeye Dorothy Baker na Mikono wengine kama vile Ali Akbar Furutan, Ugo Giachery, Herman Grossman, AliMuhammad Varqa, George Townshend na Dhikrullah Khadem

kuendesha mkutano huo mkubwa. Alifariki Januari 10, 1954 katika ajali ya ndege iliyoangukia kwenye bahari ya Mediterranian akiwa safarini kutoka Pakistani kwenda Roma, ikiwa ni mojawapo ya safari zake nyingi za ufundishaji. Siku mbili baada ya ajali hiyo wavuvi waliokota pochi ya msafiri aliyekuwemo kwenye ndege hiyo, ndani ikiwa na kipeperushi cha Kibahá'i.

Kwa kuwa pochi hiyo iligundulika kuwa haikuwa ya kwake kwa hiyo ilimaanisha kuwa Dorothy Baker alikuwa akifundisha na kugawa vipeperushi ndani ya ndege hiyo; mauti yalimkuta akifundisha ujumbe wa Baha'u'lláh.

### 2. Amelia E. Collins (1873 –1962)




Amelia Engelder Collins alizaliwa Juni, 1873 Pennsylvania, nchini Marekani katika familia ya Kilutheri. Alipokuwa binti mkubwa aliolewa na Thomas Collins, mhandisi wa madini, na walihamia Michigan na baadaye California ambapo Amelia alikutana na mafundisho ya Imani na kuwa Mbahá'i kwenye mwaka 1919. Alifanya hija yake ya kwanza mwaka 1923 akiambatana na mume wake ambaye hakuwa Mbahá'i, lakini Mlinzi aliwaonesha ukarimu mkubwa. Mwaka 1924 Amelia alichaguliwa kwa mara ya kwanza kuwa mjumbe wa Baraza la Kitaifa la Marekani na Canada na aliendelea kuwa mjumbe hadi 1933 na tena kuanzia mwaka 1938 hadi 1951, Mlinzi alipomuita kwenda kuhudumia kwenye Makao Makuu ya Imani-Haifa. Wakati anahudumu kwenye Baraza la Kitaifa, pia aliteuliwa kuwa mjumbe wa kamati ya kitaifa ya Ufundishaji na Maendeleo ya Mabaraza, na alishiriki kwa kiasi kikubwa katika kazi ya ufundishaji na uimarishaji wa Mabaraza ya Kiroho ya Mahali katika maeneo mengi nchini Marekani. Mwaka 1937 Shoghi Effendi alipotoa zawadi maalum ya fundo la nywele za Baha'u'lláh kwa Wabahá'i wa Marekani, Amelia ndiye alipata bahati ya kuipeleka zawadi hiyo Marekani na aliiwasilisha kwenye konvesheni ya kitaifa ya mwaka 1938. Thomas Collins japo hakuwahi kujitangaza kuwa Mbahá'i hadi alipofariki

ghafla kwa ugonjwa wa moyo mwaka 1937, lakini alimsaidia sana mkewe Amelia kuhudumia Imani na hasa kumwezesha kifedha. Pato la Amelia na mume wake lilitokana na mume wake kuwa na hisa katika mgodi wa madini alizopata wakati anafanya kazi kama mhandisi wa madini nchini Marekani.

Baada ya mumewe kufariki Amelia alibaki na hisa hizo kama mrithi pekee. Amelia Collins ingawa aliishi maisha ya kawaida lakini alitoa kwa ukarimu michango mikubwa ya kifedha kwa Imani. Mwaka 1944 alimtumia Mlinzi kiwango kikubwa cha mchango kilichowezesha kukamilisha ujenzi wa kuba ya Kaburi la Báb kwenye Mlima Carmel. Michango mingine kutoka kwake ni pamoja na fedha zilizowezesha ununuzi wa ardhi kwa ajili ya Nyumba ya Ibada itakayojengwa kwenye Mlima Carmel, mchango kwenye mfuko wa ujenzi wa Nyumba ya Ibada ya Marekani, mchango mkubwa wa fedha za ununuzi wa viwanja vya Nyumba za Ibada za Amerika Kusini, Ulaya na Asia; sehemu kubwa ya fedha za ununuzi wa eneo kubwa linalozunguka kaburi la Baha'u'lláh kule Bahji, fedha za ujenzi wa Jengo la Makumbusho ya Kibahá'i kwenye mlima Carmel na kwa kiasi kikubwa kuwezesha ujenzi wa Mashriqu'l-Adhkar mama za mabara ya Ulaya, Afrika na Australia. Japo mchango wa mtu katika Imani ya Kibahá'i ni siri yake kwa Mungu, mchango wa Amelia Collins wa mali za kidunia ulikuwa wa kipekee. Na kwa kutambua upekee huo Shoghi Effendi aliamua kuwa lango kuu la kuingilia kwenye kaburi la Baha'u'lláh liitwe 'Lango la Collins' (Collin's Gate) kama kumbukumbu ya ukarimu wake usio wa kawaida. Kujitoa kwake Mlinzi alikuita 'utoaji wa ukarimu usio na kifani'. Yeye binafsi kila alipotoa hakutaka ijulikane kuwa ametoa, kwani alisema alitoa ili kutimiza agizo la 'Abdu'l-Bahá katika wasia Wake uliosema kuwa waumini wana wajibu wa kuhakikisha Mlinzi anakuwa mwenye furaha, kwa hiyo kila alipohisi Mlinzi ana mahitaji ya fedha kutimiza lengo fulani kwa ajili ya maendeleo ya Imani basi alitoa sehemu ya mali zake. Mwaka 1951 Mlinzi alimteua Amelia Collins kuwa Mkono wa Hoja na pia makamu mwenyekiti wa Halmashauri ya Kibahá'i ya Kimataifa aliyokuwa ameiunda, na hivyo Amelia alilazimika kuhamia makao makuu ya Imani mjini Haifa kutekeleza majukumu mapya ya kumsaidia Mlinzi katika kazi za kiutawala za Imani. Wakati wa kifo cha gafla cha Mlinzi, Amelia haraka alikwenda jijini London kumsaidia mjane wake Ruhiyyih Khanum kuandaa shughuli za maziko kwa kusaidiana na Mikono wengine kadhaa. Aliendelea na majukumu yake kama Mkono wa Hoja hadi kile kipindi cha mpito cha utawala wa Mikono wa Hoja, ambapo

alichaguliwa kuwa mmoja wa Waangalizi, huduma aliyoendelea nayo mpaka mwisho wa maisha yake. Mwaka 1961 akiwa Haifa alianguka na kuvujika mkono na mguu na akawa mtu mwenye kuhitaji msaada wa kiti cha magurudumu, hata hivyo aliendelea na majukumu kama Mkono wa Hoja na pia Mwangalizi. Tarehe 1 Januari 1962, Amelia Collins alifariki akiwa mikononi mwa rafiki yake wa karibu Ruhiyyih Khanum. Tukio hili lilitokea mjini Haifa wakati Amelia Collins alipokuwa na umri wa miaka 91.

### 3. Ali-Akbar Furután (1905 – 2003)



Ali- Akbar Furutan alizaliwa Februari, 1905 huko Sabzivar, Khurasan nchini Irán katika familia ya Kibahá'i. Akiwa mdogo mwaka 1914 familia yao ilihamia Ashkabad (nchini Urusi wakati huo) kutokana na kuongezeka kwa mateso kwa Wabahá'i mjini Khurasan. Alisoma shule huko Ashkabad hadi sekondari na alipomaliza masomo akaanza kufundisha kwenye shule ya Kibahá'i. Mwaka 1926 alipata nafasi ya kwenda kusoma shahada ya kwanza katika chuo kikuu cha Moscow. Alipangiwa kusomea Ualimu na Saikolojia ya Watoto. Baada ya kumaliza masomo ya chuo kikuu jijini Moscow alijishughulisha zaidi na ufundishaji wa Imani hali iliyopelekea mwaka 1930 kufukuzwa nchini Urusi na kurudi tena nchini Irán. Aliporudi Irán alijishughulisha na uendeshaji wa shule za jamii zilizojulikana kama 'Tarbiyat' na ufundishaji wa madarasa ya watoto ya Kibahá'i. Mwaka 1934 Ali Akbar Furutan alichaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Kiroho la Kitaifa la Irán na aliendelea kuwa mjumbe na katibu wa Baraza hilo hata baada ya kuteuliwa kuwa Mkono wa Hoja Desemba 1951 hadi 1957 alipolazimika kuhamia Haifa. Mwaka 1941 alifanya hija yake ya kwanza kwenda Nchi Takatifu akiambatana na mke wake, binti yake wa miaka minane na mama yake mzazi. Alipata fursa ya kufanya mazungumzo ya kina na Mlinzi juu ya maendeleo ya Imani nchini Irán kwa kuwa katika kipindi hicho alikuwa katibu wa Baraza la Kiroho la jiji la Tihrán na pia katibu wa Baraza la Kitaifa la Irán. Desemba, 1951 aliteuliwa na Mlinzi kuwa Mkono wa Hoja na jukumu lake la kwanza alilopewa wakati huo lilikuwa ni kuhamasisha marafiki wa


Irán kuchangia gharama za ujenzi wa kaburi la Báb kwenye mlima Carmel, kazi ambayo aliifanya kwa ufanisi mkubwa. Mwanzoni mwa mwaka 1953, kwa maelekezo ya Mlinzi alishiriki mikutano ya mabara ya uzinduzi wa mpango wa miaka kumi – Kampala (Afrika), Chicago (America), Stockholm (Ulaya) na New Delhi (Asia). Baada ya kifo cha ghafla cha Mlinzi Novemba 1957, Ali Akbar Furutan alishiriki mkutano maalum wa faragha wa Mikono wa Hoja katika Nchi Takatifu ambapo waliunda Asasi ya Waangalizi. Katika mkutano huo Ali Furutan alichaguliwa kuwa miongoni mwa Mikono tisa wajumbe wa Asasi ya Waangalizi na kuanzia hapo akalazimika kuhamia Haifa kwenye Makao Makuu ya Imani kutekeleza majukumu hayo mapya. Baada ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kuchaguliwa mwaka 1963, Ali Akbar Furutan aliombwa na shirika hilo kuu kukaa makao makuu ya Imani kusaidia majukumu ambayo Nyumba ya Haki iliendelea kumpa, kwa hiyo aliendelea kukaa Haifa hadi mwisho wa maisha yake. Miongoni mwa majukumu aliyopewa ilikuwa ni kuiwakilisha Nyumba ya Haki katika mikutano na matukio makubwa katika sehemu mbalimbali duniani na kuzungumza na mahujaji wakati wakiwa hija kwenye Makao Makuu ya Imani. Kwa mfano, mwaka 1990 alikwenda Urusi kusaidia uundwaji wa Baraza la Kiroho la Jiji la Moscow ambalo lilishindwa kuwepo kwa zaidi ya miaka hamsini kutokana na sera za ukomunisti, na mwaka uliofuata aliiwakilisha Nyumba ya Haki huko jijini Moscow kwenye uchaguzi wa Baraza la Kiroho la Kitaifa la Urusi. Mwaka 1973 Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ilipounda Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa, Ali Akbar Furutan pamoja na Mikono wengine watatu waliteuliwa kuwa miongoni mwa wajumbe wake wa kwanza. Aliendelea kuihudumia Imani kwa moyo wa ibada na utiifu mkubwa hadi mwisho wa maisha yake. Alipokuwa akiongea na vijana katika mikutano mbalimbali kila mara alipenda kuwapa ushauri kwamba: 'Ili uweze kudumu katika njia sahihi na kutochanganywa na nadharia na falsafia za kisomi zinazoibuka kila siku, zingatia na tafakari aya hizi kutoka Kitab-i-Aqdas:

**"Tongoeni aya za Mungu kila asubuhi na jioni. Yeyote ashindwaye kuzitongoa aya hizi hajawa mwaminifu kwa Agano la Mungu na Wasia Wake, na yeyote ageukiaye mbali kutoka aya hizi takatifu katika Siku hii, yu miongoni mwa wale ambao milele yote wamegeukia mbali kutoka kwa Mungu".** (aya ya 149)

Na nyingine: **"Someni Nyaraka Zangu ili muweze kujua kile kilichokusudiwa katika Vitabu vya Mungu, Mtukufu-Kabisa, Mwenye Baraka-Daima".** (aya ya 36). Alisisitiza mara zote kuwa huu

ulipaswa kuwa msingi wa kufanya maamuzi na kuendesha maisha'. Ali Akbar Furutan alifariki siku ya Agano; tarehe 26, Novemba 2003 wakati akiwa anazungumza na mahujaji kwenye ukumbi wa mikutano mjini Haifa, akiwa na umri wa miaka 98. Ali Akbar Furutan alikuwa na uwezo wa kuongea kwa ufasaha lugha tano, na aliandika vitabu na machapisho kadhaa juu ya Imani na elimu ya watoto. Baadhi ya vitabu vyake vya Kiingereza ni 1. *Principles of Education, 2. The Story of My Heart*, *3. Scientific Essays), 4. A Glimpse of History*, *5. Mothers, Fathers and Chidren, na 6. Stories of Baha'u'lláh.*

**4. Ugo Giachery (1896 --1989)**



Ugo Giachery alizaliwa Mei, 1896 katika kisiwa cha Cisily, nchini Italia. Alisoma hadi chuo kikuu na kutunukiwa shahada ya uzamivu katika somo la kemia huko huko Cisily. Baada ya kufundisha chuo kikuu kwa muda alihamia Marekani na kuanzisha biashara. Alikutana na Angeline ambaye alikuwa Mbahá'i na baadaye walifunga ndoa wakiwa jijini New York, mwaka 1926. Siku chache baada ya kufunga ndoa Ugo naye akajitangaza kuwa Mbahá'i. Hapo alianza juhudi za ufundishaji Imani na baadaye alichaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Kiroho la jiji la New York. Mwaka 1947 kwa ushauri wa Shoghi Effendi, Ugo na mke wake waliamua kurudi Italia kama watangulizi. Hivyo waliuza nyumba yao huko Marekani na kuhamia Italia, na baada ya mwezi mmoja tangu kuwasili kwao, raia wa kwanza wa Italia mbali na Ugo akajitangaza kuwa Mbahá'i. Mwaka mmoja baadaye, yaani 1948 Baraza la kwanza la jiji la Roma likaundwa. Jambo hili lilimfurahisha sana Mlinzi na akawaandikia ujumbe wa kuwapongeza. Pamoja na huduma zingine kwa Imani, Ugo alisaidia kufanya tafsiri ya vitabu vingi vya Imani kwa Kiitalia. Huduma zingine alizotoa Ugo ni pamoja na kumsaidia Mlinzi kufanya mikataba na kununua marumaru na vifaa vingine vya ujenzi wa kuba ya kaburi ya Báb ambavyo vilikuwa vinapatikana nchini Italia. Alikuwa akisimamia ununuzi, upakiaji na usafirishaji wa vifaa hivyo kwenda Haifa kwa niaba ya Mlinzi. Vile vile, Ugo Giachery aliiwakilisha Imani katika

shirika la Umoja wa Mataifa mara kadhaa katika miaka hiyo ya mwanzoni ya shirika hilo na alikuwa mmoja wa wajumbe wa asasi zisizo za kiserikali wakati wa kupitisha Azimio la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa mnamo mwaka 1948. Desemba 1951 Mlinzi alimteua Ugo Giachery kuwa Mkono wa Hoja na Machi mwaka uliofuata, 1952 akamteua kuwa mjumbe wa Halmashauri ya Kibahá'i ya Kimataifa. Mwaka 1953 Ugo alisaidia kuundwa kwa Baraza la Kitaifa la Italia na Uswisi na yeye akachaguliwa kuwa mjumbe na aliendelea kuhudumu kwenye Baraza hilo hadi 1962 ambapo kila moja ya nchi hizo ilipopata uwezo wa kuunda baraza lake yenyewe. Baada ya kuteuliwa kuwa Mkono wa Hoja kati ya 1951 na 1957 mara nyingi alipewa jukumu la kumwakilisha Mlinzi katika matukio na mikutano mbalimbali duniani na hasa barani Ulaya. Wakati wa kifo cha Mlinzi Novemba 1957, Ugo alikuwa mmoja wa Mikono wa Hoja walioandaa na kushiriki katika maziko yake jijini London na alikuwa mmoja kati ya Mikono watano waliopewa wajibu wa kupekua kwenye makazi na ofisi ya Mlinzi ili kuona kama kulikuwa na nyaraka zozote kuhusu mrithi wake. Pia alishiriki kwenye kikao maalum cha faragha cha Mikono wa Hoja huko Bahji kilichounda asasi ya Waangalizi. Kuanzia mwanzoni mwa mwaka 1964, Ugo na mkewe Angeline walihamia tena barani Amerika baada ya yeye kupangiwa kuhudumia bara la Amerika kama Mkono wa Hoja. Hata hivyo aliendelea kupewa majukumu ya kuiwakilisha Nyumba ya Haki ya Ulimwengu katika matukio na mikutano mbalimbali duniani. Kwa mfano, mwaka 1967 aliwasilisha nakala ya waraka wa '*Tangazo la Baha'u'llah*' kwa mfalme Malietoa Tanumafili II wa Samoa na mwaka 1968 aliwasilisha ujumbe huo huo kwa utawala wa Vatican kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Mara kadhaa kwa maelekezo ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, alimtembelea Mfalme Malietoa Tanumafili II wa Samoa na mwaka 1976 aliambatana naye kutembelea kaburi la Mlinzi jijini London. Mwaka 1989, Dr. Ugo Giachery akiwa anatembelea Samoa aliugua ghafla na kufariki tarehe 5 Machi, 1989.

## 5. Hermann Grossmann (1899—1968)



Hermann Grossmann alizaliwa Februari 1899 huko Rosario Argentina, lakini wazazi wake walikuwa ni Wajerumani. Baadaye mwaka 1909 familia yake ilirudi Ujermani. Alisomea Leipzig na Hamburg hadi shahada ya juu ya uzamivu katika sheria na sayansi ya siasa. Mwaka 1920 akiwa mwanafunzi chuoni ndipo alipokutana na mafundisho ya Baha'u'lláh, aliyasoma kwa kina hadi akafikia uamuzi wa kuwa Mbahá'i. Baada ya masomo akawa mkurugenzi wa kiwanda kimoja jijini Hamburg na alitumia muda wake wa ziada kufundisha Imani na kuandika katika lugha ya Kiesperanto. Alihudumu kama mjumbe wa Baraza la Kitaifa la Ujerumani tangu mwaka 1924 hadi 1936. Mwaka 1932 aliandika kitabu kuhusu mafundisho ya Imani alichokiita (In the Morning of a New Time- Collapse or Redesign?) 'Asubuhi ya Wakati Mpya – Poromoka au Jipange Upya? '; na pia akaanzisha jarida la Kibahá'i kwa Kiesperanto (La Nova Tago) yaani 'Siku Mpya '. Hivyo vyote baadaye mwaka 1937 vilipigwa marufuku, Imani ikazuiwa na vitabu vyote vya Kibahá'i vikakusanywa na kuchomwa moto na utawala wa Nazi wa wakati huo. Mwaka 1937 Grossmann alifanya hija yake ya kwanza Nchi Takatifu na akapata bahati ya kukutana na Mlinzi. Mwaka 1944 Imani ya Kibahá'i ilishtakiwa na utawala wa Nazi na Dkt. Grossmann akajitolea kusimama kizimbani kama shahidi wa utetezi na baadaye naye alishtakiwa na kuhukumiwa kifungo cha miezi sita kwa makosa ya "kuhujumu juhudi za serikali za vita vya kiuchumi ". Baada ya vita, kwa kuwa hakukuwa na kitabu chochote cha Kibahá'i kilichobakia nchini Ujerumani, Grossmann alianza kuandika na kuchapisha vijitabu vidogo vidogo vya mafundisho ya Imani na alitafsiri kitabu cha Mabonde Saba na Hekima ya 'Abdu'l-Bahá ili vitumike kufundishia Imani. Mwaka 1951 aliteuliwa na Mlinzi kuwa Mkono wa Hoja katika kundi la kwanza la Mikono 12. Mwaka 1953, Grossmann alistaafu kazi yake na akaanza kutumia muda wote kwa shughuli za Imani. Kati ya mwaka 1959 na 1962 Grossmann alitumia muda mwingi kusafiri katika nchi za Amerika Kusini kusaidia kuunda mabaraza ya kitaifa na kuyaimarisha. Miaka yake ya mwishoni, yaani 1962 aliitumia kuandika vitabu na

machapisho ya Kibahá'i nyumbani kwake Neckargemünd, Ujerumani. Baadhi ya vitabu vyake maarufu ni "*What Does the Bahá'í Religion Teach?"* na "*The Baha'i and the Baha'i Community* ". Dkt. Hermann Grossmann alifariki nyumbani kwake tarehe 7 Julai, 1968.

## 6. Horace Holley (1887—1960)



Horace Hotchkiss Holley alizaliwa tarehe 7 Aprili 1887, Connecticut nchini Marekani. Alisoma hadi chuo kikuu katika masomo ya fasihi. Alitambulishwa kwenye Mafundisho ya Imani mwaka 1909 na msafiri mwenzake Bertha Herbert akiwa safarini kwenye meli akielekea Ulaya. Baadaye mwaka huo huo akawa Mbahá'i na wakaoana na huyo mwalimu wake wa Imani Bertha Herbet. Wakiwa Ufaransa mwaka 1911 wakati wa ziara ya 'Abdu'l-Bahá nchini humo Horace na mkewe Bertha walipata baraka ya kukutana Naye jijini Paris. Wakati wa vita vya kwanza vya dunia Horace na familia yake walikimbia Ulaya na kurudi nchini Marekani na kujiunga na jamii ya Wabahá'i wa New York. Mwaka 1923 alichaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Kitaifa la Marekani na aliendelea kuwa mjumbe hadi 1959, alipotakiwa kuhamia Haifa. Hii ilitokana na moyo wake wa kujitoa kubeba majukumu bila kuchoka wala kulalamika kila alipoombwa kufanya hivyo. Mwaka 1951 Mlinzi alimteua Horace Holley kuwa Mkono wa Hoja lakini aliendelea na majukumu yake kama mjumbe na katibu wa Baraza la Kitaifa la wakati huo. Baada ya hapo ilimlazimu pia kusafiri katika nchi mbalimbali ili kumwakilisha Mlinzi katika baadhi ya matukio. Kwa mfano, wakati wa mikutano mikubwa ya mabara mwaka 1953, alishiriki mikutano ya Kampala, Stockholm, New Delhi na Chicago. Baada ya kifo cha Mlinzi alishiriki mkutano maalum wa faragha uliounda asasi ya Watangalizi ambapo naye mwaka 1959 alishiriki kuwa mjumbe wa asasi hiyo hadi alipofariki Julai 1960. Kwa mujibu wa mazungumzo ya wajumbe wenzake, kutokana na tajiriba yake katika mambo ya kiutawala, Horace Holley alisaidia sana wakati wa mkutano maalum wa faragha wa Mikono wa Hoja. Hii ilitokana na ukweli

kwamba kwa miaka mingi hapo kabla alikuwa katibu wa Baraza la Kitaifa la Marekani.

## 7. Leroy Ioas (1896- 1965)



Leroy Ioas alizaliwa Februari 1896 huko Wilminton, Illinois-Marekani. Wazazi wake walijiunga na Imani miaka miwili baadaye, yaani mwaka 1898, hivyo yeye alilelewa ndani ya Imani ya Kibahá'i. Wakati wa ziara ya 'Abdu'lBahá huko Amerika mwaka 1912, Leroy Ioas akiwa na miaka 16, aliambatana na wazazi wake kwenda kumuona na alishuhudia tukio la 'Abdu'l-Bahá kuweka jiwe la msingi la Hekalu mama la Marekani, huko Wilmette. Baada ya masomo yake, akiwa bado kijana aliajiriwa katika shirika la reli. Alifanya kazi katika shirika hilo kwa miaka 40. Baada ya kuanza kazi alihamia San Fransico ambapo yeye akishirikiana na wenzake walifanya ufundishaji wa nguvu hadi wakaweza kuwa na jamii kubwa ya Kibahá'i jijini humo. Alichaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Kiroho la mahali la mji huo, huduma ambayo aliendelea nayo kwa miaka ishirini. Huduma yake katika ngazi ya kitaifa ilianza mwaka 1932 alipochaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Kitaifa la Marekani. Akiwa mjumbe wa Baraza alipewa jukumu la kusimamia ujenzi wa Hekalu mama la Wilmette, na pia kwa kipindi kirefu alikuwa mjumbe wa Kamati ya Ufundishaji ya Kitaifa—kamati iliyoratibu na kufanikisha upanuzi wa Imani katika majimbo yote ya Marekani, Canada na Alaska. Mwaka 1948 Leroy Ioas na wenzake wanne waliiwakilisha Imani kwenye mkutano wa Umoja wa Mataifa wa haki za binadamu huko Geneva. Mwezi Desemba 1951, Mlinzi alimteua Leroy Ioas kuwa Mkono wa Hoja na miezi michache baadaye akamteua tena kuwa katibu wa Halmashauri ya Kibahá'i ya Kimataifa na hivyo akatakiwa kwenda kuishi Makao Makuu ya Imani mjini Haifa. Akiwa Haifa, Mlinzi alimpa jukumu la kusimamia ujenzi wa kuba ya kaburi la Báb na jengo la Makumbusho ya Kimataifa kwenye mlima Carmel. Majukumu mengine muhimu aliyopewa na Mlinzi na kuyafanikisha ni kusimamia mchakato wa ununuzi zaidi wa eneo kwa ajili ya Nyumba ya Ibada itakayojengwa baadaye kwenye mlima Carmel na kusimamia juhudi za kisheria na hatimaye kuwaondoa wavunja Agano

kwenye maeneo matakatifu huko Bahji. Pia alisimamia mchakato wa ununuzi wa eneo zaidi kuongezea ukubwa wa eneo la bustani za Bahji. Alikuwa ni yeye aliyefuatilia kila hatua mpaka kuhakikisha ardhi na majengo yote ya Imani nchini Israel yanapata hatimiliki kutoka serikalini. Mbali na shughuli alizokuwa akizifanya kwenye Makao Makuu ya Imani, Leroy kama Mkono wa Hoja, alimwakilisha Mlinzi katika mikutano na matukio mbalimbali duniani. Baada ya kifo cha ghafla cha Mlinzi Leroy alishiriki kwenye mkutano wa faragha wa Mikono wa Hoja na alikuwa ni mmoja wa Mikono waliochaguliwa kuwa Waangalizi. Baada ya uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, miaka yake ya mwisho aliitumia kwa kutembelea na kuimarisha jamii mbalimbali za Amerika, ingawa afya yake ilikuwa inaendelea kuwa dhaifu. Mwezi Julai, 1965, Leroy Ioas alifariki akiwa mjini Haifa, baada ya kuzidiwa na kulazwa hospitalini. Amezikwa katika makaburi ya Kibahá'i, Haifa.

### 8. William Sutherland Maxwell (1874 – 1952)



William Maxwell alizaliwa Novemba 1874, jijini Montreal- Canada. Tangu utoto wake alipenda fani ya sanaa na uchoraji. Baada ya kumaliza masomo ya sekondari alianza kufanya kazi kwenye kampuni ya ujenzi ya kaka yake. Baadaye mwaka 1895 alihamia Boston Marekani na kuanza kufanya kazi za uchoraji huku akijifunza masomo ya usanifu majengo kwa masomo ya jioni. Huko alikutana na profesa mmoja mahiri wa usanifu majengo ambaye alifurahishwa na juhudi yake, na hivyo akamfundisha kwa ukaribu zaidi mbinu mbalimbali za usanifu wa kiuhandisi. Masomo yake ya kitaaluma yalimchukua miaka kumi hadi kuhitimu. Alisoma katika chuo kikuu cha MIT nchini Marekani na baadaye chuo kingine nchini Ufaransa ambacho kilisifika sana kote duniani kwa taaluma za usanifu na uchoraji. Mnamo mwaka 1900 alihitimu akiwa na ujuzi mkubwa katika usanifu wa majengo. Alirudi Canada na kuwa mshirika katika kampuni ya kaka yake na kutokana na ujuzi wake waliweza kupata kazi za miradi mikubwa za usanifu majengo nchini humo. Kipindi kile akiwa masomoni jijini Paris, Ufaransa alikutana na Mason

Remey na Randolph Bolles ambao walimfundisha Imani ya Kibahá'i ambayo aliendelea kujifunza. Baadaye mwaka 1902 alifunga ndoa jijini London na May Ellis Bolles, dada yake Randolph Bolles, mmoja wa walimu wake wa Imani. Mwaka 1909 naye akajitangaza kuwa Mbahá'i. Baada ya kurudi kwao Canada, yeye na mkewe wakawa Wabahá'i motomoto na nyumbani kwake ikawa ndiyo kitovu cha shughuli za Kibahá'i jijini Montreal. Mwaka 1910 William na May walipata mtoto wa kike ambaye walimuita Mary Maxwell ambaye walimlea katika maadili ya Kibahá'i. Wakati wa ziara Yake nchini Canada mwaka 1912, 'Abdu'l-Bahá alifikia nyumbani kwao. William Maxwell aliendelea na kazi yake ya usanifu majengo na wakati huo huo akiihudumia Imani. Yeye na mkewe walikwenda hija Haifa mara kadhaa na safari mojawapo waliambatana na binti yao Mary wakati akiwa na miaka 16. Katika taaluma yake ya usanifu majengo, Maxwell aliheshimika sana na alipewa tuzo kadhaa za kutambua mchango na umahiri wake katika fani hiyo nchini Canada. Mwaka 1937 mtoto wao Mary aliolewa na Shoghi Effendi na baadaye akajulikana kama Amatu'l Bahá Ruhiyyih Khanum. Mwaka 1940 wakiwa mjini Buenos Aires, Argentina, mkewe May aliugua ghafla na kufariki. Baada ya tukio hilo Mlinzi alimuita William kwenda kukaa Haifa ambapo alikaa tangu wakati huo hadi 1949. Katika kipindi hicho akiwa Haifa ndipo alijitolea kusanifu mchoro wa kuba ya kaburi la Báb ambao aliusanifu mwaka 1942. Mbali na hilo, pia alimsaidia Mlinzi kazi zingine kama vile kupokea barua, kupokea wageni na kufanya mawasiliano na viongozi wa serikali kwa niaba ya Mlinzi. Baada ya kuishi Haifa kwa miaka kadhaa afya yake ilianza kudhoofu na hivyo akaondoka kurudi Montreal Canada akiwa na muuguzi wa kumsaidia. Desemba 1951 aliteuliwa na Mlinzi kuwa Mkono wa Hoja. Miezi michache baadaye, Machi 25, 1952 alifariki akiwa nyumbani kwake jijini Montreal, Canada.

## 9. **Charles Mason Remey** (1874 -1974)

Charles Mason Remey alizaliwa Mei, 1874 nchini Marekani. Alisomea usanifu majengo katika chuo kikuu kati ya mwaka 1893 na 1896. Alifundishwa Imani na rafiki zake hadi akawa Mbahá'i mwaka 1999 akiwa jijini Paris, Ufaransa. Mwaka 1901 alikwenda hija yake ya kwanza na akapata bahati ya kukutana na 'Abdu'l-Bahá. Baadaye alirudi Marekani na kuanza kufundisha Imani na mwaka 1909 alichaguliwa kuwa mjumbe wa 'Bahai Temple Unity' shirika la kwanza la kiutawala la kitaifa lililotangulia Baraza la Kitaifa la Marekani. Mwaka 1922, Mlinzi aliwaita kwa mashauriano baadhi ya Wabahá'i mashuhuri wa Amerika akiwemo Mason Remey na baada ya

mashauriano kila mmoja wao alikabidhiwa nakala ya Wasia na Agano na akawasisitiza kuwa wausome kila mara na kufanya jitihadi kulinda umoja wa Wabahá'i. Mwaka 1931 Remey alimuoa Getrude Klemm- mjane ambaye mwaka mmoja baadaye alijiua kwa kujipiga risasi. Tangu mwaka 1939 hadi 1949 Mason Remey alifanya safari nyingi za ufundishaji wa Imani katika bara la Amerika na Ulaya. Mwaka 1950, Mlinzi alimuita Haifa na mwaka uliofuata 1951, alimteua kuwa Mkono wa Hoja na pia mwenyekiti wa Halmashauri ya Kimataifa ya Kibahá'i aliyokuwa ameiunda. Kama Mkono wa Hoja, alimwakilisha Mlinzi katika matukio mbalimbali, ikiwemo mkutano wa Kampala, New Delhi, Chicago na Stockholm akiwa na Mikono wenzake. Vile vile, kama msanifu majengo, alisanifu mchoro wa Jumba la Makubusho ya Kibahá'i lililoko Haifa, Hekalu mama la Kampala na la Sydney-Australia. Mwaka 1957 alipata tatizo la kutosikia vizuri kwa kiwango ambacho alihitaji kifaa maalum cha kumsaidia kusikia. Mwaka 1957 baada ya maziko ya Mlinzi huko London, Remey akiwa na Mikono wenzake kama vile Ruhiyyih Khanum, Amelia Collins, Ugo Giachery, na Leroy Ioas, Novemba 15, waliwasili Haifa na kufunga ofisi na kabati za Mlinzi ili ziwe salama kwa ajili ya ukaguzi hapo baadaye. Siku chache baadaye baada ya kundi la Mikono wote kujiridhisha kwamba hakukuwa na dalili zozote za Mlinzi kuwa ameteua mrithi wake, Charles Mason Remey aliungana na Mikono wengine wote kusaini hati ya tamko kuwa hakukuwa na wasia wa Shoghi Effendi, na pia hakuna mtu aliyekuwa ameteuliwa naye kuwa mrithi wake. Na pia alishiriki kuunda asasi ya Waangalizi ambayo naye pia alichaguliwa na wenzake kuwa mjumbe. Katika mkutano wa pili wa faragha wa Mikono wa Hoja mwaka 1958 Remey alitoa hoja kuwa nafasi ya Mlinzi ilipaswa kuendelea kuwepo, lakini hoja hiyo ilikataliwa na Mikono wote. Na katika mkutano wa tatu wa faragha wa Mikono, Novemba 1959, mkutano uliamua kuwa asasi ya Halmashauri ya Kibahá'i ya Kimataifa kuanzia wakati huo ingekuwa ya kuchaguliwa, kama matayarisho ya uundwaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Mason Remey alikataa kusaini azimio hilo la maamuzi, akajiuzulu ujumbe wa asasi ya Waangalizi na kuondoka Nchi Takatifu kwenda Marekani. Miezi michache baadaye, Aprili 1960, Mason Remey alijitangaza kuwa yeye alikuwa ni mrithi wa Mlinzi - yaani Mlinzi wa pili, japokuwa hapo nyuma alikuwa ameshiriki kusaini tamko la kwamba Mlinzi hakuwa na mrithi na hakukuwa na uwezekano wowote wa kuwa na Mlinzi mwingine. Baada ya asasi ya Mikono wa Hoja kumpa nafasi ya kujirudi bila mafanikio, hatimaye 26 Julai, 1960, walifanya uamuzi na kumtangaza Charles Mason Remey kuwa mvunja Agano, na hivyo tangu wakati huo akapoteza sifa za kuwa Mkono wa Hoja kwa kuwa sasa hakuwa Mbahá'i tena.

Wabahá'i kote duniani walipuuza madai yake na kuwa watiifu kwa asasi ya Mikono wa Hoja, na wale wachache sana waliomfuata nao walifukuzwa katika Imani. Kipindi kifupi kilichofuata yeye na waasi wenzake kwa haraka walianza kugombana na kusambaratika vipande vipande hali iliyoendelea hadi wakakosa mwelekeo na kapotea. Mason Remey alifia nchini Italia mwaka 1974 akiwa katika hali ya kuhuzunisha sana.

### 10. Ṭaráẓu'lláh Samandarí (1874 - 1968)




Tarazu'lláh Effendi Samandari alizaliwa mwaka 1874, Qazvin, Irán. Baba yake aliyeitwa Samandari alikuwa mfuasi mwaminifu wa Baha'u'lláh na bibi yake alikuwa Mbábi na mshirika wa karibu wa Tahirih. Tarazu'lláh alilelewa na wazazi wake pamoja na bibi yake katika maadili ya Kibahá'i. Kwa kuwa wakati huo hakukuwa na shule katika eneo lao, Tarazu'lláh alifundishwa nyumbani na Mulla Ali. Ni mwalimu ambaye Baha'u'lláh wakati fulani alimsifu kuwa alikuwa mwalimu bora wa Kibahá'i wa kipindi hicho. Alifundishwa sarufi ya lugha ya Kiajemi na Kiarabu na pia sanaa ya mwandiko (kaligrafia). Jina la Tarazu'lláh alipewa na Baha'u'lláh likimaanisha 'Pambo la Mungu'. Alipofikisha miaka 13 alianza kumsaidia baba yake kazi ya biashara na pia akaanza kufanya kaligrafia ya maandiko ya Imani. Alikwenda safari ya hija ya kwanza 'Akká akiambatana na dada yake na mama yake mdogo. Wakati huo Tarazu'lláh akiwa na umri wa miaka 16. Hiyo ilikuwa mwaka 1891 ambapo alipata baraka iliyokuwa nadra sana ya kufika mbele ya Baha'u'lláh katika umri ule mdogo. Alikaa 'Akká kwa miezi sita na kupewa fursa ya kuwepo katika matukio kadhaa ambayo alikuwepo Baha'u'lláh Mwenyewe. Mara mbili alishuhudia Baha'u'lláh Akifunua Maandiko Matakatifu na pia alihudhuria maadhimisho ya sikukuu za Naw Rùz na Ridván za mwisho ambazo Baha'u'lláh Alishiriki; na vile vile alipata baraka ya kuwepo Bahji siku ya kupaa kwa Baha'u'lláh, 1892. Pia alihudhuria tukio la kusomwa kwa Wasia na Agano Lake mbele ya familia Yake na waumini. Akisimulia baadhi ya matukio Tarazu'lláh alisema ''Siku ya Naw

Rùz, Baha'u'lláh. Aliwapokea wageni katika bustani iliyokuwa imepambwa kwa miti aina ya michungwa. Washairi maarufu Nabil na Andalib walikuwa wametunga mashairi kwa ajili ya siku kuu hiyo ambayo yaliimbwa kwa umaridadi mkubwa. Wageni waliohudhuria walipata baraka ya kumsikia Baha'u'lláh akifunua aya takatifu. Baadaye karamu ya chakula iliandaliwa na kila mmoja alishiriki pamoja Naye". Akisimulia tukio mojawapo la maadhimisho ya siku za Ridván, Tarazu'lláh alisema "Alitupokea wageni wote-waumini, wenyeji na mahujaji katika Bustani ya Ridván. Mshairi maarufu Andalib alighani mashairi aliyoyatunga maalum kwa ajili ya tukio hilo. Baha'u'lláh alimimina baraka kwa kila aliyekuwepo ambapo tulisimama katika safu, akitugawia kwa mkono Wake maji ya waridi, nyama na machungwa, na kwa Andalib alimpa chupa ya maji-waridi na machungwa mawili". Huu ulikuwa ni upendeleo mkubwa ambao Baha'u'lláh aliamua kumtunukia kijana huyo kutokana na upendo wake Kwake. Mwaka 1895 Tarazu'lláh alimuoa Taraziyyih jina alilopewa na Baha'u'lláh pia, ambaye baadaye alifungua shule ya Kibahá'i kule Qazvin. Mwaka 1898 alikwenda hija ya pili na mwaka 1908 alifanya hija ya tatu ambapo 'Abdu'l-Bahá alimpa waraka maalum kwa ajili ya Wabahá'i wa Irán akiwahimiza kuwa watiifu kwa Agano. Mwanzoni mwa mwaka 1910 alikwenda tena Nchi Takatifu ambapo 'Abdu'l-Bahá alimshauri akakae Qazvin ili afya yake iimarike na tangu hapo aliikaa Qazvin kwa miaka 17 akihudumu kama katibu wa Baraza la Mahali la Qazvin. Baada ya kupaa kwa 'Abdu'l-Bahá, Mlinzi alimwagiza kuandaa makusanyo ya nakala za Nyaraka kadhaa za Baha'u'lláh na kuzithibitisha kwa kuwa alikuwa akiujua vyema mwandiko wa Baha'u'lláh. Kazi hiyo aliifanya kwa miaka miwili na aliwasilisha nyaraka hizo zikiwa katika juzuu 18. Kuanzia mwaka 1927 alianza tena kuwa mwalimu msafiri katika majimbo mbalimbali ya Irán, yakiwemo Yazd, Zanjan, Tehrán, Shiraz, Isfahán na Adhirbaijan. Mwaka 1947 aliweza kupata nakala halisi ya **Kitabu cha Yakini** huko Irán ambayo aliituma kwa Mlinzi. Mwaka 1951 Tarazu'lláh aliteuliwa na Mlinzi kuwa Mkono wa Hoja na hivyo akaanza majukumu ya kimataifa katika wadhifa huo. Mwaka 1953 wakati wa kuzindua mpango wa miaka kumi ilifanyika mikutano ya uzinduzi katika mabara manne na Tarazu'lláh alihudhuria yote minne akiwa na Mikono wengine. Mwaka 1957 alihudhuria mazishi ya Mlinzi jijini London na pia mkutano wa faragha wa Mikono wote uliothibitisha kutokuwepo kwa mrithi wa Mlinzi na kuundwa kwa asasi ya Waangalizi. Aliendelea kufanya majukumu kama Mikono wa Hoja wengine ikiwemo kufanya mikutano ya kuhamasisha ufundishaji katika mabara na kuhudhuria konvensheni katika nchi mbalimbali. Kwa mfano, alishiriki konvensheni ya Afrika Mashariki, India, Burma na Uturuki. Pia

alishiriki mikutano yote ya Mikono wa Hoja, maadalizi na pia uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu mwaka 1963. Katika mkutano wa dunia wa kuadhimisha miaka mia moja ya kujitangaza kwa Baha'u'lláh uliyofanyika jijini London mwaka 1963, Tarazu'lláh alipewa nafasi na kuelezea kumbukumbu yake ya kufika mbele ya Baha'u'lláh akiwa kijana mdogo wakati huo. Kati ya mwaka 1967 na 1968 alitembelea Marekani na baadaye alirudi Nchi Takatifu na muda mfupi baadaye aliugua na Septemba 2, 1968 alifariki mjini Haifa akiwa na umri wa miaka 94.

## 11. George Townshend (1876--1957)



George Townshend alizaliwa Juni, 1876 mjini Dublin, Ireland. Alisoma hadi chuo kikuu cha Oxford akawa mwandishi wa habari na baadaye mwaka 1904 alihamia Marekani. Akiwa na umri wa miaka 31 alipewa daraja la ukasisi katika kanisa la Anglikana nchini Marekani. Akiwa huko aliendelea kusoma hadi akafikia kiwango cha kuwa profesa msaidizi katika fani ya lugha ya Kiingereza. Alioa na kupata watoto wawili ambao baadaye walikuja kuwa Wabahá'i. Baadaye alirudi nchini mwake na kuendelea kutoa huduma za uchungaji hadi akafikia ngazi ya kuwa askofu wa kanisa kuu la Anglikana la Dublin. Lakini kutoka mwaka 1918 alikutana na mafundisho ya Baha'u'lláh na akaanza kujifunza Imani ya Kibahá'i na tangu mwaka huo akaanza mawasiliano na Abdu'l-Bahá kuhusu mafundisho mbalimbali ya Imani. Ni kutokana na mawasiliano haya ndipo akawa amepata uelewa mkubwa juu ya Mafundsho ya Imani. Kutokana na uelewa wake mpya wa mafundisho ya Imani akaandika vitabu viwili *("The Heart of the Gospel" na "The Promise of All Ages*"). Hatua hii ilisababisha mgogoro kati yake na makasisi wenzake kwani walimuona kama ni mtu aliyekuwa amechanganyikiwa. Hivyo, mwaka 1921, akiwa na umri wa miaka 70 akaamua kutangaza kujiuzulu nyadhifa zake zote katika kanisa na kutangaza rasmi kuwa mfuasi wa Baha'u'lláh. Na hivyo akatoka kwenye majengo ya kanisa na kuhamia mtaani na kuendelea na shughuli za ufundishaji wa Imani ya Kibahá'i. Kipindi kifupi baadaye

akachaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la kwanza la mji wa Dublin. Baadaye kuanzia mwaka 1926 Mlinzi akaanza kumpa majukumu ya kumsaidia katika kazi za uandishi kama vile kuhariri maandiko yake. Townshend ndiye aliyeandika utangulizi wa kitabu muhimu cha historia kilichoandikwa na Mlinzi cha Kiingereza kiitwacho “God Passes By” na vile vile aliandika utangulizi kwenye tafsiri ya Kiingereza ya “Wana Mapambazuko”. Mnamo mwaka 1951 aliteuliwa na Mlinzi kuwa Mkono wa Hoja. Katika siku zake za mwisho akiwa amezidiwa na ugonjwa ujulikanao kama ‘Parkinson’s disease’, watoto wake Brian na Una walimsaidia kumalizia kuandika kitabu chake cha mwisho kiitwacho “Christ and Baha’u’lláh”. Alifariki Machi, 1957 mjini Dublin-Ireland. Baadhi ya vitabu alivyoandika ni 1. *The Mission of Bahá’u’lláh, 2. The Promise of All Ages, 3. The Heart of the Gospel*, *4. Christ and Bahá’u’lláh, na 5. ‘Abdu’l-Bahá, the Master*

**12. Valiyu’lláh Varqa (1884- 1955)**



Valiyu’lláh Varqa alizaliwa mwaka 1884 mjini Tabriz, Irán. Alikuwa ni mtoto wa tatu wa Ali Muhammad Varqa ambaye aliuawa kifo cha kishahidi na pia alikuwa ametajwa kuwa Mkono wa Hoja. Baada ya kuuawa kuuawa kishahidi kwa baba yake na kaka yake (Ruhu’lláh), wakati huo akiwa na umri wa miaka minane tu, yeye akalelewa na mama yake mjini Tabriz. Alipofikisha umri wa miaka 16 alihamia Tehrán kwa kaka yake Azizu’lláh na kuanza masomo katika shule ya Kibahá’i. Baadaye alikwenda kwenye chuo kikuu cha American University huko Beirut kwa ajili ya masomo ya juu. Akiwa chuoni, wakati wa likizo alikuwa akienda Nchi Takatifu na kupata bahati ya kukutana na ‘Abdu’l-Bahá ambaye Aliwawekea mpango yeye na wanafunzi wenzake wawe wakipata masomo ya Imani kutoka kwa Mirza Haydar-Ali. Baada ya kumaliza masomo mwaka 1909 alirudi Irán na kuajiriwa katika ofisi ya ubalozi wa Urusi jijini Tehrán na wakati huo huo akihudumia Imani. Alioa na kubahatika kupata watoto watano, mmoja wao aliyeitwa Ali Mohammad

Varqa naye alikuja kuteuliwa kuwa Mkono wa Hoja. Wakati wa ziara ya ‘Abdu’l-Bahá nchini Marekani aliitwa na kuteuliwa kuwa kati ya timu ya waumini walioambatana Naye kwenye ziara hiyo. Baada ya ziara hiyo alirudi Tehrán na kuajiriwa na ubalozi wa Uturuki nchini Irán. Baada ya miaka kadhaa alijiuzulu kazi na akaendelea kuihudumia Imani, na mnamo mwaka 1938 baada ya kifo cha Haji Amin aliteuliwa na Mlinzi kuwa mdhamini wa Huq´uqu´lláh, jukumu aliloendelea nalo hadi mwisho wa maisha yake. Mwaka 1951 Mlinzi alimteua Valiyu’lláh Varqa kuwa Mkono wa Hoja. Mnamo mwaka 1953 alitumwa na Mlinzi kwenda kuhudhuria mikutano kadhaa ya mabara ya uzinduzi wa Mpango wa miaka kumi na kutembelea nchi kadhaa zikiwemo Brazil, Marekani, Sweden, Ujermani, India, Uturuki, Misri, Iraq na Syria ili kuimarisha jamii za Kibahá’i na kuhamasisha shughuli za ufundishaji. Mwaka 1955 kutokana na afya yake kuzidi kuzorota alielekea Ulaya kwa ajili ya matibabu na mnamo Novemba 12, 1955, alifariki dunia jijini Sturtgart, Ujerumani.

***Kundi la pili: Walioteuliwa tarehe 29 Februari, 1952***

| **Na** | **Jina La Mkono wa Hoja** | **Kuzaliwa** | **Kufariki** |
|---|---|---|---|
| 1 | Shu'a'u'lláh 'Ala'i | 1889 | 1984 |
| 2 | Musa Banani | 1886 | 1971 |
| 3 | Clara Dunn | 1869 | 1960 |
| 4 | Dhikru'lláh Khadem | 1904 | 1986 |
| 5 | Adelbert Muhlschlegel | 1897 | 1980 |
| 6 | Siegfried Schopflocher | 1877 | 1953 |
| 7 | Corinne True | 1861 | 1961 |

### 1. Shu'á'u'lláh 'Alá'í (1889 -1984)



Shu’a’u’lláh Ala’i alizaliwa Novemba 1889 jijini Tihrán akiwa mtoto wa pili wa Siyyid Muhammad Nazimu'l-Hukama. Huyu Siyyid Muhammad Nazimu'l-Hukama alikuwa msomi mkubwa wa dini ya kiislam kabla ya kuwa Mbahá’i. Shu’a’u’lláh akiwa na umri wa miaka saba, baba yake alipokea waraka maalum alioandikiwa na ‘Abdu’l-Bahá ambao alipewa nakala na baba yake kuukariri. Aliukariri na akawa anaughani katika maisha yake yote. Aliupenda sana kwa kuwa ulihusiana na jina lake Shu’a’u’lláh ambalo humaanisha ‘mwale wa jua la utakatifu’. Sehemu ya waraka huo ilisema:

*‘’Ee moto wa upendo wa Mungu! Mwale lazima utoe mwanga na jua lazima lichomoze; mwezi lazima uangaze na nyota lazima zimulike. Kwa kuwa wewe ni mwale, msihini Bwana kukuwezesha kutoa mwangaza na kuelimisha, kuangaza peo na kuteketeza dunia kwa moto wa upendo wa Mungu. Nategemea kuwa utaweza kufikia daraja hilo, la, kulipita. Utukufu Wake uwe juu yako”.*

Shua’u’lláh alisoma shule ya Kibahá’i ya Tarbiyat jijini Tihrán na baadaye alikwenda chuoni na kusomea uhasibu. Baada ya kumaliza masomo aliajiriwa kama mhasibu wa idara ya polisi na baadaye wizara ya fedha. Aliendelea na kazi ya uhasibu serikalini na huku akiihudumia Imani. Mwaka 1927, kutokana na weledi wake mkubwa katika fani hiyo, aliteuliwa kuwa mjumbe mwanzilishi wa bodi ya benki kuu ya Irán. Uaminifu wake na weledi katika kazi ulimfanya aaminike sana na viongozi wa serikali kiasi kwamba vingozi wake walipenda kila kazi nyeti akabidhiwe yeye kuisimamia. Kwa mfano, wakati utawala wa serikali ulipotaka kupata thamani ya vito vya mfalme, aliteuliwa yeye kusimamia kazi hiyo (thamani yake ilikuwa dola za Marekani bilioni 7 wakati huo). Mwaka 1913 alichaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Kiroho la jiji la Tehrán, huduma ambayo aliendelea nayo hadi mwaka 1943; na mwaka 1944 alichaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Kitaifa la Irán. Mwaka 1952, alikwenda hija Nchi Takatifu, na baada ya safari hiyo akateuliwa na Mlinzi kuwa Mkono wa Hoja ya Mungu. Baada ya uteuzi huo alistaafu ujumbe wa Baraza ili afanye majukumu ya kimataifa. Mwanzoni mwa mwaka 1953, Shu’a’ulláh alihudhuria mikutano minne ya mabara ya uzinduzi wa mpango wa miaka kumi-Kampala (Afrika), Wilmette (Amerika), New Delhi (Asia) na Stockholm (Ulaya). Vile vile, katika vipindi mbalimbali alitembelea jumuiya za Kibahá’i za nchi mbalimbali katika mabara hayo. Pamoja na majukumu mengine, pia Shu’a’u’lláh alipewa na Mlinzi jukumu la usimamizi wa maeneo matakatifu na mali za Kibahá’i nchini Irán. Mwaka 1978 alihamia nchini Ufaransa na baadaye mwaka 1981 alihamia tena Arizona nchini Marekani. Mwaka 1984 Novemba, ikiwa ni siku yake ya kutimiza miaka 96 alifariki dunia nyumbani kwake Arizona–

Marekani.

## 2. Músá Banání (1886-1971)



Musa Banani alizaliwa katika familia ya Kiyahudi jijini Baghdád, Iraq mwaka 1886. Baba yake alifariki yeye akiwa mtoto wa miaka minne, hivyo alilelewa na kaka yake. Akiwa na umri wa miaka 12 yeye na kaka yake walihamia Uajemi na kuanza kujitafutia maisha kwa kufanya biashara. Katika mazingira magumu ya maisha ya utotoni Musa hakuweza kwenda shule, hivyo aliweza kujifunza kuandika jina lake tu kwa herufi za kiyahudi alizofundishwa akiwa mtoto. Wakiwa nchini Iran kaka yake alikutana na mafundisho ya Imani na baada ya muda akawa Mbahá'i, lakini yeye hakupenda kabisa kujihusisha na mambo ya dini. Mwaka 1911 wakiwa wanaendelea na shughuli za biashara mjini Kirmanshah lilitokea tukio ambalo lilikuja kubadilisha maisha yake. Mwalimu wa Kibaha'i aliyeitwa Siyyid 'Abdul-Ḥusayn-Ardistáni alikuwa ametumwa na 'Abdu'l-Bahá kwenda mjini humo kuwatembelea Wabahá'i. Baada ya mkutano mwalimu huyo alipiga picha ya pamoja ya kikundi cha Wabahá'i wa mji huo akiwemo kaka yake Mussa Banani. Baada ya siku chache yule mwalimu wa Imani alikamatwa akateswa na ile picha ya Wabahá'i waliyopiga pamoja naye ikakamatwa na kutumika kuwasaka Wabahá'i wa mji huo. Katika msako huo Mussa Banani naye akakamatwa kimakosa na kuwekwa gerezani akidhaniwa ni kaka yake ambaye walikuwa wanafanana sana. Humo gerezani alishuhudia na kushangazwa na mzee mmoja Mbahá'i aliyeitwa Abrar aliyekataa kuikana Imani licha ya mateso mengi aliyofanyiwa. Mussa alikataa katakata kuwa yeye si Mbahá'i na akathibitisha hilo kwa kuidhihaki Imani hadi akaachiwa huru. Lakini tangu wakati huo akaanza kupata tatizo lililomsumbua sana hata akawa anakosa usingizi. Kila mara alisumbuliwa na wazo la kuikana Imani kule gerezani ambapo alikuwa hata hajui inafundisha

nini. Aliona lilikuwa kama jambo baya na la kijinga, hakujua ni kwa nini wazo hilo halikutoka akilini mwake muda wote ingawa alijaribu kujisahaulisha lakini bado liliendelea kumsumbua sana na hasa alipokuwa akikumbuka mateso aliyopata yule mzee kule gerezani. Hali ile ya kukosa usingizi iliendelea kwa kipindi kirefu mpaka akawa kama anachanganyikiwa. Hatimaye katika juhudi ya kuondokana na hali hiyo ikamfanya ajifunze Imani ili kuijua na baada ya kuyaelewa mafundisho na kuyapenda hatimaye akaamua kuwa Mbahá'i. Baada ya hapo hali ile ya mwanzo iliyokuwa inamsumbua ikaisha na akaipenda sana Imani. Moja ya maamuzi yake ya mwanzoni baada ya kuwa Mbahá'i yalikuwa ni kwamba lazima aje kufunga ndoa na Mbahá'i ili akizaa watoto waweze kulelewa katika mafundisho ya Kibahá'i. Baada ya miaka kadhaa Musa alioa binti wa Kibahá'i.Alipofanya uchunguzi alikuja kugundua kuwa huyo mke wake alikuwa ni binti wa Siyyid 'Abdul-Ḥusayn-Ardistáni–yule mwalimu wa Imani aliyekuwa amewatembelea Wabahá'i wa Kirmanshah mwaka 1911.Tukio ambalo lilisababisha yeye kukamatwa kulikompelekea kuwa Mbahá'i. Mwaka 1934 Mussa Banani alifanya hija yake ya kwanza huko Nchi Takatifu ambako alipata fursa ya kukaa na Mlinzi Shoghi Effendi kwa siku 26, kitu ambacho kilimjengea upendo mkubwa kwa Mlinzi, upendo uliodumu maisha yake yote. Nchini Irán Mussa Banani pamoja na mambo mengine pia alifanya kazi ya kutambua na kuyapata maeneo muhimu ya kihistoria ya Imani, jukumu ambalo lilisababisha yeye kununua nyumba aliyozaliwa Baha'u'lláh huko Tehrán kwa ajili ya Imani. Aliendelea kuihudumia Imani huku akifanya biashara ambayo sasa ilishamiri sana mjini Kirmanshah. Mwaka 1950 Mlinzi alipotoa wito kwa waumini kwenda kufungua bara la Afrika kwa ajili ya Imani, Musa Banani aliamua kwenda kuwa mtangulizi Afrika pamoja na kwamba alikuwa na biashara nzuri sana kule Irán. Aliambatana na mke wake, watoto wake na mume wa mtoto wake Viollete- Ali Nakhjavan na wote walihamia na kuishi Kampala, Uganda. Alifanya kazi kubwa ya kueneza Imani katika nchi mbalimbali za Afrika. Mwaka 1952 alipokwenda hija Haifa alikutana na Mlinzi ambaye alikuwa akimpa maelekezo ya jinsi Imani itakavyopanuliwa katika bara la Afrika. Siku yake ya mwisho ya hija ndipo Mlinzi akamwambia kuwa amemteua kuwa Mkono wa Hoja. Yeye alikataa kusema kuwa hakuwa na uwezo na hadhi ya kuwa Mkono wa Hoja, 'sijui kusoma wala kuandika na si muongeaji mzuri, kwa nini usimpe nafasi hiyo Ali Nakhjavan ambaye naona ana uwezo huo?'. Mlinzi alijibu "ni kuinuka

kwako kulikolikomboa bara la Afrika, Nakhjavan nafasi yake itakuja muda ukifika, na kwa taarifa yako nimeshautangazia ulimwengu wa Kibahá'i kwamba nimekuteua kuwa Mkono wa Hoja." Hivyo Februari 29, 1952 Mussa Banani alitangazwa kuwa Mkono wa Hoja. Pamoja na majukumu mengine, Mussa Banani kwa maelekezo ya Mlinzi alisaidia kutafuta na kununua eneo la ujenzi wa Hekalu Mama la Afrika jijini Kampala. Baada ya kifo cha Mlinzi alishiriki katika mikutano, maamuzi na majukumu yote yaliyofanywa na Mikono wa Hoja. Kuanzia mwaka 1960 afya yake ilianza kudhoofika hadi akalazimika kukatwa mguu mmoja na jicho lake moja kushindwa kuona kabisa. Hata hivyo, aliendelea na huduma kwa Imani hadi alipopata kiharusi na kushindwa kuamka kabisa. Alifariki tarehe 4 Septemba, 1971 jijini Kampala na akazikwa kwenye viunga vya Hekalu Mama la Afrika kama ilivyokuwa shauku yake ya siku zote. (9)

## 3. Clara Dunn (1869-1960)



Clara Davis Dunn alizaliwa Mei 29,1869 jijini London, lakini alikulia Canada kutokana na ugomvi wa wazazi wake. Alipitia maisha magumu sana katika maisha yake ya mwanzoni, kama vile kufiwa na mume wake wa kwanza, kufiwa na mtoto wake na ukosefu wa kipato cha kuendesha maisha yake. Mwaka 1902 alihamia Marekani, na mwaka 1907 alikutana na Hyde Dunn huko jijini Washington ambaye alimfundisha Imani hadi akawa Mbahá'i. Baada ya miaka 5 kupita alikutana tena na Hyde katika mkutano wa 'Abdu'lBahá wakati wa ziara yake huko Amerika mwaka 1912. Baadaye, mwaka 1916 mke wa kwanza wa Hyde Dunn alifariki na mwaka mmoja baadaye wakafunga ndoa na Clara. Mwaka 1920 Hyde na Clara Dunn waliamua kwenda kuwa watangulizi nchini Australia. Hii ilikuwa baada na kusoma wito wa 'Abdu'l-Bahá uliowataka waumini kwenda kufungua nchi nyingine kwa ajili ya Imani. Hivyo, 10 Aprili, 1920 walifika jijini Sydney, Australia. Kwa miongo miwili iliyofuata Clara na mumewe walifanya juhudi bega kwa bega kusitawisha Imani katika bara hilo hadi mumewe alipofariki 1941. Walifanya kazi kubwa ya ufundishaji na uanzishwaji wa Baraza la

Kwanza la Kitaifa la Australia manmo mwaka 1934. Kuanzia mwaka 1943 alifanya safari za ufundishaji katika miji mbalimbali ya Australia baada ya kuombwa na Baraza la Kitaifa. Tarehe 29 Februari, 1952 Clara Dunn alitangazwa na Mlinzi kuwa Mkono wa Hoja. Baada ya kifo cha Mlinzi, Clara, licha ya umri mkubwa na kuwa na afya duni, alishiriki na kutia saini kukubaliana na maamuzi yote muhimu yaliyofanywa na Mikono wa Hoja. Mwaka 1958 ndoto yake ilitimia aliposhiriki kuweka jiwe la msingi la hekalu mama la Australia. Alifariki 18 Novemba, 1960 na kuzikwa kando na kaburi la mumewe jijini Sydney, Australia.

## 4. Dhikru'lláh Khadem (1904-1986)



Dhikru'lláh au Zikrulláh Khadem alizaliwa 1904 jijini Tehrán akiwa mtoto wa pili wa Nasru'lláh Khadem ambaye alikuwa mtumishi wa 'Abdu'l-Bahá mjini 'Akká kwenye miaka ya 1890. 'Abdu'l-Bahá ndiye aliyempa baba yake jina la Khadem (mtumishi). Baada ya kumaliza masomo yake, Zikrullah alifundisha shule ya Kibahá'i ya Tarbiyat mjini Tehran kabla ya kujiunga na kampuni ya mafuta ya Waingereza kama mtafsiri na mwalimu wa Kiajemi kwa wafanyakazi wa kiingereza. Baadaye alifanya kazi kwenye ubalozi wa Iraq mjini Tehran.Alikuwa na ujuzi katika lugha za Kiajemi, Kiarabu, Kiingereza na Kifaransa. Mwaka 1925 alienda hija kwenye Makao Makuu ya Imani ambapo Mlinzi alimpa majukumu ya kutembelea waumini wapya na kupiga picha za maeneo muhimu ya kihistoria ya Imani nchini Iran. Zikrullah alihudumu katika Baraza la Kitaifa la Iran toka mwaka 1938 hadi 1960.Vile vile alikuwa ni kiungo cha mawasiliano kati ya Mlinzi na waumini wa Iran hasa katika kipindi cha vita ya pili ya dunia ambapo njia za mawasiliano zilikuwa ngumu sana. Na tena alihusika sana kutafuta vifaa vilivyohusiana na historia ya Imani katika kipindi cha mwanzoni. Ni yeye aliyefanikiwa

kupata jambia alilokuwa anatumia Mulla Husayn, ambalo linatunzwa kwenye jumba la Makumbusho mjini Haifa. Zikrulláh Khadem aliendelea kuhudumia Imani huku akiwa mfanyakazi katika ubalozi wa Iraq hadi mwaka 1952 alipoteuliwa kuwa Mkono wa Hoja na kupewa majukumu maalum yaliyomhitaji kusafiri sana kimataifa. Kwa mfano, kwa kipindi cha miaka 10, kati ya 1953 hadi 1963 alisafiri katika nchi zaidi ya 50 na kutembelea zaidi ya jumuiya za Kibaha'i 1000 katika mabara ya Amerika, Ulaya na Asia. Baada ya kifo cha Mlinzi alishiriki katika vikao vyote na maamuzi yote yaliyofanywa na Mikono wa Hoja. Mwaka 1960 Zikrulláh alihamia Amerika, sababu mojawapo ya kuhamia ikiwa ni kwenda kusaidia kutuliza mawazo hasi yaliyokuwa yameamshwa na uasi wa Mason Remey; jukumu ambalo alilifanya kwa ufanisi mkubwa. Mwaka 1972, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ilimwomba Zikrullah kufanya utafiti na kufanya makusanyo ya maeneo na watu wote waliokuwa muhimu kwa kihistoria ya Imani, kazi ambayo aliifanya na kuikabidhi ikiwa kwenye kabrasha lenye vitabu 134, mnamo mwaka 1977. Zikrulláh Khadem alifariki tarehe 15 Novemba 1986 nyumbani kwake Skokie, Illinois-Marekani baada ya huduma iliyotukuka kwa Imani ya kipindi kirefu.

## 5. Adelbert Mühlschlegel (1897 –1980)



Adelbert Mühlschlegel alizaliwa Juni 1897 mjini Berlin nchini Ujermani. Baba yake alikuwa daktari wa jeshi nchini mwake, hali iliyomvutia naye kusomea kazi ya udaktari. Mwaka 1920 akiwa na umri wa miaka 23 na pia mwanafunzi wa chuo mjini Greifswald alipokea barua kutoka kwa mama yake ikimweleza kuwa alikuwa amepata dini mpya iliyokuwa na lengo la kuunganisha watu wote, na kwamba iliitwa dini ya Bahà'i. Kuanzia hapo Adelbert akaanza kuitafiti, akatafuta vitabu vya Imani na kuvisoma hadi

akaipenda na hatimaye akaamua kuwa Mbahà'i. Hivyo akamwandikia 'Abdu'l-Bahà na mnamo Oktoba 1920 alipata uthibitisho wa kuwa Mbahà'i. Mwaka 1922 alianza kazi ya udaktari ambapo alijitahidi kupatanisha taaluma yake, maisha yake binafsi na Mafundisho ya Imani. Miaka miwili baadaye alimuoa Herma Weidle ambaye naye alikuwa Mbahà'i. Mwaka 1937 dini ya Kibahà'i ilizuiwa na utawala wa Nazi nchini Ujermani na katika kipindi chote cha vita Adelbert alikaa na familia yake mjini Stuttgart akiendelea na kazi yake ya udaktari na kufanya tafsiri ya Maandiko ya Imani kwa lugha ya Kijermani. Baada ya vita 1945, aliendelea na kazi ya kutafsiri vitabu vya Imani na vile vile nyumba yake ikawa kama kituo cha shughuli za Kibahà'i. Baada ya vita Imani iliruhusiwa tena nchini Ujermani na hivyo kuanzia 1946 na miaka mingi iliyofuata Adelbert alihudumu kama mjumbe wa Baraza la kitaifa la Ujermani na Austria hadi mwaka 1958. Mwaka 1936 Adelbert na mkewe Herma walienda hija ambapo walipata fursa ya kukutana na Shoghi Effendi. Mnamo Februari, 1952 Adelbert aliteuliwa na Mlinzi kuwa Mkono wa Hoja. Mwaka 1957 kilipotokea kifo cha Mlinzi, mkewe Amatul-Bahà alimuomba Adelbert akiwa daktari na Mkono wa Hoja kuuandaa mwili wa Mlinzi kwa ajili ya maziko. Alitekeleza jukumu hili la kipekee kwa umakini na moyo ya ibada kama ilivyostahili. Alisema kuwa tukio hilo lenye tajiriba ya kiroho lilimgusa sana na kumpa nguvu ya kuhudumia Imani bila kuchoka kwa muda wa maisha yake yote yaliyokuwa yamebaki. Baadaye aliandika "niliona huu ulikuwa ni upendeleo mkubwa kwangu kwani mikono yangu haikustahili kuosha mwili adhimu kiasi hicho na nikasali na kusema kimoyo moyo kuwa kwa muda mfupi uliobaki wa maisha yangu nitatembea katika njia yake ya huduma kwa hoja ya Mungu bila kusita." Katika mkutano maalum wa faragha wa Mikono wote uliofuatia kifo cha Mlinzi, Dkt. Adelbert Muhlschlegel alichaguliwa na Mikono wenzake kuwa mjumbe wa asasi ya Waangalizi na aliitumikia asasi hiyo hadi mwisho wake 1963. Katika kipindi hicho alitembelea nchi nyingi za Ulaya na kusaidia uundwaji wa Mabaraza ya Kitaifa kutoka kuwa 3 mwaka 1953 hadi 16 mwaka 1963. Mwaka 1964 mke wake Herma alifariki baada ya kuugua kwa muda mrefu. Baadaye mwaka huo huo alihamia Vienna Austria kwenda kuimarisha jamii ya huko na baadaye akamuoa Ursula Kohle. Baadaye 1970 alihamia Switzerland kuendelea na huduma kwa Imani. Kwa mwito wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, mwaka 1969 alitembelea bara la Asia, safari iliyompeleka hadi Iràn, India, Bangladesh na Nepal na baadaye Afrika na Amerika kusini kati ya 1972 na 1975. Mwaka 1977 yeye na mkewe walihamia Athens, Ugiriki kuendelea na kazi ya ufundishaji, na mwaka huo huo Baraza la kwanza la

Kitaifa la Ugiriki likachaguliwa. Julai 29, 1980 Mkono wa Hoja Dkt. Adelbert Muhlschlegel alifariki dunia akiwa mjini Athens, Ugiriki.

**6. Siegfried Schopflocher (1877 - 1953)**



Siegfried Schopflocher (Fred) alizaliwa Septemba,1877 huko Bavaria nchini Ujermani. Alilelewa katika dini ya Kiyahudi lakini alipokuwa kijana akaanza kuwa na imani ya wale waaminio kuwa hatuwezi kujua habari za Mungu (Agnostic) na hii ilimfanya aanze kutafiti juu ya mambo ya kiroho. Alijiunga na kampuni ya kaka zake iliyokuwa inajishughuliza na madini ya "bronze na aluminium" akawa mtu wa mauzo. Mwaka 1906 alihamia Montreal nchini Canada na kuanzisha kampuni iliyojishughulisha na madini hayo hayo na akaiita 'Canadian Bronze Powder'. Kwa juhudi zake kampuni yake ilipanuka na kuwa ya kimataifa na kumfanya awe na mafanikio makubwa kibiashara kwa kuwa ndiye alikuwa na hataza ya bidhaa za madini hayo. Mwaka 1918 alifunga ndoa na Florence Evaline 'Lorol' lakini hawakubahatika kupata watoto kwenye ndoa yao. Miaka michache baadaye, mke wake alifundishwa Imani akaipenda na akaamua kumshirikisha mumewe. Wote wawili wakaendelea kujifunza na mwaka 1921 wakatangaza kuwa Wabahà'i wakiwa Green Acre, huko Marekani. Mwaka 1922 kwa mara ya kwanza walikwenda hija Nchi Takatifu, na baadaye 1924 na 1925 Siegfried alirudi tena Haifa na kupata fursa ya kukutana na Mlinzi ambaye baada ya hapo wakajenga uhusiano wa karibu. Baada ya kuwa Mbahà'i aliweza kusafiri na kufundisha sehemu nyingi duniani na katika kila bara na huku akiendeleza biashara zake. Vile vile aligharamia safari nyingi za ufundishaji za mkewe pamoja na marafiki wengine. Alichaguliwa na kuhudumia Baraza la Kitaifa la Marekani na Canada kwa miaka 15 kwa vipindi kati ya mwaka 1924 hadi 1947 na baadaye Baraza la Kitaifa la Canada 1948 hadi 1953 mtawalia. Alikuwa ni yeye aliyefanya kazi kubwa kuhakikisha Baraza la Kitaifa la Canada linaanzishwa na kusajiliwa na serikali ya Canada. Moja ya sifa ya kusifika sana ya Schopflocher ilikuwa ni ukarimu wa kutukuka; alitoa michango mikubwa kwa ajili ya maendeleo ya Imani nchini Marekani na Canada

hususan ujenzi wa Hekalu Mama la Bara Amerika, ujenzi wa shule ya Kibahà'i ya Green Acre na ujenzi wa Haziratul-Quds ya kitaifa ya Canada. Katika moja ya barua iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi, mwaka 1936 ilisema ''ilikuwa ni kutokana na usaidizi wa ukarimu wake mkubwa usioshindwa kwamba Hekalu la Wilmette lilijengwa,……jina lake (Schopflocher) litahusishwa na Hekalu hilo milele''. Mwezi Februari, 1952 Siegfried Schopflocher aliteuliwa na Mlinzi kuwa Mkono wa Hoja. Licha ya kuwa tajiri mkubwa lakini alichangamana na kila mtu na katika mazingira yoyote yale na mara zote huduma kwa Imani ndiyo ilikuwa kipaumbele chake. Schopflocher alifariki Julai 1953, miezi miwili baada ya kuhudhuria uzinduzi wa Hekalu Mama la Amerika alilojitolea kwa dhati kuhakikisha linakamilika. Anakumbukwa sana na kila aliyehudumu naye kwa tabia yake ya ukarimu na kuwahi sana kila alipohitajika.

---

### 7. Corinne Knight True (1861 -1961)



Corinne Knight True alizaliwa Novemba 1861 Louisville, Kentucky Marekani, katika familia ya kidini. Miezi michache baada ya kumaliza shule mwaka 1882 aliolewa na kijana jirani yao aliyeitwa Moses True. Corinne na mumewe walizaa haraka haraka na kuwa na jumla ya watoto wanane, lakini walipoteza watoto wanne katika kipindi kifupi. Hali hiyo iliwafanya watafakari sana na hivyo wakaanza kujishirikisha na mambo ya dini. Ni katika harakati hizo ndipo Corinne alialikwa kwenye mkutano wa Kibahà'i na rafiki yake. Alivutiwa na Mafundisho na hatimaye akajiunga na Imani mwaka 1899. Baada ya hapo akaanza kujiimarisha kwa kusoma Maandiko ya Imani na kuanza kushirikiana ujumbe wa Baha'u'llàh na kila mtu aliyekutana naye. Wazo la ujenzi wa Hekalu Mama la Amerika lilipoanza Corinne mwanzoni hakuliunga mkono lakini baada ya kuandikiwa waraka na 'Abdu'l-Bahà juu ya suala hilo mara moja akaanza kuliunga mkono kwa nguvu. Alikuwa ni yeye

aliyetafuta na kupata kiwanja cha kujenga hekalu hilo kando kando mwa ziwa Michigan, Wilmette mnamo mwaka 1908. Vile vile alipoenda Akkà alipata fursa ya kukutana na 'Abdu'l-Bahà na ndipo akapewa maelekezo ya kina juu ya ujenzi wa Nyumba ya Ibada ya Marekani. Akiwa katibu wa kamati ya usaidizi ya ujenzi, aliandika barua nyingi na kuzunguka maeneo mengi kuhamasisha Wabahà'i kushiriki juhudi za ujenzi wa Nyumba ya Ibada hadi akaitwa jina la utani la 'Mother of the Temple" (Mama wa Hekalu). Mwaka 1909 alichaguliwa kuwa mjumbe wa kamati ya kusimamia ujenzi wa Hekalu (Bahà'i Temple Unity) na akawa katibu wa fedha wa kamati hiyo. Mwaka huo huo mumewe Moses True alifariki na mwaka 1912 mwanaye wa kiume pia alifariki. Lakini matukio yote haya makubwa hayakukatisha juhudi za Corinne katika huduma yake. Wakati wa ziara ya 'Abdu'l-Bahà huko Marekani kabla ya kwenda kuweka jiwe la msingi la Nyumba ya Ibada alichukua muda kidogo kumfariji Corrine True kwa vifo vya mume na mtoto wake vilivyokuwa vimemtokea kipindi kifupi kilichokuwa kimepita.Wakati wa miaka ya mwanzo ya uongozi wa Shoghi Effendi, Bahà'i Temple Unity ndiyo ilikuwa ikishughulika na mambo yote ya kiutawala ya Imani. Kwa maelekezo ya Shoghi Effendi ilibadilishwa na kuwa Baraza la Kiroho la Kitaifa la Marekani na Canada mwaka 1922. Hili likawa ndilo Baraza la kwanza la kitaifa duniani na Corinne True akiwa mjumbe. Kati ya mwaka 1920 hadi 1930 Corinne alienda hija mara kadhaa na mara zote alipata fursa ya kukutana na kufanya mazungumzo na Mlinzi na mara ya mwisho alienda 1952 akiwa na umri wa miaka 91. Februari 29, 1952 Corrine True aliteuliwa na Mlinzi kuwa Mkono wa Hoja. Mei 2, 1953 ilikuwa ni furaha kubwa kwa Corinne True wakati yeye pamoja na Mikono wengine kadhaa walipohudhuria uzinduzi wa Nyumba ya Ibada ya Marekani mradi ambao alikuwa ametumia sehemu kubwa ya maisha yake kuhakikisha unakamilika. Baada ya kifo cha ghafla cha Mlinzi mwaka 1957, Corinne True kwa sababu ya afya yake na umri mkubwa hakuweza kuhudhuria mkutano maalum wa Mikono wa Hoja uliounda asasi ya Waangalizi, lakini alitaarifiwa maamuzi yote akayaunga mkono na baadaye alitia saini hati zote za maamuzi kama Mkono wa Hoja. Corinne True alifariki nyumbani kwake Wilmette tarehe 3, Aprili 1961, miezi michache kabla ya kufikisha umri wa miaka moja.

***Kundi la tatu: Walioteuliwa mmoja mmoja kwa nyakati tofauti na Shoghi Effendi***

| Na | Jina La Mkono wa Hoja | Kuzaliwa | Kufariki | Kutangazwa—Mkono wa Hoja |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Amatu'l-Bahà Ruhiyyih Khanum | 1910 | 2000 | 26 March 1952 |
| 2 | Jalal Khazeh | 1897 | 1990 | 06 Desemba 1953 |
| 3 | Paul E. Haney | 1909 | 1982 | 19 March 1954 |
| 4 | 'Ali-Muhammad Varqa | 1911 | 2007 | 15 Novemba 1955 |
| 5 | Agnes B. Alexander | 1875 | 1971 | 27 Machi 1957 |

### 1. Amatu'l-Bahá Rúhíyyih Khánum (1910 – 2000)



Mary Sutherland Maxwell (au Amatu'l-Bahà Ruhiyyih Khanum kama alivyojulikana baadaye) alizaliwa mwaka 1910 mjini New York, Marekani akiwa mtoto pekee wa William Sutherland Maxwell na May Bolles Maxwell. Mwaka mmoja kabla ya kuzaliwa kwake, wazazi wake walienda hija, na wakati wakiwa Akkà 'Abdu'l-Bahà alimuuliza May kama alikuwa anatamani kuzaa mtoto. May alijibu kuwa angependa kupata mtoto, na 'Abdu'l-Bahà akamwambia kuwa atamuombea kwa kile anachokipenda. Waliporudi Marekani akapata ujauzito ambao baadaye alikuja kujifungua mtoto wa kike, waliyempa jina la Mary. Baadaye Mary na wazazi wake walihamia Montreal Canada ambapo ndiyo kulikuwa nyumbani kwa baba yake. Mary alilelewa katika maadili ya Imani ya Kibahà'i kwani wazazi wote walikuwa Wabahà'i madhubuti. Wakati 'Abdu'l-Bahà alipotembelea Canada alikaa nyumbani kwao kina Mary. Wakati huo mwaka 1912 Mary alikuwa mtoto wa miaka

miwili. ‘Abdu’l-Bahà alimsifia mtoto huyo mdogo ingawa muda mwingi alikuwa akimsumbua kwa maswali na michezo yake ya kitoto. Kwa kuwa mama yake alipenda kumpa mtoto wake elimu iliyo na utofauti, hivyo alianzisha shule ya mitaala ya Montessori nyumbani kwake ambayo ilikuwa ni ya kwanza ya aina hiyo nchini Canada. Mary alijifunza na kujua kusoma na kuandika katika umri mdogo. Akiwa kijana tayari alikuwa na uwezo wa kuongea kwa ufasaha Kiingereza na Kifaransa. Alipata kwenda hija Nchi Takatifu mara mbili, ya kwanza akiwa na rafiki yake na ya pili akiwa na rafiki wa wazazi wake wakati huo akiwa na umri wa miaka 16. Ni katika safari hizi za hija ndipo Mary alimuona Shoghi Effendi kwa mara ya kwanza. Baada ya hija hizo, Mary alijihusisha sana na shughuli za vijana katika jumuiya ya Kibahà’i, huduma iliyomfanya atembelee nchi kadhaa za bara la Amerika. Alipofikisha umri wa miaka 21 alichaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la mji wa Montreal, Canada. Baadaye mwaka 1935 alienda kuishi Ujerumani kwa ushauri wa Mlinzi ili akaziimarishe jumuiya za Kibahà’i nchini humo. Huko alijifunza lugha ya Kijerumani na kuzijua mila na tamaduni za Wajerumani. Akiwa nchini Ujerumani, Mary alipata mwaliko wa kwenda hija yeye na mama yake. Walifika Haifa Januari 1937, na siku chache baadaye Shoghi Effendi akamwambia Mary nia ya kumpa heshima ya kuwa mchumba wake. Baada ya makubaliano mwezi Februari, Mary akamtumia baba yake simu ya kumtaka aende Haifa haraka. Na tarehe 25, Machi, 1937 Mary Maxwell akafunga ndoa na Shoghi Effendi, katika tukio lililokuwa rahisi sana bila shamrashamra zozote. Wakati huo Shoghi Effendi akiwa na miaka 40, na Mary Maxwell akiwa na miaka 26. Ni kuanzia hapo ndio Shoghi Effendi akampa jina la "*Amatu'l-Bahá Rúhíyyih Khánum*" (*Amatu'l-Bahá* maana yake ni "Kijakazi wa Utukufu".) Akisimulia juu ya tukio la ndoa yao miaka kadhaa baadaye katika kitabu chake kiitwacho “The Priceless Pearl” Amatu’l –Bahà alisema: ukiondoa siku aliyoniambia kuwa ameamua kunipa heshima ya mimi kuwa mke wake, na siku nyingine kama mbili ambazo tulikutana kwenye bwalo la chakula wakati wa chakula cha jioni, hatukuwahi kukaa kuongea pamoja tukiwa wawili hadi siku ya ndoa. Mpango wenyewe wa ndoa yetu haukujulikana kwa watu wengine isipokuwa sisi wawili, wazazi wangu, wazazi wake, kaka yake na dada zake wawili. Kwa hiyo ilikuwa ni mshangao kwa watumishi na Wabahà’i wa Haifa walipoona tukipanda gari moja kuelekea Bahji tukiwa wawili tu na dereva wake mchana wa tarehe 25 Machi, 1937. Tulipofika Bahji kwenye kaburi la Baha’u’llàh, alinivisha pete, halafu akazoa maua yaliyokuwa yametandazwa kwenye sakafu ya kaburi na kuyafunga kwenye kitambaa, halafu akaghani Waraka wa Kuzuru. Alipomaliza tukaondoka kurudi Haifa moja kwa moja hadi kwenye chumba


cha Jani Kuu Kabisa ambapo ndipo hasa ndoa yetu ilipofungiwa. Ilikuwa ni rahisi mno, hakukuwa na sherehe wala shamrashamra au mapambo wala gauni la harusi. Baada ya hapo nilienda kuongea na wazazi wangu kwenye Nyumba ya Mahujaji iliyokuwa mtaa wa pili, naye (Shoghi Effendi) akaenda kufanya shughuli zake kama kawaida. Baadaye tulikutana kwenye chakula cha jioni ambacho tulishiriki wote pamoja na wazazi. Baada ya hapo wazazi walisaini cheti cha ndoa halafu alimpa mama yangu maua aliyoyaleta kutoka kwenye kaburi la Baha'u'llàh kama zawadi yake na shughuli ikaishia hapo. Jioni hiyo mama yake Shoghi Effendi alituma simu ya kebo kwa Wabahà'i wa ulimwengu kuwajulisha kuwa Mlinzi alikuwa amefunga ndoa na Mary Maxwell siku hiyo. Shoghi Effendi alimtia moyo Amatu'l-Bahà kuanza kujifunza lugha ya Kiajemi na baadaye aliweza kuijua na kuimudu vizuri. Muda mfupi baada ya ndoa, Amatu'l-Bahà akaanza kuwa katibu wa Mlinzi, na kutoka 1941 hadi 1957 Amatu'l-Bahà alikuwa ndiye katibu wa Mlinzi. Mwaka 1951 Mlinzi alimteua Ruhiyyih Khanum kuwa mjumbe wa Halmashauri ya Kibahà'i ya Kimataifa. Na Machi 26, 1952 baada ya kifo cha baba yake (ambaye pia alikuwa Mkono wa Hoja) Ruhiyyih Khanum aliteuliwa na Mlinzi kuwa Mkono wa Hoja. Baada ya kifo cha Mlinzi wakati wapo safarini London, Ruhiyyih alishiriki maziko na baadaye alikuwa ni mmoja wa Mikono walioteuliwa kupekua ofisini na nyumbani kwa Mlinzi kuona kama kuna wasia au hati yoyote inayohusu urithi wake. Katika mkutano maalum wa faragha wa Mikono, Amatu'l-Bahà alichaguliwa kuwa mmoja wa wajumbe wa asasi ya Waangalizi na alihudumia kwa uaminifu mkubwa hadi mwisho 1963 ilipochaguliwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Wakati huo huo Wabahà'i wa ulimwengu waliendelea kumchukulia kama kiungo pekee aliyebaki kati yao na familia ya kiini cha Agano- ('Abdu'l-Bahà).

Baada ya kipindi hicho Amatu'l-Bahà alifanya safari katika nchi nyingi katika mabara yote kwa lengo la kufundisha na kuimarisha jumuiya mbalimbali za Kibahà'i. Baadhi ya safari zake zilikuwa ndefu na za muda mrefu. Kwa mfano, alisafiri kwa miaka minne kwa kilometa zipatazo 58,000 kwa gari akikatiza Afrika, akipita katika nchi 34 baadhi ya hizo akikutana na wakuu wa nchi. Katika safari nyingine alitembelea nchi 30 katika bara la Asia na visiwa vya Pacific, safari iliyomchukua miezi saba. Mwaka 1975 hadi 1976 alisafiri kwa mashua katika mto Amazon wa Brazil na kutembelea safu za milima ya Peru na Bolivia ambapo alikutana na watu wa makabila 36 tofauti tofauti. Katika safari zake hizo alipokelewa na kufanya mazungumzo na viongozi wafuatao: Mfalme Haile Selassie wa Ethiopia, Mfalme Malietoa Tanumafili II wa Samoa, Waziri Mkuu Indira Gandhi wa India, Rais Félix HouphouëtBoigny wa Ivory Coast, Rais Carlos Menem wa Argentina, Waziri

Mkuu Edward Seaga wa Jamaica, na Javier Pérez de Cuellar, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Ruhiyyih Khanum alifariki Januari 19, 2000 huko Haifa na akazikwa mjini Haifa karibu na nyumba ya 'Abdu'l-Bahà. Katika maisha yake Ruhiyyih Khanum aliandika vitabu kadhaa, baadhi yake ni: *1. The Priceless Pearl*, 2. *Twenty-Five Years of the Guardianship*, 3. *Prescription for Living*, na 4. *The Desire of the World*

Vilevile alitengeneza filamu mbili: *The Green Light Expedition* na *The Pilgrimage*; moja ni masimulizi ya safari yake ya ufundishaji kandokando ya mto Amazon na nyingine ni maelezo kwa ufupi ya maeneo matakatifu katika Nchi Takatifu ambayo mahujaji huyatembelea.

## 2. Jalal Khazeh (1897 – 1990)




Jalal Khazeh au Khadim alizaliwa katika familia ya Kibahà'i tarehe 24 Februari, 1897 mjini Tehràn. Baba yake Ghulam-Rida alifariki wakati Jalal akiwa na miaka saba tu, kutokana na mateso mengi aliyokuwa ameyapata kutoka kwa maadui wa Imani. Jalal alisoma shule ya Tarbiyat mjini Tehràn iliyokuwa inaendeshwa na Wabahà'i. Baadaye alienda jeshini kwa mujibu wa sheria za nchi hiyo
kwa wakati huo, ambako huko alipata mafunzo ya kijeshi na pia mafunzo ya uganga wa mifugo aliyoyapata kwenye chuo cha kijeshi, na kutokana na kufanya vizuri kwenye mafunzo akaajiriwa na jeshi. Jalal alifunga ndoa na Jamaliyyih Khanum akiwa na miaka 19, ndoa ambayo ilibarikiwa kupata watoto watano. Hadi alipostaafu jeshi mwaka 1943 alikuwa amefikia cheo cha kanali. Mwaka uliofuata 1944, alichaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Kitaifa la Iràn ambalo alilihudumia kwa miaka mitano mfululizo huku akifanya safari nyingi za ufundishaji kuzunguka miji mbalimbali nchini humo. Mnamo mwaka 1952, alipoenda hija Nchi Takatifu alipata fursa ya kukutana na Shoghi Effendi, ambapo alishauriwa kuendelea kufundisha Imani katika nchi yote ya Iràn. Februari 1953 Jalal alihudhuria mkutano mkubwa wa mjini Kampala kwa maelekezo ya Shoghi Effendi na baadaye

kutembelea Kenya, Ethiopia, Eritrea na Muskat kabla ya kurudi Iràn. Baadaye akiwa nchini Iràn wakati ametoka kwenye safari ya miezi 2 ya ufundishaji, saa kumi za alfajiri ya Desemba, 1953 aliamshwa na marafiki wawili waliomletea habari kuwa alikuwa ameteuliwa kuwa Mkono wa Hoja. Jalal Khazeh aliteuliwa tarehe 7 Desemba, 1953. Khazeh ambaye jina lake 'Khazeh' kwa Kiajemi humaanisha mnyenyekevu, alituma ujumbe kwa Mlinzi kwa unyenyekevu akimuomba amsaidie 'ili mgongo huu dhaifu wa huyu asiye chochote uweze kubeba mzigo huu mzito'; Mlinzi alimjibu mara moja kuwa 'Uwe na hakika kuwa utapata ushindi mkubwa'. Jalal aliteuliwa baada ya kifo cha Mkono wa Hoja Siegfried Schopflocher mwezi Julai mwaka huo. Jalal aliendelea na safari za ufundishaji ndani ya nchi ya Iràn na mwaka 1954 alichaguliwa tena kuwa mjumbe wa Baraza la Kitaifa la Iràn. Kati ya mwezi Juni na Julai mwaka 1954, Jalal pamoja na Ali Akbar Furutan walitembelea eneo la Nur na Takur kwenye nyumba ya Baha'u'llàh na wakawafundisha Imani baadhi ya wana-ukoo wa Baha'u'llàh na baadaye Jalal alienda Shiràz kuimarisha jumuiya ya Wabahà'i na kuilinda dhidi ya vitendo vya wavunja-Agano. Akiwa huko, mwaka 1956 alisaidia kuyahamisha mabaki ya mwili wa mke wa Bàb kutoka Shiràz. Pia alimwakilisha Mlinzi katika konvensheni huko Tokyo, Japan mwaka 1955 na
1957. Vile vile alifanya safari za ufundishaji huko Taiwan, Hong Kong na Macau na kutuma taarifa kwa Mlinzi. Wakati wa kifo cha Mlinzi hakuweza kwenda kuhudhuria maziko huko London lakini aliweza kusafiri pamoja na Furutan kwenda Nchi Takatifu kushiriki mkutano maalum wa Mikono wa Hoja uliounda asasi ya Waangalizi. Baada ya kuchaguliwa kama mjumbe wa Waangalizi alilazimika kuhamia Haifa ambapo aliishi hadi mwaka 1963. Akiwa mmoja wa Waangalizi moja ya majukumu yake yalikuwa kupokea na kuzungumza na mahujaji wa kutoka nchi za mashariki. Mwaka 1958, Jalal alitumwa na Waangalizi kuhudhuria mkutano mkubwa wa Kibahà'i wa Frankfurt, Ujermani. Jalal alihudhuria mkutano wa uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na Mkutano wa Dunia wa Kibahà'i uliofuatia huko London mwaka 1963. Baada ya mkutano huo alitembelea nchi kadhaa za Ulaya kama Switzerland, Luxembourg, Austria, Ubelgiji, Ufaransa, Ujermani, Uholanzi na Uturuki kabla ya kurudi Haifa. Mnamo Septemba, Jalal Khadeh aliondoka Nchi Takatifu baada ya kuomba kwenda kuhudumia bara la Amerika kama Mkono wa Hoja. Kwanza alikwenda kukaa nchini Brazil ambako alishiriki mikutano kadhaa katika nchi za Brazil, Bolivia, Peru, Ecuador, Colombia, Venezuela na Marekani hasa juu ya mipango ya kutekeleza Mpango wa Miaka Tisa. Mwaka 1969 yeye na mkewe walirudi Iràn kuendelea na huduma ya ufundishaji, na kipindi hicho yeye aliombwa mara kadhaa kuiwakilisha Nyumba ya Haki katika uzinduzi wa Mabaraza ya

Kitaifa barani Afrika kama vile Dahomey, Togo, Niger na Ghana. Baadaye miaka ya 1973 na 1974 akikumbuka maneno ya Mlinzi aliyowaambia wao Mikono kuwa “mnapaswa kuhudumia Hoja hadi pumzi ya mwisho ya maisha yenu hapa duniani” alifanya safari ndefu za ufundishaji kwenye nchi za India, Canada, Marekani, Switzerland, Ufaransa na visiwa vya Caribbean. Hatimaye mnamo mwaka 1984 baada ya kusumbuliwa, kukamatwa na kunyanga’anywa mali zake na serikali ya Kiislam ya Iràn alishauriwa kuondoka nchini humo na kwenda kuishi Canada. Kutokana na afya yake kuwa dhaifu kwa miaka iliyofuata alipumzika nyumbani kwake huko Toronto, Canada hadi tarehe 21 Februari, 1990 roho yake ilipoitwa kwenye Ufalme wa Abhà.

### 3. Paul Haney (1909 -1982)



Paul Edmond Haney alizaliwa Agosti 20, 1909 mjini Los Angeles, California nchini Marekani, katika familia ya Kibahà’i.Wazazi wake walikuwa Wabahà’i tangu mwaka 1900. Mama yake akiwa na mimba ya Paul alienda hija mjini Akkà na kupata bahati ya kufika mbele ya ‘Abdu’l-Bahà. Baba yake Paul alifariki wakati ana miaka kumi, hivyo alilelewa na mama tu katika hali ngumu ya kiuchumi. Akiwa kijana alihudhuria shule za kiangazi mara nyingi na huko alikutana na Mary Maxwell na yule aliyekuja kuwa mke wake, Helen Margery katika shule ya Green Acre kwenye mojawapo ya mikutano hiyo. Mwaka 1921 akiwa kijana wa miaka 12 hivi, yeye na mama yake walifanikisha kuandaa mkutano wa kwanza wa umoja kati ya watu weupe na weusi mjini Washington D.C, Marekani. Baada ya kumaliza shule ya kati walihamia mjini Washington D.C ambapo alipata kazi serikalini na wakati huo huo akiendelea na masomo wakati wa usiku. Mwaka 1931 aliteuliwa na Baraza la Kitaifa kuwa mjumbe wa Kamati ya Ufundishaji ya Kitaifa. Alisoma chuo kikuu cha Northwestern ambapo alipata shahada ya uzamivu katika biashara na uchumi, na baada ya kuhitimu aliendelea na kazi serikalini. Mwaka 1942, Paul Haney alifunga ndoa na Helen Margery na baada ya ndoa waliendelea

kuishi mjini Washington D.C, kwa kipindi chote hadi 1958 walipolamizimika kuhamia Haifa. Mwaka 1946 alichaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Kiroho la Kitaifa kwa mara ya kwanza na aliendelea kuchaguliwa kwa mfululizo hadi 1957. Tarehe 19 Machi, 1954 Paul Haney aliteuliwa na Mlinzi kuwa Mkono wa Hoja ya Mungu. Akiwa Mkono wa Hoja alimwakilisha Mlinzi katika konvensheni ya kwanza ya Alaska Aprili, 1957. Baada ya kifo cha Mlinzi Paul Haney alichaguliwa na Mikono wenzake kuwa mmoja wa wajumbe wa asasi ya Waangalizi na hivyo akalazimika kuhamia Haifa. Ilimlazimu kuacha kazi nzuri yenye malipo makubwa huko kwao Marekani ili kwenda kuhudumia Imani huko Makao Makuu kama mmoja wa Waangalizi. Katika kipindi hicho aliwawakilisha Mikono wa Hoja kwenye konvesheni za nchi kadhaa duniani. Baada ya uchaguzi wa Nyumba ya Haki mwaka 1963, alikuwa ni mmoja wa Mikono wa Hoja watano walioombwa na shirika hilo kuu kubaki Makao Makuu ya Imani kama washauri wake. Aliiwakilisha Nyumba ya Haki katika matukio mbalimbali duniani kama alivyotumwa na shirika hilo. Pia akiwa Haifa aliiwakilisha Nyumba ya Haki kwa serikali ya Israel katika masuala mbalimbali ya kidiplomasia. Alishiriki kwenye konvensheni zote nne za kimataifa zilizofanyika katika uhai wake, na mwaka 1968 akawa mwenyekiti wa konvensheni ya kimataifa. Alishiriki kwa kiwango kikubwa katika uanzishwaji wa asasi ya Washauri wa bara mnamo 1968, na ile ya Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa 1973—ambapo yeye alikuwa mmoja wa wajumbe wake wa mwanzoni. Tarehe 3 Desemba, 1982 Paul Haney alifariki gafla mjini Haifa kwa ajali ya gari barabarani.

## 4. Agnes Baldwin Alexander (1875–1971)



Agnes Baldwin Alexander alizaliwa tarehe 21 Julai, 1875 mjini Honolulu katika kisiwa cha Hawaii huko Marekani. Babu zake walikuwa ni wamisionari na watu wa kwanza walioipeleka dini ya kikristo katika kisiwa hicho na familia hizo ziliheshimika sana hapo Hawaii. Historia ilijirudia wakati baadaye mjukuu wao Agnes alipokuwa mtu wa kwanza kuipeleka Imani ya Kibahà'i Hawaii.Wamisionari hao (babu zake) walikuwa ni

mchungaji William Patterson Alexander (babu mzaa baba) na mchungaji Dkt. Dwight Baldwin (babu mzaa mama). Agnes alilelewa na kukulia katika maadili ya dini ya kikristo kulingana na imani na hadhi ya wazazi wake. Baada ya kuhitimu masomo katika chuo kikuu cha Oahu mwaka 1895, alifanya kazi kwa miaka michache, baadaye akaacha kwa sababu ya ugonjwa uliompata wakati huo na baada ya kupona akafungua mkahawa mjini Honolulu. Mwaka 1900 alijiunga na kundi la watu waliokuwa wanakwenda kutalii Ulaya. Akiwa mjini Rome, Italia katika nyumba ya wageni alikutana na mama mmoja kutoka Marekani (Charlotte Dixon) aliyekuwa anatoka hija Nchi Takatifu, ambaye alimweleza habari za ufunuo wa Baha'u'llàh. Baada ya siku tatu katika kile alichokiita maono au njozi akagundua kuwa Yesu alikuwa amekwisharudi kama alivyoahidi na hivyo akaukubali ufunuo huo mpya, akawa Mbahà'i. Alitambulishwa kwa Wabahà'i wengine waliokuwa huko Ulaya wakati huo ambao aliweza kukutana nao mjini Paris. Kati ya hawa, alikuwa ni Bi. May Ellis Bolles (baadaye May Maxwell-mama yake Ruhiyyih Khanum) na mwalimu msomi mashuhuri wa Kibahà'i Mirza Abu'lFadl aliyekuwa ametumwa na 'Abdu'l-Bahà kuziimarisha jumuiya mpya za Ulaya. Mnamo tarehe 26 Desemba, 1901 Agnes akafika Hawaii, sasa akiwa Mbahà'i wa kwanza kufikisha Imani ya Baha'u'llàh kisiwani humo. Alirudi kwao Hawaii akiwa na shauku kubwa na mara moja alianza kufundisha Imani katika kisiwa hicho na baada ya muda akaanza kupata Wabahà'i wa mwanzo hapo Hawaii. Mnamo mwaka 1914 Agnes alipata waraka toka kwa 'Abdu'l-Bahà wa kumtaka aipeleke Imani nchini Japan. Akaanza safari, japo alikwama nchini Uswisi kutokana na vita ya kwanza ya dunia lakini aliweza kuwa mtangulizi. Vile vile ndiye alikuwa mtu wa kwanza kuifikisha Imani nchini Japan mwaka huo huo. Mnamo mwaka 1921 Agnes alikwenda Korea kufundisha Imani kwa mwezi mmoja hivi, na hivyo kuwa mtu wa kwanza kuipeleka Imani nchini humo. Kwa kutambua juhudi yake, 'Abdu'l-Bahà ameandika katika Nyaraka za Mpango Mtakatifu "**Fikiria ninyi Bi. Agnes Alexander, binti wa Ufalme, mpendwa kijakazi wa Ukamilifu Uliobarikiwa, alisafiri peke yake katika visiwa vya Hawaii..........na sasa anapata ushindi wa kiroho huko Japan! Tafakarini jinsi binti huyu alivyothibitishwa katika visiwa vya Hawaii. Alikuwa ni sababu ya mwongozo wa mkusanyiko wa watu.**

**"Kwa wakati huu katika visiwa vya Hawaii, kupitia juhudi za Bi. Alexander roho kadhaa zimefikia ufuko wa bahari ya Imani! Fikirieni, ni furaha ya jinsi gani, ni shangwe ya jinsi gani hii!..........**[10]

Waraka huu uliandikwa miaka miwili baada ya kuwa Agnes amefika Japan. Mwaka 1924 Agnes aliambatana na Martha Root kwenda kufundisha China, ambako walifanikiwa kukutana na aliyekuwa kiongozi wa nchi hiyo Sun Yat Sen na kumpa vitabu viwili vya Kibahà'i, na pia walikutana na watu mashuhuri kadhaa nchini humo. Vile vile alifanya safari za ufundishaji katika nchi zingine kama Ufilipino, Taiwan, Hong Kong na zingine za Ulaya. Kitu kimoja kilichomsaidia Agnes kufikisha ujumbe wa Baha'u'llàh katika nchi hizi za mbali ilikuwa ni ujuzi wake na uanachama wake wa chama cha lugha ya Esperanto. Alitumia lugha hii kufundisha Imani na aliwatumia waesperanto wenzake kuwa wakalimani wake, kila alipokwenda kufundisha. Pia alitafsiri kitabu cha "*Maneno Yaliyofichwa*" kwa lugha ya Esperanto. Mwaka 1937 Agnes Alexander alikaribishwa kwenda hija Nchi Takatifu ambapo alipata fursa ya kuonana na Shoghi Effendi. Baada ya hapo Agnes hakuweza kurudi Japan, kutokana na vita vya pili vya dunia hadi mwaka 1950. Baada ya kufika Japan alihamia kwenye mji wa Kyoto badala ya Tokyo na kuendeleza juhudi za ufundishaji huko. Mnamo Machi 27, 1957 Agnes Alexander aliteuliwa na Shoghi Effendi kuwa Mkono wa Hoja ya Mungu wa bara la Asia. Kwa ujumla, Agnes alipokea barua zipatazo 100 kutoka kwa Mlinzi katika kipindi chote cha uongozi wa Mlinzi. Alikuwa thabiti katika Agano tangu kipindi cha 'Abdu'l-Bahà hadi kipindi cha uongozi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Agnes alishuhudia uundwaji wa Baraza la Kiroho la Kitaifa la Mashariki-Kaskazini ya Asia lililokuwa na makao makuu yake mjini Tokyo mwaka 1957, ambalo yeye alikuwa mjumbe kuanzia 1957 hadi 1963. Katika kipindi hicho alisafiri mara kadhaa kwenda Nchi Takatifu kuhudhuria mikutano ya Mikono wa Hoja. Alishiriki kikamilifu katika mkutano maalum wa Mikono wa Hoja baada ya kifo cha Mlinzi. Pia, mwaka 1963 alishuhudia uundwaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na alihudhuria mkutano mkuu wa London uliofuatia tukio hilo la kihistoria. Mwaka uliofuata, 1964 Agnes kwa furaha kubwa alihudhuria uundwaji wa Baraza la kwanza la Kitaifa la Hawaii akiwa mwakilishi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, mjini Honolulu. Mwaka 1965 alianguka na kuvunjika nyonga, hali iliyomlazimisha alazwe hospitali mjini Tokyo kwa miaka miwili. Licha ya maumivu aliyokuwa nayo akiwa hospitalini yeye mara zote alisema 'hakuna kinachotokea bila sababu, bila shaka kulikuwa na busara ya Mungu kunifungia sehemu moja kwa miaka miwili'. Baadaye mwaka 1967 Agnes aliondoka Japan kurudi nyumbani kwao Hawaii ambapo aliendelea kuishi kwa miaka minne zaidi huku afya yake ikizidi kutetereka. Januari 1, 1971 Agnes Baldwin Alexander alifariki dunia nyumbani kwao Honolulu akiwa na miaka 95. Alizikwa kando

ya makaburi ya babu zake—wamisionari wa kwanza wenzake waliopeleka dini katika visiwa vya Hawaii.

## 5. Alí-Muḥammad Varqá (1912 -2007)



Ali Muhammad Varqa alizaliwa Januari, 1912 mjini Tehràn, Iràn. Alizaliwa katika familia maarufu katika Imani ya Valliyu'llàh Varqa ambaye alikuwa Mkono wa Hoja na mdhamini wa Huq´uqu´lláh. 'Abdu'l-Bahà ndiye alimpa jina la Ali Mohammad Varqa, jina la babu yake ambaye pia alikuwa Mkono wa Hoja na mfia dini. Ali Varqa mwanzoni alisomea mjini Tehràn kabla ya kwenda nchini Ufaransa kwa shahada za juu. Alifunga ndoa mwaka 1935, ndoa ambayo ilijaliwa kupata watoto watatu. Kwenye miaka ya 1940 alipata udhamini wa kwenda Ulaya kusomea shahada ya juu. Alisoma na kuhitimu shahada ya uzamivu katika mitambo ya maji na umwagiliaji kutoka chuo kikuu cha Sorbonne nchini Ufaransa mwaka 1950. Baada ya masomo alirejea nchini Iràn na kuwa mhadhiri katika vyuo vikuu vya Tabriz na Tehràn na wakati huo huo aliendelea na shughuli za huduma katika Imani. Katika kipindi hicho vile vile alianza kumsaidia baba yake jukumu la kushughulika na makusanyo ya Huq´uqu´lláh. Mwaka 1955, tarehe 14 Novemba, siku 2 baada ya kifo cha baba yake, Dkt. Ali Mohammad Varqa aliteuliwa na Shoghi Effendi kuwa Mkono wa Hoja na pia mdhamini wa Huq´uqu´lláh kama alivyokuwa baba yake. Ali Mohammad Varqa alikuwa ni Mkono wa Hoja pekee ambaye japokuwa aliteuliwa na Shoghi Effendi lakini hakubahatika kuonana naye uso kwa uso. Aprili 1956 Varqa alimwakilisha Mlinzi kwenye konvensheni huko Buenos Aires, Argentina iliyojumuisha nchi tano za ukanda huo. Mwezi Novemba 1957, Ali Varqa alishiriki mkutano maalum wa faragha uliounda asasi ya Waangalizi kufuatia kifo cha Mlinzi. Baada ya hapo alirejea Iràn kuendelea na huduma za Mpango wa Miaka 10, kama Mkono wa Hoja wa bara la Asia na pia kama mjumbe wa Baraza la Kitaifa la Iràn. Mwaka 1962 Ali Varqa alitumwa na asasi ya Waangalizi kwenda Ufaransa kuimarisha jumuiya ya nchi hiyo kufuatia mkanganyiko uliosababishwa na wavunja-Agano nchini humo. Na mwaka 1963, akiwa mjumbe wa Baraza la Iràn, alishiriki kama mjumbe kwenye konvensheni ya kwanza ya kimataifa

kuchagua Nyumba ya Haki ya Ulimwengu licha ya yeye pia kuwa Mkono wa Hoja. Baada ya kuundwa kwa Nyumba ya Haki Ali Varqa aliendelea kuhudumu kama Mkono wa Hoja wa bara la Asia akiishi nchini Iràn. Mwaka 1970 alishiriki mkutano wa Bodi ya Washauri wa Bara la Asia uliofanyika nchini Iràn, na pia mwaka 1971 alikwenda Afrika kuiwakilisha Nyumba ya Haki katika kuunda Baraza la Kitaifa la Congo na Gabon. Septemba 1976 aliambatana na mfalme Malietoa Tanumafili II wa Samoa kutembelea kaburi la Shoghi Effendi mjini London. Kufuatia mapinduzi ya mwaka 1979 nchini Iràn, Ali Mohammad Varqa alilazimika kuhamia nchini Canada ambako aliendelea kutoa huduma kwa Imani kama Mkono wa Hoja. Mei 1983, Nyumba ya Haki ilimuomba Ali Varqa kwenda kuhudumia Makao Makuu ya Ulimwengu kufuatia kifo cha Mkono wa Hoja Paul Haney. Mwaka 1989 akiwa mdhamini wa Huq´uqu´lláh alianzisha juhudi za kuunda Ofisi ya Huq´uqu´lláh Makao Makuu na baadaye 1992 alianzisha Bodi za kikanda na kitaifa za Wadhamini wa Huq´uqu´lláh. Na mwaka 2005 Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ilianzisha Bodi ya Kimataifa ya Udhamini wa Huq´uqu´lláh ili kuzisaidia bodi za kikanda na za kitaifa. Septemba 22, 2007 Dkt. Ali Mohammad Varqa alifariki mjini Haifa akiwa Mkono wa Hoja wa mwisho kuishi.

## Simulizi ya utabiri wa ‘Abdu’l-Bahà juu ya Ali Mohammad Varqa

*Wakati wa ziara ya ‘Abdu’l-Bahà huko Marekani 1912, Valliyu’llàh Varqa alikuwa ni mmoja wa watu waliochaguliwa kwenda Naye kwenye ziara hiyo ya kihistoria. Siku moja wakiwa huko Amerika, wakati wanapumzika baada ya chakula cha mchana, Valliyu’llàh alifungua barua iliyokuwa na picha ndani iliyokuwa imetumwa kutoka kwa kaka yake Azizullàh. ‘Abdu’lBahà alimuona Valliyu’làh akijawa na furaha wakati alipokuwa anasoma barua hiyo na akamuuliza kitu gani kilikuwa kinamfurahisha sana kwenye hiyo barua? Valliyu’llàh akajibu “Bwana mpendwa, nimepata barua kutoka Tehràn kwa kaka yangu ambayo imetumwa pamoja na picha ya mtoto wangu mchanga aliyezaliwa” ‘Abdu’l-Bahà akasema “lete hiyo picha niione”. Alipopewa picha hiyo ‘Abdu’l-Bahà alichukua kalamu Yake na akaandika kwenye mkono mmoja wa mtoto huyo kwenye picha ‘Yed’ (Mkono) na katika mkono mwingine akaandika ‘Mo’ayyed’ (amethibitishwa) na pia akasema huyu mtoto jina lake ni ‘Ali Mohammad Varqa’ kama babu yake. ( 11 )*



*Picha ya Dkt Ali Mohamad Varqa akiwa bado mtoto*

### ***Kundi la mwisho: Walioteuliwa tarehe 2 Oktoba, 1957***

| **Na** | **Jina La Mkono wa Hoja** | **Kuzaliwa** | **Kufariki** |
|---|---|---|---|
| 1 | Hasan Balyuzi | 1908 | 1980 |
| 2 | Abu'l-Qasim Faizi | 1906 | 1980 |
| 3 | H. Collis Featherstone | 1913 | 1990 |
| 4 | John Ferraby | 1914 | 1973 |
| 5 | Rahmatu'llàh Muhajir | 1923 | 1979 |
| 6 | Enoch Olinga | 1926 | 1979 |
| 7 | John Robarts | 1901 | 1991 |
| 8 | William Sears | 1911 | 1992 |

## 1. Hasan M. Balyuzi (1908 – 1980)



Hasan Muvaqqar Balyuzi alizaliwa Septemba 7, 1908, huko Shiràz, Iràn. Alikuwa ni Afnan yaani mzaliwa wa ukoo wa familia ya Mtukufu Bàb. Kwa kweli, babu yake na babu yake Shoghi Effendi walikuwa watoto wa baba mmoja aliyeitwa Haji Mirza Abdu'l-Qasim ambaye pia alikuwa ni kaka yake Khadijih-Bagum, mke wa Bàb. Baba yake Hasan Balyuzi alikuwa ofisa mwenye cheo kikubwa katika serikali ya Iràn. Wakati wa vita vya kwanza vya dunia familia yao ilikimbilia India, na wakiwa huko Hasan alifundishwa lugha za Kiajemi, Kiarabu na Kiingereza. Baada ya vita familia ilirejea Iràn, naye Hasan akapata nafasi ya kwenda kusoma Beirut kwa maandalizi ya kwenda chuo kikuu. Lakini kabla ya kuondoka akawa amealikwa na Shoghi Effendi apitie Haifa kumtembelea wakati akiwa njiani kuelekea Beirut. Kwa siku moja aliyokaa na Shoghi Effendi pale Haifa ilitosha kubadilisha fikra zake na Imani yake ya awali na akaikubali Imani ya Kibahà'i kama dini ya Mungu. Hivyo tangu wakati huo hakujiona tena kama Muislamu bali kama Mbahà'i. Wakati huo, mwaka 1925 alikuwa ni kijana wa miaka 17. Huko Beirut alisoma hadi shahada ya kwanza na baadaye mwaka 1932 alienda Uingereza kusoma shahada ya pili, wakati huo huo akijishughulisha na shughuli nyingi za Imani. Mwaka 1933 akachaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Kitaifa la Uingereza, nafasi ambayo aliendelea kuchaguliwa kwa miaka mingi mfululizo hadi 1958. Katika kipindi hicho pia alihudumu kama mjumbe wa Baraza la mji wa London. Moja kati ya juhudi zake binafsi ilikuwa ni kuandika makala na machapisho mbalimbali kuhusu Baha'u'llàh na Mafundisho Yake kwa Kiingereza. Mwaka 1942 hadi 1958 alifanya kazi katika Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) kitengo cha Kiajemi akitayarisha vipindi kuhusu historia ya Iràn. Vile vile, kwa maelekezo ya Mlinzi, kuanzia mwaka 1936 Hasan Balyuzi alikuwa akifanya majukumu ya kiutawala katika ofisi ya Umoja wa Mataifa (League of Nations), Geneva huku akiendelea kuwa mjumbe wa Baraza la Uingereza. Mnamo Oktoba 1957 aliteuliwa na Mlinzi kuwa Mkono wa Hoja. Muda mfupi baadaye, baada ya kifo cha Mlinzi, Hasan Balyuzi alijumuika kwenye mkutano maalum wa Mikono wa Hoja na kuchaguliwa kuwa mjumbe wa asasi ya Waangalizi,

nafasi aliyoitumikia hadi kwenye kilele chake kwa uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Baada ya hapo afya yake ilianza kuzorota na hivyo akabaki anajishughulisha zaidi na kazi za uandishi wa vitabu kuhusu Imani. Hasan Balyuzi alifariki tarehe 12 Februari, 1980 mjini London. Aliandika vitabu vingi na akaacha maelekezo kuwa ianzishwe maktaba ya utafiti wa historia ya Imani na iitwe Afnan Library. Ndoto yake hiyo ilitimizwa mwaka 1985 ilipoanzishwa Afnan Library Trust; maktaba ambayo ipo Sandy, Cambridge - Uingereza na ina vitabu na machapisho zaidi ya 10,000.

---

Vitabu vya Kiingereza alivyoandika Hasan Balyuzi ni: *1."Bahá'u'lláh," London: Bahà'i Publishing Trust, 1938, 2."A Guide to the Administrative Order," London: Bahà'i Publishing Trust, 1941, 3. "The World made Flesh." London: George Ronald, 1963, 4."Edward Granville Browne and the Bahà'i Faith," London: George Ronald, 1970, 5."Abdu'lBahà: The Center of the Covenant of Baha'u'llàh," London: George Ronald, 1971, 6."The Báb: The Herald of the Day of Days," Oxford: George Ronald, 1973, 7."Muhammad and the Course of Islam," Oxford: George Ronald, 1976, 8."Bahá'u'lláh: The King of Glory," Oxford: George Ronald, 1980, 9."Khadijih Bagum: The Wife of the Báb," Oxford: George Ronald, 1981, 10 "Eminent Bahá'ís in Iràn During the Time of Bahá'u'lláh," Oxford: George Ronald, 1985.*

---

## 2. Abu'l-Qásim Faizí (1909- 1980)



Abu'l Qásim Faizí alizaliwa katika familia ya kiislam mjini Qum, Iràn mnamo mwaka 1909. Baadaye familia yake ilihamia Tehràn akiwa na miaka nane na akaanza shule ya Tarbiyat ambapo ndipo alipoanza kusikia Imani ya Kibahà'i kwa mara ya kwanza. Akiwa shuleni hapo alialikwa kwenye madarasa ya Kibahà'i, akavutiwa na mafundisho, akaanza kuyafuatilia na baada ya muda akaikubali Imani. Ingawa mama yake alibaki kuwa muislam lakini

alimuunga mkono mtoto wake katika kuifuata kikamilifu Imani. Baadaye, akiwa na miaka 19 alikwenda kusoma American University, Beirut mwaka 1927. Akiwa huko alipata bahati ya kwenda Haifa na kukutana na Shoghi Effendi wakati wa likizo zake akiambatana na Hasan Balyuzi. Baada ya kuhitimu shahada ya fasihi ya Lugha ya Kiingereza alirudi Iran kwa lengo la kufundisha katika shule za Kibahà'i za Tarbiyat, lakini haikuwezekana kwani mwaka huo huo 1934, shule zote za Kibahà'i nchini Iràn zilifungwa; naye akaenda kufundisha watoto wa Kibahà'i wa vijijini kwa muda wa miaka mitano. Baadaye alianza kuwaandaa vijana wa Kibahà'i nchini humo kwa ajili ya kwenda kuwa watangulizi. Mwaka 1939 alimuoa Gloria Ala'i, na baada ya hapo walienda Baghdád kusaidia kazi kwenye Baraza la Kitaifa la Iraq kwa mwaka mmoja kabla ya kwenda kuwa mtangulizi huko Uarabuni ambako alikaa kwa miaka 15 kama mtangulizi. Alipofika Bahrain alipata kazi ya kufundisha shule moja ya sekondari lakini baadaye alifukuzwa kazi baada ya kugundulika kuwa alikuwa Mbahà'i, na pia kwa sababu alikuwa akiwafundisha watu Imani. Hii ni kwa sababu wakati huo Imani ilikuwa imepigwa marufuku nchini humo. Baada ya kuachishwa kazi aliendesha maisha yake kwa kufanya kazi ya uandishi ambapo aliandika vitabu vya hadithi na tamthilia pamoja na kutafsiri vitabu.

Qasim Faizi alikuwa mjuzi sana wa lugha za Kiarabu, Kiajemi na Kiingereza, na kutokana na ujuzi huo aliweza kutafsiri vitabu vya *The Priceless Pearl* na *Portals to Freedom* kutoka Kingereza kwenda Kiajemi na *Delight of Hearts* na *The Life of Mirza Haydar-Ali* kutoka Kiajemi kwenda Kiingereza. Baadhi ya vitabu vya Imani alivyoandika ni pamoja na: *Flame of Fire, The Prince of Martyrs, From Adrianople to `Akká, Stories from the Delight of Hearts, Mírzá Haydar-`Alí, na Meditations on the Eve of November 4th Explanations of the Symbol of the Greatest Name.*

Mwaka 1954, zilipoanzishwa Bodi za usaidizi za mabara, Qasim Faizi aliteuliwa kuwa mjumbe wa Bodi ya usaidizi ya Asia. Oktoba 1957, Qasim Faizi aliteuliwa pamoja na wenzake 7 kuwa Mikkono wa Hoja na Shoghi Effendi majuma manne tu kabla hajafariki. Qasim Faizi alikuwa ni mmoja wa Mikono waliohudhuria maziko ya Mlinzi Shoghi Effendi na ni yeye aliyechaguliwa kughani sala ya maziko katika tukio hilo muhimu. Baadaye alikuwa ni mmoja wa wale Mikono waliochaguliwa kuhudumu kwenye asasi ya Waangalizi na kuanzia hapo akalazimika kuishi Nchi Takatifu na

kuhudumu katika asasi hiyo hadi ilipochaguliwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Mwaka 1960 wakati wa uasi wa Mason Remey, Qasim Faizi alitumwa kwenda kukutana na Baraza la Kitaifa la Ufaransa ambalo baadhi ya wajumbe wake walikuwa wamemuunga mkono Remey. Na baada ya kukutana naye na baadhi ya wajumbe kushindwa kujitenga na madai ya Remey, Baraza hilo lilivunjwa na wajumbe 5 walioshindwa kutii mamlaka halali wakawa wavunja Agano. Mara baada ya Nyumba ya Haki kuchaguliwa Qasim alisafiri mara kadhaa, safari zote akiwakilisha Nyumba ya Haki sehemu mbalimbali hasa katika uundwaji wa Mabaraza ya Kitaifa, kwani wakati huo yeye pamoja na Ruhiyyih Khanum na Paul Haney waliombwa na Nyumba ya Haki kukaa Makao Makuu ili kusaidia kazi za kiutawala za Imani. Kati ya mwaka 1963 na 1968 alitembelea nchi kadhaa za Ulaya, Amerika na Asia. Mwaka 1970 aliiwakilisha Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwenye uzinduzi wa kuundwa kwa Mabaraza ya Kitaifa ya Afrika ya Kati na Zaire (sasa Congo –DRC). Wakati wa kuundwa kwa asasi ya Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa mwaka 1973, yeye pamoja na Mikono wengine waliteuliwa kuwa wajumbe na waliombwa kukaa Makao Makuu ili kufanya kazi za kiutawala za kituo hicho. Kuanzia mwaka 1969 hadi 1979, Qasim Faizi alifanya safari nyingi za ufundishaji na kuhudhuria mikutano katika nchi mbali mbali katika mabara yote. Alikuwa mzungumzaji mahiri katika mikutano mikubwa ya kimataifa. Abu'l Qasim Faizi ambaye mlinzi alimuita 'mshindi wa kiroho wa Uarabuni' alifariki Novemba, 1980 mjini Haifa.

### 3. Harold Collis Featherstone (1913 –1990)



Harold Collis Featherstone alizaliwa Mei 13, 1913 huko Quorn-Adelaide, Australia. Awali alisomea uhasibu na baadaye uhandisi na baada ya masomo akafanya kazi katika kampuni kubwa ya uhandisi hadi mwaka 1936. Mwanzoni alikuwa na ndoto ya kuwa mchungaji katika kanisa la Anglikana, lakini alizuiwa na ugumu wa kanuni za kidini na wingi wa makanisa wakati huo. Alifunga ndoa mwaka 1938 na baadaye mwaka 1944 yeye na mkewe

wakawa Wabahà'i wakiwa miongoni mwa watu wa kwanza kwenye jumuiya ya Adelaide. Alijifunza Imani kwa juhudi kubwa na kila alipokosa jibu juu ya fundisho lolote alimwandikia Mlinzi ili kupata jibu sahihi, na kwa hiyo alimiliki akiba ya barua kama 20 hivi alizoandikiwa na Mlinzi. Mwaka 1946 alisaidia kuanzishwa kwa Baraza la Mahali la Woodville. Harold Featherstone alichaguliwa na kuhudumu katika Baraza la Kitaifa la Australia kuanzia mwaka 1949 hadi 1962. Alikuwa ni mtu imara na makini ambaye alilisaidia Baraza katika masuala ya mali na uanzishwaji na usajili wa Mabaraza ya Mahali. Yeye na mkewe walipoenda hija Haifa, Collis alihakikisha anamuuliza Mlinzi maswali mengi kadiri alivyoweza akiwa na nia ya kuelewa hasa kile ambacho jamii yao ya Australia ilitakiwa kumakinikia katika kipindi hicho. Alirudi nyumbani akiwa na nguvu na shauku kubwa na kusaidia sana mipango ya ufundishaji ya eneo hilo la Asia ya kusini licha ya kuwa na majukumu ya kuhudumia familia yake. Mwaka 1954 aliteuliwa na Mkono wa Hoja Clara Dunn kuwa Mshauri Msaidizi kwa eneo la Australia, New Zealand na eneo lote la Pacific. Pia Collis alishiriki katika majukumu ya upatikanaji wa Haziratu'l-Quds za Aukland na Suva pamoja na Bahà'i senta kadhaa za mahali. Vile vile akiwa mshauri msaidizi alibeba jukumu la kuitambulisha Imani ya Kibahà'i kwa viongozi wa serikali na viongozi wa dini. Oktoba 1957, Collis Featherstone aliteuliwa na Shoghi Effendi kuwa Mkono wa Hoja. Alishiriki mkutano maalum wa Mikono wa Hoja uliounda asasi ya Waangalizi na baada ya hapo aliendelea kusimamia mpango wa Mpambano wa Miaka Kumi katika bara lake hadi hitimisho lake 1963. Baada ya mwaka huo Collis alisafiri sehemu mbalimbali barani mwake akiiwakilisha Nyumba ya Haki ya Ulimwengu katika mikutano mikubwa, uzinduzi wa Mabaraza ya Kitaifa na mawasiliano na viongozi wa serikali. Mwaka 1968 zilipoundwa na kuteuliwa Bodi za Washauri wa bara, Collis sasa alikuwa huru kusafiri nje ya bara la Australasia, hivyo aliweza kusafiri sehemu mbalimbali duniani kwa shughuli za Imani. Alitembelea Afrika, India, Asia mashariki na visiwa vya Pacific. Septemba 29, 1990, Collis Featherstone alifariki akiwa katika safari ya kuwatembelea Wabahà'i mjini Kathmandu, Nepal. Siku chache baadaye, mkewe na watoto wake watano walifika huko na kushiriki maziko ya mpendwa wao.

**4. John Graham Ferraby (1914- 1973)**



John Ferraby alizaliwa Januari, 1914 Southsea nchini Uingereza na alikulia na kusomea nchini humo. Mwaka 1936 baada ya kifo cha baba yake alihamia mjini London ambako pia aliendelea na masomo. Ilikuwa ni mwaka 1941 ndipo alisikia juu ya Imani ya Kibahà'i kwa mara ya kwanza kutoka kwa mtu ambaye naye hakuwa Mbahà'i bali alikuwa amekutana na Wabahà'i, na habari hizo zilimvutia. Baadaye alienda maktaba kupata habari zaidi ambapo alikutana na kitabu cha "Baha'u'llàh na Wakati Mpya" ambacho kilimvutia zaidi. Mwanzoni alipata shida namna ya kuwapata Wabahà'i ili ajifunze zaidi lakini baadaye aliwapata na baada ya kuwatembelea mara kadhaa kwa majuma mawili aliamua kujiunga na Imani. Mmoja wa Wabahà'i wa mwanzoni nchini humo aliyemsaidia kujifunza zaidi Imani alikuwa ni Hassan Balyuzi. Mwaka uliofuata, 1942 alichaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la mji wa London na mjumbe wa Baraza la Kitaifa. Mwaka 1943 alifunga ndoa na mjumbe mwenzake wa Baraza la Kitaifa, Dorothy Cansdale. Mwaka 1946 alihudumu kama katibu wa Baraza la Kitaifa huku akiendelea kufanya kazi kwenye kampuni ya British Export Trade Organization.

Kuanzia mwaka 1950 akahudumu kama katibu wa Baraza la Kitaifa wa muda wote, na mwaka 1954 akahamia kwenye Haziratu'l-Quds ya kitaifa ambako aliendelea kuishi hadi 1959 alipotakiwa kwenda kuishi Haifa akiwa mjumbe wa asasi ya Waangalizi. Katika kipindi cha 1953 hadi 1956 alihusika sana katika kamati iliyoundwa kuhakikisha nchi nyingi za Kiafrika zinafunguliwa kwa Imani. Mwaka 1953, alishiriki katika mkutano mkubwa wa uzinduzi wa Mpambano wa Miaka 10 kwa bara la Afrika mjini Kampala, Uganda. Mwaka 1955 alienda hija Nchi Takatifu ambako alipata fursa ya kukutana na Shoghi Effendi, na kutokana na ushauri wake, aliporudi Uingereza akaandika kitabu kiitwacho 'All Things Made New' (*Vitu Vyote Vimefanywa Vipya*), ambacho kimewasaidia watu wengi kuitambua Imani hasa nchini Uingereza, Marekani na India. Mnamo Oktoba 2, 1957, John Ferraby aliteuliwa na Shoghi Effendi kuwa Mkono wa Hoja. Majuma machache baada ya kuteuliwa

wakati wa kifo cha Mlinzi, John Ferraby akiwa Mkono mwenyeji mjini London, alisaidia sana katika kufanikisha maandalizi na maziko ya Mpendwa Mlinzi. Baadaye alishiriki katika mkutano maalum wa Mikono wa Hoja uliounda asasi ya Waangalizi. Mwaka 1959 alichaguliwa na Mikono wenzake kuwa mjumbe wa asasi ya Waangalizi, asasi aliyoihudumia hadi mwisho mwaka 1963 ilipochaguliwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Baada ya hapo alirudi kuishi Cambridge, Uingereza na familia yake na kuendelea kutekeleza majukumu aliyopangiwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Alifanya safari nyingi za ufundishaji na kuhudhuria mikutano mbalimbali barani Ulaya katika kipindi hicho hadi afya yake ilipoanza kuwa dhaifu. Tarehe 5, Septemba 1973, John Ferraby alifariki nyumbani kwake akiwa usingizini mjini Cambridge. Baadhi ya kazi zake za uandishi ni hizi: *1. All Things Made New:* Bahá'í Publishing Trust, London 1957, *2. The Passing of Shoghi Effendi*. Bahá'í Publishing Trust, London 1958, *3. Bahá'í Teachings on Economics*. Bahá'í Publishing Trust, London 1954, *na 4. Progressive Revelation*.

## 5. Raḥmatu'lláh Muhájir (1923 -1979)



Rahmatu'llàh Muhajir alizaliwa Aprili, 1923 huko Abdu'l-Azizi, Kashan-Iràn katika familia ya Kibahà'i. Alikulia katika familia ambayo nyumbani kwao ilikuwa ni kitovu cha shughuli za Kibahà'i katika eneo lao. Rahmatu'llàh alikuwa mwalimu mahiri wa Imani tangu akiwa mdogo, mara nyingi akiwaalika wanafunzi wenzake na watoto majirani kuja kupata mafundisho ya Imani nyumbani kwao. Akiwa na miaka tisa, familia yao ililazimika kuhamia Tehràn kutokana na kuongezeka kwa chuki za viongozi wa dini ya kiislam katika eneo lao. Baada ya kuhitimu masomo ya sekondari ya juu alikwenda kuwa mtangulizi kwa miaka miwili katika jimbo la Adhirbayjan. Baadaye alijiunga na masomo ya udaktari katika chuo kikuu mjini Tehràn. Mara kadhaa alikatisha masomo yake kwenda kushiriki utekelezaji wa malengo ya mpango wa miezi 45 wa Baraza la Kitaifa la Iràn. Wakati huo huo alikuwa akihudumu kama katibu wa Kamati ya Utangulizi ya Kitaifa. Alipokuwa mwaka wa mwisho wa masomo, 1951 alifunga ndoa na Iràn

Furutan (binti yake Ali Akbar Furutan). Alihitimu masomo ya udaktari kwa ushindi wa juu wa daraja la kwanza mwaka 1952. Baada ya kuhitimu mafunzo akaanza kazi ya udaktari mjini Isfahàn, na baadaye mwaka huo huo yeye na mkewe walikwenda hija Nchi Takatifu ambapo alipata fursa ya kufanya mazungumzo na Mlinzi hasa kuhusiana na jinsi ya kueneza Imani katika nchi za Indonesia na visiwa vya Pacific. Baadaye yeye na mkewe walifanya uamuzi wa kwenda utangulizi kwenye bara la Asia na hivyo wakauza mali zao zote na kwenda kuwa watangulizi. Mwezi Februari 1954, Rahmat na mkewe waliwasili katika kisiwa cha Muara Sibert (mojawapo ya visiwa kadhaa vya Indonesia) na Mlinzi akawatangaza kuwa Mashujaa wa Baha'u'llàh. Dkt. Muhajir aliajiriwa na Wizara ya Afya ya Indonesia na kupangiwa kwenda kisiwa cha Mentawai. Wenyeji wa kisiwa hiki hawakuwa na huduma zozote za afya na walikuwa wakisumbuliwa sana na magonjwa ya kuambukiza, hivyo Dkt. Muhajir akaanzisha mfumo wa kielimu wa kupambana na hali hiyo ya magonjwa. Hivyo Dkt. Muhajir akawa anawafundisha Imani na wakati huo huo akiwapa huduma za kiafya. Akaendesha kampeni kubwa ya mpango wa afya kwa umma na akafanikiwa kupunguza magonjwa kwa kiasi kikubwa. Alikuwa akitembea kwa miguu akipita kwenye misitu yenye maji na tope zito ili kupeleka huduma za afya pamoja na mafundisho ya Baha'u'llàh kwa kuzunguka visiwani humo na mara nyingi akilala kwenye vilago kwenye vijumba vya wenyeji. Mawasiliano pekee yalikuwa ni kwa barua ambazo zingebebwa na boti ya serikali iliyokwenda huko mara moja kwa miezi miwili. Furaha yake kubwa ilikuwa ni pale wenyeji wengi walipoanza kuipokea Imani na wakati huo huo magonjwa yakipungua kwa kiasi kikubwa. Maisha ya wenyeji yalibadilika sana kutokana na mafundisho ya kiroho na ya kiafya yaliyoendeshwa na Dkt. Muhajir. Katika kipindi cha miaka minne aliyokaa katika kisiwa cha Mentawai zaidi ya Wabahà'i elfu nne, mabaraza ya mahali 33, shule 12 za Kibahà'i zilianzishwa na mali wakfu ya Imani ilipatikana. Vile vile, alikwenda mji mkuu wa Djakarta kusaidia upatikanaji wa Haziratu'l-Quds ya kitaifa. Mwezi Oktoba, 1957 Dkt. Rahmatu'llàh Muhajir alikuwa ni miongoni mwa wale katika kundi la mwisho kuteuliwa kuwa Mikono wa Hoja. Baada ya kifo cha Mlinzi, Dkt. Muhajir alihudhuria mkutano maalum wa Mikono huko Haifa uliounda asasi ya Waangalizi, mnamo 1957. Baada ya hapo, kama Mkono wa Hoja alilazimika kuondoka nchini Indonesia, jambo ambalo lilikuwa gumu sana kwake. Katika kipindi cha kati ya 1958 hadi 1979 alifanya safari nyingi za ufundishaji akizungukia takriban nchi zote za dunia. Alitembelea Ufilipino, India, nchi kadhaa za Afrika, Ulaya na Amerika. Nchini India alisaidia ununuzi wa majengo ya Kibahà'i, uanzishwaji wa shule

kadhaa za Wabahà'i na mashirika ya uchapishaji wa vitabu vya Kibahà'i. Vile vile alikutana na kufanya mazungumzo na mfalme Malietoa Tanumafili wa Samoa. Mnamo Desemba 29, 1979 akiwa nchini Ecuador akishiriki mkutano wa ufundishaji, ghafla alipata ugonjwa wa moyo na kufariki mjini Quito, Ecuador. Sifa ya kipekee aliyokuwa nayo Dkt. Muhajir ni kwamba alikuwa mwalimu mahiri wa Imani, ambaye alipenda muda wote ashiriki mafundisho ya Baha'u'llàh na roho yoyote aliyokutana nayo.


### 6. Enoch Olinga (1926 – 1979)



Enoch Olinga alizaliwa Februari 1926 katika eneo la Teso, mashariki mwa Uganda. Wazazi wake walikuwa wa kabila la Iteso na Wakristo wa madhehebu ya Anglikana. Alisoma shule ya msingi katika kijiji cha Tilling na baadaye sekondari katika mji wa Mbale. Akiwa sekondari alisoma masomo ya lugha na uchumi, na akapata ujuzi wa kutumia lugha katika kutafsiri lugha kadhaa. Mwaka 1941 alijiunga na jeshi la Waingereza la Afrika Mashariki na kupata mafunzo nchini Kenya. Baadaye alipelekwa vitani katika nchi za Burma, Bangladesh na India. Baada ya vita vya pili vya dunia mwaka 1946, alirejea Uganda na kuajiriwa na Idara ya uhusiano na usitawi wa jamii wilayani Teso. Mwaka huo huo alioa na pia aliandika vitabu 2 katika lugha ya Teso. Mnamo mwaka 1950 alihamia mjini Kampala akiwa na familia yake. Baadaye alifukuzwa kazi serikalini kutokana na tabia ya ulevi uliokithiri. Mwaka mmoja baadaye akiwa Kampala alikutana na mafundisho ya Imani ya Kibahà'i yaliyokuwa yakiendeshwa na Ali Nakhjavani na Musa Banani. Baada ya muda mfupi, Februari 1952 akafanya uamuzi wa kuwa Mbahà'i na kubadilisha maisha yake ikiwemo kuacha kunywa pombe. Alikuwa Mbahà'i wa kwanza kutoka kabila lake na Mbahà'i wa tatu nchini Uganda. Alianza kuhudhuria mafundisho ya Imani kila mara kwenye familia za Ali Nakhjavani na Musa Banani, na baada ya muda alikwenda kufundisha Imani maeneo ya nyumbani kwao na baada ya muda mfupi, mwezi Oktoba 1952 baba yake na mke wake nao wakawa Wabahà'i. Miezi 18 baada ya kuikubali Imani mwaka 1953 aliitikia mwito wa Shoghi Effendi na akawa Mganda wa

kwanza kwenda kuwa mtangulizi katika nchi ya Cameroon, na hivyo akatunukiwa hadhi ya kuwa 'Shujaa wa Baha'u'llàh' wa nchi hiyo. Baadaye Wabahà'i wa nchini Cameroon waliongezeka na miongoni mwao wakaenda kufungua nchi za jirani kama vile Togo na Ghana nao wakatunukiwa kuwa Mashujaa wa Baha'u'llàh. Kwa kipindi cha miaka mitatu makoloni 29 kati ya 33 yakafunguliwa kwa Imani. Kutokana na juhudi zake hizo Enoch Olinga akapewa na Mlinzi jina la "Abu'l-Futuh", (Baba wa ushindi). Baadaye mwaka 1956, Olinga alichaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la kwanza la Kitaifa la Afrika Kaskazini–Magharibi. Mwezi Februari 1957, Enoch Olinga alipata fursa ya kwenda Nchi Takatifu ambapo alipata siku 10 za kukaa na Mlinzi na fursa hiyo iliweka kumbukumbu ya kudumu katika maisha ya Olinga. Enock Olinga akawa Mbahà'i wa kwanza mwafrika mweusi kufanya hija katika Nchi Takatifu. Baada ya safari hiyo alirejea Afrika Magharibi na kuendeleza juhudi za ufundishaji. Oktoba 2, mwaka huo huo aliteuliwa na Shoghi Effendi kuwa Mkono wa Hoja akiwa Mkono pekee mwafrika na kijana wa miaka 31. Majuma machache baadaye alihudhuria mkutano maalum wa Mikono wote wa Hoja uliofanyika Nchi Takatifu baada ya kifo cha Mlinzi. Mara baada ya uchaguzi wa Nyumba ya Haki, pamoja na Mikono wenzake walihudhuria mkutano wa Dunia wa Wabahà'i uliofanyika mjini London ambapo aliteuliwa kuwa mwenyekiti wa mkutano huo. Baada ya 1963, Enoch Olinga kwa maelekezo ya Nyumba ya Haki alifanya safari nyingi za ufundishaji katika nchi kadhaa zikiwemo nchi za Amerika ya Kusini, Amerika Kaskazini, Mexico, Japan, India na kwingineko. Wakati wa utawala wa Iddi Amin kuanzia mwaka 1971, nchi ya Uganda haikuwa na utulivu na usalama wa raia, na mnamo mwaka 1977 Imani ya Kibahá'í ilizuiliwa nchini Uganda. Kutokana na hali hiyo Enoch Olinga alirudi Uganda katika kipindi hicho hicho kigumu ili kuilinda jumuiya ya Kibahà'i nchini humo. Jioni ya tarehe 16 Septemba, 1979, baada ya vita na kuondolewa kwa utawala wa Iddi Amin kwa vita na wakati bado nchi haijawa na utulivu, Enoch Olinga, mkewe na watoto wake watatu kati ya watano waliuawa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana waliovamia nyumbani kwake. Hakika lilikuwa tukio la huzuni kwa jumuiiya ya Kibahà'i kote duniani. Tarehe 24, Septemba 1979 Enoch Olinga alizikwa katika viunga vya Hekalu mama la Afrika mjini Kampala kando ya kaburi la mmoja wa walimu wake wa Imani na Mkono wa Hoja Musa Banani.


## 7. John Robarts (1901 – 1991)



John Aldham Robarts alizaliwa Novemba 1901 mjini Waterloo-Ontario, Canada. John Robarts alikulia na kusoma katika eneo la Thunder Bay ambako baba yake alikuwa akifanya kazi. Baada ya masomo yake katika chuo cha Ridley College alianza kazi katika shirika la reli. Baadaye aliacha kazi na akaungana na David Graham kuanzisha kampuni yao iliyoitwa Overhead Door Company of Canada. Mwaka 1928 John Robarts alifunga ndoa na Audrey FitzGerald na baadaye walijaliwa kupata watoto wanne. Mwaka 1934 hali mbaya ya uchumi iliwalazimisha kuuza kampuni yao na yeye akajiunga na kampuni ya bima. Ni katika kipindi hicho ndipo alipoanza kusikia juu ya Imani ya Kibahà'i na kuifuatilia, kujifunza na mnamo 1937, John Robarts na mkewe wakajiunga na Imani. Tangu wakati huo, John Robarts alitoa maisha yake kwa Imani ambayo aliihudumia bila kuchoka. Juhudi zake za mwanzoni zilisaidia sana kuanzishwa kwa jumuiya ya Kibahà'i ya Hamilton na Ottawa ambazo ziliweza kuunda Mabaraza yao ya Mahali mnamo mwaka 1940 na 1948 mtawalia. Kuanzia mwaka 1953, John na mkewe walifanya safari nyingi za ufundishaji wa Imani. Mwaka 1953, baada ya Mlinzi kutoa wito wa kufungua Bachuanaland (Botswana) kwa Imani, John Robarts na mkewe Audrey waliinuka mara moja na kuelekea Bachuanaland barani Afrika. Walifanikiwa kuifungua nchi hiyo kwa Imani na hivyo Mlinzi akawapa hadhi ya kuwa Mashujaa wa Baha'u'llàh wa nchi hiyo. Alipoinuka kwenda kufungua nchi ya Bachuanaland, John ilimbidi kuacha kazi yake nzuri nchini Canada na kwenda kwenye nchi ambayo wakati huo haikuwa na barabara na ambayo ilikuwa nusu jangwa. Vile vile alisafiri na kufundisha Imani Southern Rhodesia (Zimbabwe), Morocco, Liberia na Cameroon; na baadaye Japan, Korea, Taiwan, Hong Kong, Phillipines, Hawaii, Jamaica, Iceland Ireland, Australia, New Zealand, Fiji, Papua New Guinea, Visiwa vya Solomon na Samoa Magharibi. Mwaka 1957, John Robarts alikuwa ni miongoni mwa kundi la mwisho la Mikono wa Hoja lililoteuliwa na Mlinzi. Baada ya kifo cha Mlinzi, John alishiriki mikutano ya Mikono, na kuendelea kutekeleza

mpango wa Mpambano wa Miaka Kumi katika bara la Afrika. Baada ya kuundwa kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, John Robarts aliendelea kutoa huduma kwa Imani bila kuchoka licha ya kusumbuliwa na magonjwa na kifua na asthma kwa kipindi kirefu cha maisha yake. Mwaka 1984, John Robarts alirejea Canada na kuweka makazi yake Rawdon,
Quebec. Mnamo tarehe 18 Juni, 1991 John Robarts alifariki huko RawdonQuebec, Canada baada ya kuugua kwa miezi michache. Sifa ya kipekee kwa John Robarts ilikuwa ni imani yake kubwa kwa nguvu ya sala. Sala alizozipenda zaidi na kuongea juu yake kila mara ni “Mwondoa shida” na “Sala Ndefu ya Faradhi”, alizoea kusema kuwa ukiona kuna migogoro mingi katika jumuiya ya Kibahà’i, hiyo ilikuwa ni dalili kwamba marafiki wengi katika eneo hilo walikuwa hawasemi sala za faradhi. Aliamini kuwa sala hizo zina nguvu kubwa sana ya kutatua matatizo mengi ya watu.

## 8. William Sears (1911 -1992)



William Bernard Sears alizaliwa Machi 28, 1911 huko Aitkin-Minnesota, Marekani katika familia ya kikatoliki. Akiwa mtoto mdogo, aliota ndoto ambapo alimuona mzee mmoja mwenye sura ya utulivu inayong’aa na mwenye ndevu nyeupe. Mzee huyo alimuita na kumwambia, ‘uwe mvuvi kama Petro, uwe mvuvi wa watu, nakusubiri, nitafute, uwe kama Petro’ na alipoamka ndoto hiyo iliendelea kuwa akilini mwake muda wote. Alipomhadithia babu yake ndoto hiyo, babu yake akamwambia; ‘’utatakiwa kumtafuta huyo mtu mwenye sura ya kung’aa, la sivyo ndoto yako itapotea bure”. Tangu wakati huo William akawa na shauku ya kujua mambo ya dini na Mungu, na hivyo pia akaanza kujifunza biblia. Je, ndoto hiyo ilikuwa na maana gani kwa William Sears? Utajua baadaye! Baada ya William kumaliza shule ya sekondari alikwenda chuo kikuu cha Wisconsin na akiwa bado anaendelea na masomo alifunga ndoa na Kathleen. Baada ya kumaliza masomo, akawa mwandishi wa habari, mtangazaji wa redio na runinga huko Wisconsin. Mke wake wa kwanza Kathleen Sears alifariki baada ya kujifungua mtoto wao wa pili mnamo mwaka 1934, akimwachia watoto wawili wa kiume, William na Michael. Akiwa anaendelea na kazi za

utangazaji alikutana na mama mmoja Marguerite Reimer ambaye alikuja kubadilisha mwelekeo wa maisha yake. Alianza kumueleza habari za Imani ya Kibahà'i na kuhusu Baha'u'llàh na 'Abdu'l-Bahà. Mwanzoni William Sears hakuvutiwa na Imani ya Kibahà'i, lakini baada ya Margurite kumsimulia safari za 'Abdu'l-Bahà huko Marekani na kumpa kitabu kilichoandikwa kutokana na mazungumzo Yake huko Marekani, alivutiwa sana na 'Abdu'lBahà. Baada ya mkewe kumuonesha picha, mara moja aligundua kuwa yule mzee mwenye ndevu nyeupe na uso wenye kung'aa aliyemuona kwenye ndoto alikuwa 'Abdu'l-Bahà. Ndipo akaja kugundua kuwa wakati ule anaota ile ndoto akiwa mtoto kule Minnesota, kumbe ndo wakati huo huo 'Abdu'lBahà alikuwa akifanya ziara katika mji huo na alifanya mkutano umbali mfupi tu kutoka nyumbani kwao. Hiyo ilikuwa ni tarehe 20 Septemba, 1912 wakati 'Abdu'l-Bahà alipotoa hotuba huko Minneapolis-Minnesota. Hivyo William akafanya uamuzi kuwa lazima ajifunze zaidi kuhusu mafundisho hayo yaliyoletwa na 'Abdu'l-Bahà huko Marekani. Kitabu alichokisoma kwanza kilichohusiana na tukio lile ni kile kiitwacho "Utangazaji wa Amani ya Ulimwengu". Moja ya vitu vilivyomvutia ni lile fundisho lake la kuwa kila mtu lazima atafute ukweli mwenyewe na siyo kufuata wengine kwa mkumbo na upofu bila kufanya uchunguzi. Akiwa anaendelea kujifunza Imani, William Sears alifunga ndoa na Marguerite mnamo mwaka 1940 na mwaka huo huo William Sears alijiunga rasmi na Imani ya Kibahà'i. Alianzisha kipindi maarufu cha runinga kilichoitwa "*In The Park*" kilichokuwa kinaelezea mafundisho ya Kibahà'i. William aliendelea na kazi yake ya utangazaji katika vituo mbalimbali vya redio na runinga nchini Marekani hadi mwaka 1953 ambapo yeye na mkewe waliamua kwenda Afrika kama watangulizi wakiitikia wito wa Shoghi Effendi. Walihamia Afrika Kusini kama watangulizi, wakapata makazi nje kidogo ya mji wa Johanessburg, wakapata shamba dogo wakaanza kuishi kwa kulima matunda na kufuga tausi huku wakifundisha Imani. Aprili 1954, William alienda hija Nchi Takatifu ambapo aliweza kuonana na Shoghi Effendi, na kati ya ushauri aliopewa na Mlinzi ambao kamwe hakuusahau, William alieleza baadaye "nyie mnaokwenda Afrika lazima muelewe kuwa mnakwenda huko kufundisha Imani kwa Waafrika wenyeji na siyo kwa Wazungu au wengine waliohamia huko…" alisema Mlinzi. Baada ya kurudi Afrika Kusini alipata kazi katika Shirika la Utangazaji la Afrika Kusini, hivyo akaendelea kufanya kazi na huku akifundisha Imani. Alisaidia kuundwa kwa Baraza la kwanza la mji wa Johanessburg ambalo waliamua liwe na wenyeji weusi peke yao, hii ni kutokana na sheria za serikali ya kibaguzi ya wakati huo ambazo hazikuruhusu shirika lolote kuwa na mchanganyiko wa weupe

na weusi. Mwaka 1954 William aliteuliwa na Mkono wa Hoja Musa Banani kuwa mshauri msaidizi. Nafasi hiyo ilimpa fursa ya kutembelea nchi nyingi za Afrika katika majukumu ya kueneza Imani. Mnamo Oktoba 1957, William Sears aliteuliwa na Mlinzi kuwa Mkono wa Hoja. Baada ya kifo cha Mlinzi, William Sears alihudhuria mkutano maalum wa Mikono wa Hoja na kushiriki katika uanzishwaji wa asasi ya Waangalizi mnamo Novemba 1957. Mwezi Julai, 1960 kilipotokea kifo cha Mkono wa Hoja Horace Holley ambaye alikuwa mmoja wa Waangalizi, William Sears alichaguliwa na Mikono wenzake kujaza nafasi ya Horace Holley. Hivyo tangu wakati huo William Sears aliihudumia asasi hiyo hadi mwisho, 1963 ilipochaguliwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Wakati wa uongozi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, William Sears alitembelea nchi mbalimbali akitoa mafundisho katika mikutano mingi mikubwa na midogo. Kwa miaka ya 1967 hadi 1978 alikuwa nje ya Marekani; akitembelea nchi kadhaa za Afrika, Uingereza, Italia na pia Israel. Mwaka 1970 aliombwa kutembelea maeneo yote matakatifu ya nchini Iràn; kwa msaada wa Baraza la Iràn, alitembelea nyumbani kwa Bàb na Baha'u'llàh, ulipofanyikia Mkutano wa Badasht, Tabriz, gereza la Siyah-Chal, ngome ya Makku na mahali pa mapambano ya sheikh Tarbasi, na kutokana na ziara hiyo aliweza kuandika kitabu" *The Prisoner and The Kings*". Kuanzia mwaka 1971 William aliendelea kusafiri, kuhudhuria na kuhutubia mikutano mbalimbali ya jumuiya za Kibahà'i hasa nchini Marekani katika majimbo kadhaa. Kufuatia mateso ya Wabahà'i yaliyofuatia mapinduzi ya kiislam nchini Iràn aliandika kitabu (*A Cry from the Heart: The Bahá'ís in Iràn)* ambacho kilitumika kama ushahidi kwenye bunge la Marekani lilipokuwa linajadili juu ya mateso ya Wabahà'i wa Iràn. Kuanzia mwaka 1986 afya yake ilianza kutetereka sana ingawa aliweza kwenda kuhudhuria uzinduzi wa Mashriqu'l-Adhkar ya India na kutoa hotuba. Tarehe 25 Machi, 1992 William Sears alifariki dunia mjini Tucson-Marekani. William Sears alitumia taaluma yake ya uandishi vizuri katika kufundisha Imani. Alitengeneza kazi nyingi za kiuandishi kufikisha ujumbe wa Baha'u'llàh kwa watu kadiri ilivyowezekana. Baadhi ya vitabu maarufu alivyoandika ni pamoja na: *Release the Sun, Thief in the Night, All Flags Flying, The Prisoner and The Kings, God Loves Laughter, A Cry from the Heart: The Bahá'ís in Iràn, na The Wine of Astonishment*.

# 6

## HUDUMA YA MIKONO WA HOJA BAADA YA SHOGHI EFFENDI



*Mikono wa Hoja baada ya msiba wa Shoghi Effendi wakiwa nje ya Jumba la Baha'u'llàh, Bahji*

### Kuundwa kwa Asasi ya Waangalizi

Tarehe 4 Novemba, 1957 ilikuwa ni siku ya mshtuko mkubwa kwa Wabahá'i wote ulimwenguni. Ilikuwa siku ambayo Mikono wa Hoja pamoja na Wabahá'i wote kwa jumla walijikuta yatima kwani kiongozi na mpendwa wao Mlinzi wa Imani ya Mungu hakuwa tena nao hapa duniani. Mara tu kifo cha ghafla cha Mlinzi kilipotokea, taarifa ilitumwa kwa Mikono wa Hoja wote ikiwahimiza Mikono wote wasio na kikwazo kwenda kushiriki mazishi ya kiongozi wao mpendwa Shoghi Effendi mjini London. Kwa wakati huo kulikuwa na Mikono wa Hoja 27; wanawake 5 na wanaume 22 wakiwa wanatoka katika mabara yote na wachache wakikaa Makao makuu ya Imani

mjini Haifa. Baadhi wakiwa ni majuma manne tu tangu walipoteuliwa naye kuwa Mikono wa Hoja. Vituo vyao vya huduma vilikuwa kama ifuatavyo:

| **Na** | **Jina la Mkono wa Hoja** | **Kituo** | | **Na** | **Jina la Mkono wa Hoja** | **Kituo** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Amelia Collins | Haifa | | 15 | 'Ali-Akbar Furután | Irán |
| 2 | Tarazu'lláh Samandari | Irán | | 16 | Abu'l-Qasim Faizi | Bahrain |
| 3 | Mason Remey | Haifa | | 17 | Hasan Balyuzi | Uingereza |
| 4 | Agnes Alexander | Japan | | 18 | Paul Haney | Marekani |
| 5 | Musa Banani | Uganda | | 19 | Amatu'l-Bahá Ruhiyyih Khanum | Haifa |
| 6 | Horace Holley | Marekani | | 20 | 'Ali-Muhammad Varqa | Irán |
| 7 | Shu'a'u'lláh 'Ala'i | Irán | | 21 | William Sears | Afrika Kusini |
| 8 | Leroy Ioas | Haifa | | 22 | Corrine True | Marekani |
| 9 | Ugo Giachery | Italia | | 23 | Clara Dunn | Australia |
| 10 | Jalal Khazeh | Irán | | 24 | Collis Featherstone | Australia |
| 11 | Adelbert Muhlschlegel | Ujerumani | | 25 | John Ferraby | Uingereza |
| 12 | Hermann Grossmann | Ujerumani | | 26 | Rahmatu'lláh Muhajir | Indonesia |
| 13 | John Robarts | Botswana | | 27 | Enoch Olinga | Cameroon |
| 14 | Dhikru'lláh Khadem | Irán | | | | |

Wakati wa maziko ya Mlinzi huko London jumla ya Mikono wa Hoja 18 waliweza kuhudhuria na baada ya maziko walikutana na kukubaliana kuwa hakukuwa na muda wa kupoteza, hivyo wakaitisha mkutano wa Mikono wote katika Makao Makuu ya Imani mjini Haifa kuanzia tarahe 18 Novemba 1957. Ilipofika tarehe 18 Novemba, Mikono wa Hoja 26 walikuwa wamefika Nchi Taifa kwa ajili ya mkutano huo maalum wa faragha ili kushauriana juu ya hatima na mwelekeo mpya wa Hoja. Mmoja wao, Clara Dunn, ingawa

alisafiri kutoka Australia hadi Haifa hakuweza kushiriki kwenye mkutano huo kwa sababu ya kuumwa, lakini alikubaliana na maamuzi ya Mikono wenzake na kutia saini nyaraka zote za maamuzi. Afya na umri mkubwa wa Corrine True (miaka 96) havikumruhusu kusafiri kutoka Marekani hadi Haifa, lakini kila uamuzi alijulishwa na alikubaliana na Mikono wenzake, kwa hiyo maamuzi yote yaliafikiwa na Mikono wote 27. Hivyo, waliokuwa kwenye chumba cha mkutano na kushauriana walikuwa ni Mikono 25 kati ya 27. Kazi yao haikuwa rahisi hata kidogo kwani ilihitaji kiwango cha juu cha utiifu, unyenyekevu, ujasiri, kujitenga, ustahimilivu na dhabihu. Mmoja wao baadaye alieleza kwamba "tulikuwa kama mgonjwa mahututi ambaye kupona kwake kulitegemea yeye mwenyewe kujiamsha kitandani na kutembea hatua chache". Licha ya huzuni na mshtuko mkubwa waliokuwa nao, pia kulikuwa na hali zingine anuwai zilizoufanya mkutano huo usiwe wa kawaida. Litakuwa jambo jema kama angalau kwa kiasi tutajua hali za uanuwai wao zilivyokuwa. Kwa umri kulikuwa na tofauti kubwa baina yao; mkubwa kabisa (Corrine True) alikuwa mzee wa miaka 96 na mdogo zaidi (Enock Olinga) alikuwa kijana wa miaka 31. Kwa tajiriba na huduma katika Imani, mmoja wao alikuwa muumini tangu wakati wa Baha'u'lláh na alipata baraka ya kufika mbele Yake (Tarazu'lláh Samandari), wengine kadhaa walikuwa waumini tangu wakati wa Abdu'l-Bahá na wengine hadi hapo walikuwa na miaka michache tu tangu wamekuwa Wabahá'i wakati wanateuliwa na Mlinzi. Vile vile kwa tajiriba yao kama Mikono wa Hoja, wengine walikuwa na tajiriba ya takribani miaka sita lakini nane kati yao walikuwa wameteuliwa kuwa Mikono wa Hoja majuma manne tu kabla ya kifo cha Mlinzi na walikuwa hata hawajakutana naye tangu wateuliwe. Kwa elimu pia kulikuwa na utofauti, kulikuwa na watatu wenye majina yenye kutumia neno "daktari", wengine kadhaa walikuwa na elimu ya shahada na stashahada na mmoja ambaye hakuwa na elimu yoyote ya shuleni, alijua tu kuandika herufi za jina lake, ingawa alikuwa na ujuzi mkubwa juu ya mafundisho ya Imani. Wanawake walikuwa 5 na wanaume walikuwa 22. Kulikuwa na Mikono 2 tu kati ya wale wa kutoka Uajemi walioweza kuongea lugha mbili; Kiingereza na Kiajemi, na ni mmoja tu kutoka Magharibi (Amatu'l-Bahá Ruhiyyih Khanum) aliyekuwa na ujuzi wa kiasi wa lugha ya Kiajemi. Hivyo, ufanisi wa mkutano ulitegemea sana lugha hizi mbili kwa tafsiri ya kutoka moja hadi nyingine ili kila mmoja aweze kuelewa maoni ya mwingine. Zaidi ya hayo, wengi kati yao walikuwa hata hawajawahi kuonana.

Kwa hiyo, wote hawa na tofauti zote hizo waliunganishwa na kitu kimoja kikubwa-upendo wao kwa Baha'u'lláh na utii kwa Agano Lake.

Walikubaliana kuwa mkutano ufanyike kwenye nyumba ya Baha'u'lláh kule Bahji jirani na Kaburi Lake na wakaweka ratiba kuwa kila asubuhi wangekwenda kusali kwenye kaburi takatifu la Baha'u'lláh kabla ya kuanza mkutano, na pia kila jioni wakati wa kufunga mkutano wangekwenda kwenye chumba Chake cha kupaa kusema sala ya kufunga. Utaratibu huu uliwekwa ili kutengeneza mazingira ya hali ya kiroho na kuomba uongozi Wake wakati wote wa vikao. Walikubaliana kuweka utaratibu wa mkutano ambao ulijumuisha yafuatayo: 1) kila mjumbe awe huru kujieleza kwa lugha anayoijua vizuri 2) mjumbe anapojieleza asikatishwe, ajieleze kwa uhuru hadi mwisho 3) anayetafsiri atafsiri kila kitu ambacho mzungumzaji amesema na siyo ufupisho 4) aliyechaguliwa kuwa mwandishi ndiye pekee aandike taarifa, karatasi zingine zozote zichomwe kabla ya kufunga kikao 5) hakutakuwa na mwenyekiti wa kudumu 6) maamuzi yote muhimu lazima yatiwe sahihi ya makubaliano na kila Mkono. Baada ya utaratibu kuwekwa hatua ya kwanza ilikuwa ni kuchagua Mikono tisa kati yao kwenda kufungua na kupekua kila sehemu, ofisini na nyumbani kwa Mlinzi ili kuhakikisha kama kulikuwa na wasia au waraka wowote ambao aliuandaa kuhusu urithi wake. Ikumbukwe kuwa baada ya taarifa za kifo chake, sehemu zote (vyumba, kabati na kadhalika) zenye mali na nyaraka zake zilifungwa na Mikono waliokuwa Haifa wakati huo kwa ajili ya usalama. Jukumu hili lilitekelezwa kwa umakini na kundi hilo lililochaguliwa na baada ya kujiridhisha walitoa taarifa ambayo iliwasilishwa kwenye mkutano maalum wa faragha wa Mikono wote; taarifa yao kwa kifupi ilisema hivi "Sehemu zote zimefunguliwa na kupekuliwa na imehakikishwa kwamba Shoghi Effendi hakuacha Wasia na Agano". Baada ya taarifa hii kuwasilishwa na kukubaliwa, sasa waligeukia Wasia na Agano la Abdu'l-Bahá ili kuona kama lingewapa mwongozo. Moja ya vifungu walivyoangazia, kutafakari na kushauriana kwa kina katika Wasia na Agano ni hiki:

"….**Mikono wa Hoja ya Mungu lazima wachague kutoka miongoni mwao Mikono tisa ambao watashughulika wakati wote na huduma muhimu katika kazi za Mlinzi wa Hoja ya Mungu. Uchaguzi wa Mikono hawa tisa lazima ufanyike kwa makubaliano ya wote au kwa wingi wa sauti kutoka kundi la Mikono wa Hoja ya**

**Mungu, na hawa kwa makubaliano ya wote au kwa kura za wengi lazima waridhie kwa chaguo la yule ambaye Mlinzi wa Hoja ya Mungu amemchagua kama mrithi wake. Ridhaa hii lazima itolewe kwa njia ambamo sauti za kukubali na zile za kukataa haziwezi kutofautishwa"(8)**

Baada ya kusoma na kutafakari kwa kina Wasia na Agano la Abdu'l-Bahá, kwa pamoja walikubaliana kuwa hakukuwa na asasi nyingine ya kusimamia Imani zaidi ya Asasi ya Mikono wa Hoja, na hivyo majukumu ya ulinzi na maendeleo ya Hoja yalikuwa mabegani mwao kwa wakati huo. Wakatambua kuwa kulikuwa na mambo kadhaa mbele yao yaliyohitaji kupatiwa ufumbuzi kwa haraka na mkutano huo. Baadhi yake ni kama haya:

i) Shoghi Effendi alikuwa kiini cha Imani na sasa hayupo, nini kifanyike?

ii) Mali zote za Imani zilikuwa chini ya mamlaka ya Shoghi Effendi na sasa hayupo, hivyo mali zinahitaji kupewa ulinzi imara wa umiliki.

iii) Fedha zinahitajika kwa ajili ya kugharamia shughuli za Imani, sasa hakuna mwenye mamlaka ya kisheria kuidhinisha fedha kutoka benki, nini kifanyike?

iv) Mpango wa miaka 10 unaendelea, nani wa kuusimamia ili hatimaye Nyumba ya Haki ya Ulimwengu iweze kuundwa?

v) Jumuiya ya Kibahá'i duniani inahitaji uongozi na ulinzi, ni wajibu wa nani?

vi) Asasi yetu itawezaje kupata mamlaka bila kuwa na nyaraka zozote za kisheria za kuithibitisha?

Mkutano ulijiekeza katika kutafuta majibu ya baadhi ya hoja hizi na nyinginezo zinazohusiana na hizo. Ushauriano uliendelea kwa juma zima ndipo maamuzi muhimu yakafikiwa na kwa pamoja Mikono wote wakatoa matamko muhimu kwa jumuiya ya Kibahá'i iliyokuwa inasubiri kwa shauku kubwa. Kwa vipindi tofauti tofauti mkutano ulihitaji kupata msaada wa ushauri na utekelezaji kutoka kwa mwanasheria mahiri wa miaka mingi wa Mlinzi Dkt. Abraham Weinshall. Hatimaye, tarehe 25 Novemba 1957,

mkutano maalum wa faragha wa Mikono wa Hoja kwa pamoja ulitoa taarifa rasmi kuwa: i) Shoghi Effendi hakuacha mrithi na hakuteua mtu yeyote kuwa mlinzi mwingine baada yake ii) baada ya kupitia Wasia na Agano la Abdu'lBahá na nyaraka kadhaa za Shoghi Effendi, Mikono wa Hoja kwa pamoja wameunda asasi ya Waangalizi wa Hoja (Custodians) na kuchagua wajumbe tisa miongoni mwao kuwa wajumbe wake ambao watakaa Haifa ili kufanya kazi zote zilizokuwa zinafanywa na Mlinzi kama mkuu wa Hoja kwa niaba ya Mikono wote wa Hoja iii) baadhi ya majukumu ya asasi hii ni kutunza na kulinda mali zote za Kibahá'i katika Nchi Takatifu na duniani kote, kufanya mawasiliano na kutoa miongozo kwa mabaraza yote ya kitaifa, kuendeleza mpango wa miaka kumi kama ulivyokuwa umeasisiwa na Mlinzi na kusimamia maendeleo ya shughuli zote za Imani kote duniani na kuwa na mawasiliano ya karibu na Mikono wote wa Hoja.

Baada ya uchaguzi waliandika azimio ambalo Mikono wote walitia saini zao kama uthibitisho wao wote kukubali kuundwa kwa asasi hiyo, nalo lilisomeka hivi:

***Sisi tuliosaini hapa chini; kwa hadhi yetu kama Mikono wa Hoja ya Mungu tuliotajwa na kuteuliwa na Mlinzi wa Imani ya Kibahá'i mwadhama Shoghi Effendi Rabbani, tuliokuwa tumekutana leo tarehe 25 Novemba, 1957 katika Makao Makuu ya Kibahá'i na tukiwa asasi ya juu ya Jumuiya ya Kibahá'i ya Ulimwengu KWA PAMOJA TUNAUNDA NA KUTAMKA KAMA IFUATAVYO;***

***KWA KUWA Mlinzi wa Imani ya Kibahá'i mhashamu marehemu Shoghi Effendi Rabbani alifariki akiwa London (Uingereza) tarehe 4 Novemba, 1957 bila kuwa ameteua mrithi wake; na KWA KUWA sasa jukumu lipo kwetu kama Wasimamizi Wakuu wa Imani ya Kibahá'i Ulimwenguni, kudumisha umoja, usalama na maendeleo ya Jumuiya ya Kibahá'i ya Ulimwengu na asasi zake; NA KWA KUWA kulingana na Wasia na Agano la 'Abdu'l-Bahá "Mikono wa Hoja ya Mungu lazima wachague tisa miongoni mwao ambao muda wote watashughulika na huduma muhimu za kazi za Mlinzi wa Hoja ya Mungu". Tunateua na kuwataja hawa kutoka miongoni mwetu na kwa niaba yetu kuwa Waangalizi wa Imani ya Kibahá'i ya Ulimwengu:***

*1. <u>Ruhiyyih Rabbani</u>*

*2. Charles Mason Remey*
*3. Amelia E. Collins*
*4. Leroy C. Ioas*
*5. Hasan Balyuzi*
*6. 'Alí-Akbar Furútan*
*7. Jalal Khazeh*
*8. Paul E. Haney*
*9. Adelbert Muhlschlegel*

***Kuhudumia, kwa maelekezo na maamuzi kama yatakavyotolewa na sisi kama Wasimamizi Wakuu wa Imani ya Kibahá'i ya Ulimwengu-kazi zote, haki na mamlaka ya urithi wa Mlinzi wa Imani ya Kibahà'i, mhashamu marehemu Shoghi Effendi Rabbani ili kuendeleza maslahi ya Imani ya Kibahá'i ya Ulimwengu mpaka hapo Nyumba ya Haki ya Ulimwengu itakapokuwa imeanzishwa na kuchaguliwa kwa mujibu wa Maandiko Matakatifu ya Baha'u'lláh na Agano na Wasia wa 'Abdu'l-Bahá.***

***Tumesaini kama ifuatavyo:***

*Ruhiyyih Rabbani, Zikrulláh Khadem, Musa Banani, Charles Mason Remey, Ali Mohammad Varqa, William Sears, Amelia E. Collins, T. Samandari, John Robarts, Leroy C. Ioas, Jalal Khazeh, Enoch Olinga, Ugo Giachery, John Ferraby, Agnes B. Alexander, Hasan M. Balyuzi, Paul E. Haney, H. Collis Featherstone, Shoaullah Alai, Horace Holley, Clara Dunn, Ali Akbar Furútan, Abul Qasim Faizi, Dkt. Rahmatulláh Muhajir, Hermann Grossmann, Dkt. Adelbert Muhlschlegel* ([12])

Mabaraza ya kitaifa pamoja na jumuiya zote za Kibahá'i, baada ya kupokea taarifa hizi wote waliunga mkono na kuahidi utiifu wao kwa Asasi ya Waangalizi. Pia serikali ya Israel ilikubali na kuitambua rasmi asasi hii ya Waangalizi kama mkuu wa Imani ya Kibahá'i. Huu ulikuwa ni ushindi mkubwa kwa asasi ya Mikono wa Hoja na hatua muhimu iliyoivusha Imani kusonga mbele katika hatua nyingine. Ni uaminifu wao kwa Agano la Baha'u'lláh uliowawezesha kuvuka hatua hii nyeti na muhimu katika historia ya Imani.

## Utumishi wa Waangalizi (1957 - 1963)

Mikono wote waliochaguliwa kuwa wajumbe wa Asasi ya Waangalizi walilazimika kwenda kuishi Makao Makuu ya Imani mjini Haifa kuanzia wakati huo. Hivyo, baadhi walitoa dhabihu kazi zao nzuri, mipango yao na jumuiya zao walizozizoea na kuzipenda kwa ajili ya kuja kuihudumia Hoja kwenye Makao Makuu. Mkutano ulikuwa umefanya maamuzi kuwa asasi ya Waangalizi itafanya kazi bila kuwa na maofisa wa kudumu, kwa maana kwamba nafasi kama ya mwenyekiti au katibu zingehudumiwa kwa mzunguko kwa kila mjumbe. Pia akidi yao ya mikutano iliwekwa kuwa ya wajumbe watano. Mikono wengine wote walirejea kwenye vituo vyao ili kuendelea kusimamia maendeleo ya mpango wa Mpambano wa Miaka Kumi na walikuwa wakija Haifa kila mwaka kwa ajili ya mikutano ya Mikono wote pale ilipohitajika kufanya hivyo. Moja ya majukumu ya mwanzo kabisa yaliyotekelezwa na asasi ya Waangalizi ilikuwa ni kukamilisha mpango wa kuvunja jengo lililokuwa linakaliwa na wavunja-agano pale Bahji karibu na kaburi takatifu la Baha'u'lláh. Kazi hiyo ilikamilishwa Desemba, 1957. Vile vile walisimamia na kukamilisha ujenzi wa jengo la makumbusho ya Kibahá'i, ambalo ujenzi wake ulikuwa umeanzishwa na Shoghi Effendi, jengo ambalo lilikamilika na kufunguliwa kwa mahujaji mwaka 1961. Pia katika kuendeleza mipango na kazi za Mlinzi, asasi ya Waangalizi ilihamasisha na kukusanya michango pamoja na kusimamia ujenzi wa Nyumba za Ibada mama tatu za mabara; ya Kampala-Afrika, ya Sidney-Australia na Frankfurt-Ulaya. Ujenzi wa Hekalu la Kampala ulianza Januari, 1958 na lilifunguliwa Januari, 1961; lile la Sydney lilianza Machi, 1958 na lilizinduliwa Septemba, 1961 na lile la Frankfurt lilianza Novemba 1960 na lilikamilika 1962. Jambo lingine kubwa walilokabiliana nalo Waangalizi lilikuwa ni kesi za Wabahá'i wa nchi ya Morocco. Kesi hii ilihusisha Wabahá'i 14, ambao wengi wao walikuwa ni wafanyakazi serikalini. Walikamatwa, wakateswa na kufunguliwa mashtaka mabaya ya kusingiziwa uhaini na uchochezi, kwa sababu tu ya wao kuwa Wabahá'i. Desemba 1962, hukumu ya mahakama ya jimbo la Nador ilitoa hukumu ambapo wengine waliachiwa isipokuwa watu 5 waliohukumiwa kifungo cha maisha na 3 walihukumiwa kunyongwa. Asasi ya Waangalizi ilitafuta wanasheria wa kuwasaidia kukata rufaa kwenye mahakama kuu na vile vile kuomba nchi kadhaa hasa Amerika kuishinikiza Morocco kupitia Umoja wa Mataifa kuzingatia haki za wachache nchini humo na kutoa hukumu ya haki. Pia iliwaomba Wabahá'i kote duniani

kusema sala kwa ajili yao na kutuma malalamiko yao kwa mfalme wa Morocco. Kesi katika mahakama kuu iliendelea kwa miezi 20, mwishowe Desemba 1963, mahakama kuu ilitoa hukumu ambapo watuhumiwa wote waliachiwa huru, wakalipwa fidia na kurudishwa kazini. Hakika ulikuwa ushindi mkubwa ambao haukutegemewa.

Katika kipindi chote cha utumishi wa Asasi ya Waangalizi, Mikono wa Hoja walifanya mikutano sita kabla ya uchaguzi wa Nyumba ya Haki na yote ilifanyika Bahji kwenye Nyumba ya Baha'u'lláh. Mwaka 1959 Mason Remey na Hassan Balyuzi waliomba kupumzika kuhudumia kama Waangalizi, wakakubaliwa na hivyo wakachaguliwa John Ferraby na Horace Holley kuchukua nafasi zao na baadaye mwaka 1960 baada ya kifo cha Horace Holley, William Sears alichaguliwa kujaza nafasi yake. Na baadaye mwaka 1962, Amelia Collins alifariki na Hasan Balyuzi alichaguliwa tena kujaza nafasi yake. Mwanzoni mwa mwaka 1960, Mikono wa Hoja walikabiliana na changamoto kubwa iliyojitokeza miongoni mwao. Mkono wa Hoja, Charles Mason Remey alivunja Agano kwa kuusaliti utiifu wake pale alipotangaza kuwa yeye alikuwa ni mrithi wa Shoghi Effendi. Baada ya kuwa ameomba kupumzika kwa sababu ya umri na kukubaliwa na Mikono wenzake, miezi michache baadaye akiwa Marekani alitangaza kuwa yeye alikuwa mlinzi wa pili akimrithi Shoghi Effendi kinyume na tamko la Mikono wa Hoja la miaka mitatu kabla aliloshiriki kulitoa na kutia saini yake lililotaja wazi kuwa Shoghi Effendi hakuacha mrithi. Zaidi ya hapo Mason Remey hakuwa Ghusn (tawi) yaani hakuwa wa uzao wa Baha'u'lláh, hivyo kwa vyovyote vile asingeweza kutajwa na Shoghi Effendi kuwa mrithi wake kinyume na Wasia na Agano la 'Abdu'l-Bahá. Kwa hiyo, 28 Aprili, 1960 Mikono wa Hoja walitoa tamko kwa Wabahá'i wa Ulimwengu kuwa dai la Mason Remey lilikuwa batili na lisilo na mantiki, na kwa hiyo walipuuze. Mara moja madai yake yakakataliwa na Mabaraza yote ya Kitaifa (isipokuwa moja ambalo baadaye lilivunjwa), na jumuiya zote za Kibahá'i duniani, pamoja na Mikono wa Hoja wote. Zaidi ya hapo, Mason Remey akafukuzwa kwenye Imani kwa kuvunja Agano la Baha'u'lláh lililoweka utaratibu wa urithi wa mamlaka ya Imani Yake. Kwa hiyo, kuanzia wakati huo Charles Mason Remey akatangazwa na asasi ya Mikono wa Hoja kuwa mvunja Agano. Huu ukawa ushahidi mwingine wa uthabiti wa Mikono wa Hoja katika Wasia na Agano. Asasi ya Waangalizi ilituma baadhi ya Mikono wa Hoja kwenda katika baadhi ya mataifa kuziimarisha jumuiya zake na kutokana na athari za uasi huo. Mikono hawa walitumwa katika nchi ya Marekani, nchi kadhaa za Ulaya pamoja na Irán. Lakini jambo la muhimu zaidi ni kwamba katika kikao chao cha Novemba 1959 Mikono walishafanya uamuzi kwamba uchaguzi wa

Nyumba ya Haki ufanyike mwishoni mwa mpango wa miaka 10, hivyo waliendelea kusimamia maendeleo ya mpango huo. Kwa kuzingatia maelekezo ya Shoghi Effendi aliyokuwa ameyatoa Januari 9, 1951 ya kwamba uundwaji wa Halmashauri ya Kimataifa ya Kibahá'i ilikuwa ni hatua katika kuelekea uundwaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, hivyo, Aprili 1961, Mikono wa Hoja waliitisha uchaguzi wa Halmashauri hiyo ufanywe na wajumbe wa Mabaraza yote ya Kitaifa yaliyokuwepo wakati huo. Uchaguzi huo ulifanyika kwa kura za kutumwa kwa njia ya posta. Vile vile waliitisha mikutano mikubwa ya mabara ya mwaka 1958, kama Mlinzi alivyokuwa amepanga hapo awali kwamba kungefanyika mikutano hiyo katika muda wa katikati ya mpango. Jambo lingine muhimu kwa Mikono wa Hoja kwa kipindi hicho lilikuwa ni kuhakikisha kwamba muda wote katika Makao Makuu ya Imani kuna akidi ya Waangalizi ili kuweza kufanya maamuzi, yaani Mikono watano kati ya tisa mara zote walipaswa kuwa Haifa. Ili kutimiza hilo walichagua Mikono watatu kushika nafasi hiyo kwa muda pale likitokea pengo. Waliochaguliwa kwa ajili hiyo ni Shua'u'lláh Alai, Ugo Giachery na Ali-Muhammad Varqa. Lakini mwaka 1959 Mikono wawili waliomba kupumzika kwa sababu ilikuwa vigumu kwao kukaa Haifa muda wote, wakaruhusiwa na wengine wawili wakachaguliwa badala yao. Waliochaguliwa kuwa Waangalizi wakati huo Novemba 1959, walikuwa ni John Ferraby na Horace Holley. Vile vile katika kipindi cha uongozi wa Waangalizi, Mikono wanne walifariki dunia, wawili kati yao wakiwa Waangalizi ambao walikuwa ni Horace Holley na Amelia Collins na nafasi zao kama Waangalizi zikajazwa. Mikono wengine waliofariki katika kipindi hicho ni Clara Dunn (1960) na Corinne True (1961). Kwa jumla, Mikono waliohudumu kwenye asasi ya Waangalizi japokuwa wengine kwa kipindi kifupi walikuwa: Hasan Balyuzi, Amelia Collins, Abu'l-Qasim Faizi, John Ferraby, Ali Akbar Furután, Paul Haney, Leroy Ioas, Jalal Khazeh, Adelbert Mühlschlegel, Charles Mason Remey, Horace Holley, William Sears, na Rúhíyyih Khánum.




*Mikono waliohudumu kwenye asasi ya Waangalizi: (Juu kutoka kushoto) Hassan Baryuzi, Amelia Collins, Abu'l Qasim Faizi, John Ferraby, Ali Akbar Furutan, Paul Haney, (chini kutoka kushoto) Leroy Ioas, Jalal Khazeh, Adelbert Mühlschlegel, Horace Holley, William Sears, na Rúhíyyih Khánum*

Ili kupata uelewa wa sura nyingine ya kazi iliyofanywa na Mikono wa Hoja itakuwa vizuri kujua maendeleo na ukunjukaji wa kiasasi wa Imani ulivyotokea tangu kipindi cha Shoghi Effendi. Wakati wa uongozi wa 'Abdu'lBahá hapakuwepo na Baraza la Kitaifa hata moja, lakini wakati wa kipindi cha uongozi wa Shoghi Effendi yaliweza kuundwa Mabaraza ya Kitaifa 26 na katika kipindi cha uongozi wa Mikono wa Hoja baada ya kifo cha Mlinzi hadi kufikia uundwaji wa Nyumba ya Haki, yaliongezeka Mabaraza ya Kitaifa na kufikia idadi ya 56. Shoghi Effendi hapo kabla mwaka 1924, alikuwa ametaja kuwa Mabaraza ya Kiroho ya Mahali na ya Kitaifa ni kama 'msingi ambao nguvu yake ndipo siku za mbele Nyumba ya Haki ya Ulimwengu itaanzishwa'. Hivyo hivyo, wakati Shoghi Effendi anapokea uongozi kutoka kwa babu yake Imani ya Baha'u'lláh ilikuwa imefika kwenye nchi 35. Ilifika kwenye nchi mbili wakati wa Báb, ziliongezeka nchi 13 wakati wa Baha'u'lláh na ziliongezeka nchi 20 wakati wa 'Abdu'l-Bahá. Shoghi Effendi aliongeza idadi hii hadi kufika 219, na wakati wa kipindi cha Waangalizi ziliongezeka tano zaidi na kuwa 224. Vile vile wakati wa Ridván ya 1957 Shoghi Effendi alikuwa ametangaza kwamba kulikuwa na jumuiya za mahali zipatazo 4,200 kote ulimwenguni lakini mwishoni mwa Mpango wa Miaka Kumi, 1963 zilikuwa zimefika 11,210, ongezeko la zaidi ya 7,000. Kuelekea mwishoni mwa Mpango wa Miaka Kumi, Waangalizi waliitisha

uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Walituma ujumbe ufuatao: **''Wasimamizi wakuu wa Imani kwa hiyo wanaitisha Konvensheni katika Nchi Takatifu kwa ajili ya uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwenye siku ya kwanza, ya pili na ya tatu ya Ridván 1963. Wajumbe wote wa Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa na ya Kanda waliochaguliwa na Wabahá'i kwenye Ridván 1962, kulingana na mafundisho, watakuwa ndio wapiga kura wa chombo hiki kichanga cha Utaratibu wa Ulimwengu wa Baha'u'lláh, ambacho katika mashauriano yao imewekwa baraka ya kipekee ya kupokea uvuvio mtakatifu na ambacho maamuzi yake hayatakuwa na makosa kwani yataongozwa na Báb na Baha'u'lláh"** (13)

Katika konvensheni ya Kimataifa iliyofanyika Haifa wajumbe kutoka Mabaraza 56 ya Kitaifa na ya Kanda ndio walioshiriki kuchagua Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa mara ya kwanza. Kama ilivyokuwa mwaka 1961 wakati wa uchaguzi wa Halmashauri ya Kibahá'i ya Kimataifa, mara hii tena Mikono wa Hoja walikuwa wamefanya uamuzi na kuwajulisha wajumbe kuwa wao wasichaguliwe 'waachwe waendelee kutekeleza majukumu yao'. Tarehe 21, Aprili wajumbe wa konvesheni ya kimataifa, wengi wao wakiwa katika mavazi yao ya kiasili, wakapiga kura zao kwa hamasa kubwa. Baada ya zoezi hilo wajumbe wote pamoja na Mikono wakaelekea kwenye kaburi la Baha'u'lláh kutoa shukrani zao kwa kuwawezesha kushuhudia hatua hii ya ushindi mkuu wa kihistoria katika Imani.




*Sahihi za baadhi ya Mikono wa Hoja*

# 7

## HUDUMA YA MIKONO WAKATI WA NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU



*Mikono wa Hoja wakiwa pamoja na wajumbe wa mwanzo wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu waliochaguliwa 1963, wakiwa mbele ya Jumba la Baha'u'lláh - Bahji, Israel*

Tarehe 21 Aprili, 1963 matokeo yalitangazwa, historia ikawa imeandikwa kwa kuundwa kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Ikawa ni shangwe na nderemo kwa wajumbe wa konvensheni ya kwanza ya kimataifa pamoja na Mikono wa Hoja. Lakini ilikuwa furaha na shangwe kubwa zaidi wakati

wajumbe wa Nyumba ya Haki wa kwanza walipotambulishwa siku chache baadaye kwenye mkutano mkubwa wa watu zaidi ya elfu sita mjini London. Huu ulikuwa ni Mkutano wa kwanza wa Kibahá'i wa Dunia uliofanyika kuanzia tarehe 28 Aprili hadi 2 Mei, 1963 kuadhimisha miaka 100 ya kujitangaza kwa Baha'u'lláh mjini Baghdád 1863; na vile vile ulikuwa na dhumuni la kusherehekea mafanikio na kuhitimisha Mpango wa Miaka 10. Kati ya Mikono waliopewa nafasi ya kuongea na umati huo alikuwa ni Mkono wa Hoja Tarazu'lláh Samandari, aliyeshiriki simulizi yake yenye mvuto wa kipekee ya baraka ya yeye kufika mbele ya Baha'u'lláh huko Bahji wakati akiwa kijana mdogo wa miaka 17 hivi. Ni katika mkutano huu kwamba Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ilitoa ujumbe ambao ndani yake zilikuwa ni shukrani kwa kazi kubwa iliyokuwa imefanywa na Mikono wa Hoja: "....... wameshiriki ushindi na kamanda wao mpendwa ambaye aliwainua na kuwateua. Wameiongoza meli kwenye welekeo wake na kuifikisha salama kwenye bandari.'' Baada ya kurudi Haifa, kulikuwa na mikutano mfululizo kati ya Mikono waliokuwa kwenye asasi ya Waangalizi na wajumbe wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ili kukabidhi nyaraka zote muhimu na maelekezo ya mipangilio ya jinsi ofisi zilivyokuwa zikitenda kazi hapo Makao Makuu. Baada ya kipindi kifupi, tarehe 7 Juni, 1963, Waangalizi walijivua rasmi mamlaka na uongozi wa Imani na kukabidhi mamlaka yote kwa Nyumba ya Haki, sehemu ya tamko lao lilisema:

**SISI, TULIOTAJWA HAPA CHINI, TULIOCHAGULIWA NA KUTEULIWA KIKAMILIFU KAMA WAANGALIZI WA IMANI YA KIBAHÁ'I YA ULIMWENGU KWA AZIMIO LA MIKONO WA HOJA YA MUNGU LILILOTOLEWA BAHJI TAREHE 25 NOVEMBA, 1957 kutekeleza ......... kazi zote, haki na mamlaka kwa kumrithi Mlinzi wa Imani, Mhadhama hayati Shoghi Effendi Rabbani katika kuhudumia maslahi ya Imani ya Kibahá'i ya Ulimwengu, hadi hapo Nyumba ya Haki ya Ulimwengu itakapokuwa imeundwa na kuchaguliwa kwa mujibu wa Maandiko Matakatifu ya Baha'u'lláh na Wasia na Agano la 'Abdu'l-Bahá,....... Sasa tunatamka kuwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, imeundwa kwa utaratibu stahiki na kuchaguliwa kwa Konvensheni ya Kimataifa ya Kibahá'i, iliyofanyika Haifa Aprili 21, 22 na 23, 1963 na kwa hiyo, hapa tunaachilia majukumu, haki na mamlaka yote yaliyokuwa yamewekwa juu yetu kwa Azimio lililotajwa la 25 Novemba, 1957....................na tunatamka**

**kwamba majukumu yote yaliyotajwa, haki na mamlaka sasa yanakabidhiwa kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Tunatoa tamko hili kwa niaba ya asasi yote ya Mikono wa Hoja ya Mungu kulingana na mamlaka tuliyopewa na Azimio la Novemba 25, 1957 na asasi ya Waangalizi wa Imani ya Kibahá'i ya Ulimwengu sasa inakoma kuwepo**".(14)

Mnamo Novemba 1964, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu iliitisha kikao cha mashauriano na Mikono wa Hoja (walikuwa wamebaki 22 kwa wakati huo) juu ya hatima na majukumu ya asasi ya Mikono wa Hoja ya Mungu, na baada ya mashauriano ya kina ya siku 14, Nyumba ya Haki ilitoa tamko kuwa 'kutokana na maandiko ya Imani, haikupata njia ya kuendelea au kutunga sheria ya kuiwezesha kuendelea kuteua Mikono wa Hoja, mamlaka hayo yalikuwa yamerithishwa kwa Mlinzi tu". Iliendelea kutamka kuwa ''mamlaka ya kuamua masuala yote yanayohusu shughuli za Mikono wa Hoja kama yalivyokuwa yanafanywa na Shoghi Effendi sasa yatakuwa juu ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kama asasi kuu ya utawala wa Imani ya Kibahá'i". Pamoja na hayo, pia Nyumba ya Haki ya Ulimwengu iliamua kuwa kuanzia wakati huo Mikono wa Hoja pamoja na Washauri wasaidizi hawatahudumia katika asasi za kuchaguliwa. (15)

Hatua nyingine kubwa katika mwendelezo wa shughuli za asasi ya Mikono wa Hoja ilitokea mnamo Juni, 1968 ambapo ili kuendeleza majukumu ya Mikono wa Hoja, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ilifanya uamuzi wa kuanzisha Bodi za Washauri wa Bara. Uamuzi huu ulifanyika baada ya ushauriano kati ya Nyumba ya Haki na Mikono wa Hoja ili kuona ni jinsi gani majukumu muhimu ya Mikono yangepata mwendelezo wakati wao wakiendelea kupungua. Ndipo Nyumba ya Haki ikafanya uamuzi wa kuanzisha Bodi za Washauri wa Bara mnamo mwaka 1968. Zilianzishwa bodi kumi na moja, na kila moja ikihudumia eneo maalumu la kijiografia. Bodi hizo zilikuwa:

- i) Afrika Kaskazini Magharibi
- ii) Afrika Mashariki na Kati
- iii) Afrika Kusini
- iv) Amerika Kaskazini
- v) Amerika ya Kati

vi) Amerika Kusini
vii) Asia Magharibi
viii) Asia Kusini Mashariki
ix) Asia Kaskazini MasharikI
x) Australasia
xi) Ulaya

Katika barua ya 24 Juni, 1968; Nyumba ya Haki ilikuwa imeamua kwamba kuanzia wakati huo, Washauri wa Bara wangekuwa wanateuliwa na kuhudumia kwa vipindi maalum na kuwa urefu wa vipindi vya huduma yao ungeamualiwa hapo baadaye. Wakati huo waliteuliwa Washauri wa Bara 36. Washauri wa Bara sasa wangetekeleza majukumu muhimu ya Mikono wa Hoja ya Ulinzi na Upanuzi wa Imani. Vile vile kuanzia wakati huo wao wangeteua na kusimamia bodi za washauri wasaidizi. Na majukumu ya Mikono wa Hoja sasa yangekuwa ya kiulimwengu kwa maelekezo ya moja kwa moja ya Nyumba ya Haki kwa kila Mkono wa Hoja. Pia ikawapa jukumu Mikono wale iliyokuwa imewaomba hapo kabla kukaa Nchi Takatifu kuwa kiunganishi kati ya Washauri wa Bara na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Mnamo mwaka 1973 bodi nyingine ya Washauri ya Asia Kusini Kati iliongezwa na idadi ya Washauri wa Bara ikaongezwa na kuwa 57. Mnamo mwaka 1975 bodi ya Afrika Kaskazini Magharibi iligawanywa na kuwa bodi mbili za Afrika Kaskazini na Afrika Magharibi, na hivyo kukawa na bodi 12 za washauri. Mnamo mwaka 1979 Nyumba ya Haki ilitangaza kuwa Washauri wa Bara wangehudumia kwa vipindi vya miaka mitano na kuwa tarehe ya kuanza huduma yao ingekuwa ni Siku ya Agano.

Baadaye Novemba, 1980, Nyumba ya Haki ilitangaza kwamba idadi ya bodi za washauri wa bara zilikuwa zimepunguzwa hadi tano na hizo ni: i) Afrika ii) Amerika iii) Asia iv) Ulaya v) Australasia.

Lakini idadi ya Washauri wa bara iliendelea kuwa 57 hadi mwaka 1985 ilipoongezwa na kuwa 72. Baadaye mwaka 1995 idadi yao iliongezwa tena hadi kuwa 81.



*Wajumbe wa mwanzo wa Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa: Ali Akbar Furután, Paul Haney, Florence Mayberry, Aziz Yazdi, Rúhíyyih Khánum Hooper Dunbar, na Abu'l Qasim Faizi*

Mnamo Juni 1973, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ikafanya maendeleo mengine makubwa katika mwendelezo wa kazi za Mikono wa Hoja.

Ilitangaza kuundwa kwa asasi ya Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa katika Makao Makuu ya Imani, Haifa. Wajumbe wake wakawa ni Mikono wote waliokuwa hai wakati huo (walikuwa 17), na ikateua washauri wengine watatu kuwa wajumbe wake. Lakini waliokuwa kiini cha utendaji wa kazi za kila siku hapo Makao Makuu ya asasi hiyo walikuwa ni wale Mikono waliokuwa wanakaa makao makuu, ambao walikuwa ni Rúhíyyih Khánum, Abu'l-Qasim Faizi, Ali Akbar Furután, Paul Haney, Ali-Mohammad Varqa na Collis Featherstone. Washauri watatu waliokuwa wameteuliwa kuwa wajumbe walikuwa ni Hooper Dunbar, Florence Mayberry na Aziz Yazdi. Asasi hii baadaye iliendelea kukunjuka hadi ikawa na wajumbe tisa kama ilivyo sasa. Mwaka 1979 idadi ya Washauri iliongezwa hadi kuwa wanne, na baadaye 1983 wakawa saba na mnamo mwaka 1988 idadi yao ikafika tisa.

Katika hatua ya kuanzisha asasi hii, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ilisema **'inaleta kwenye upeo kazi ya Mikono wa Hoja wanaokaa Nchi Takatifu na kutoa njia kwa mwendelezo wa kazi zao kwa siku zijazo na inaunganisha asasi ya Bodi za Washauri wa bara kwa ukaribu zaidi na zile za Mikono wa Hoja na kwa nguvu kubwa inaimarisha utekelezaji wa majukumu yaongezekayo kwa haraka ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu'.** (16)

Shughuli za Mikono wa Hoja zilibadilika na kuwa za kimataifa zaidi hasa baada ya mwaka 1968 ambapo walikuwa huru zaidi baada ya kuanzishwa kwa Bodi za Washauri wa Bara. Sasa walifanya safari nyingi za kuiwakilisha

Nyumba ya Haki ya Ulimwengu katika mikutano mikubwa na matukio mbalimbali duniani, kama vile uzinduzi wa Mabaraza mapya ya Kitaifa, uzinduzi wa Nyumba za Ibada na kukutana na viongozi wakuu wa kiserikali na mashirika ya kimataifa.

Mnamo mwaka 1992, Mikono wa Hoja watatu waliokuwa bado hai wakati huo, (Ruhiyyih Khanum, Ali Akbar Furután na Ali Mohammad Varqa) walihutubia Mkutano wa Dunia wa Kibahá'i uliofanyika mjini New York, Marekani, ambao ulihudhuriwa na marafiki takribani elfu ishirini na saba. Mikono wa Hoja mara zote walihudhuria konvesheni za kimataifa na pia walikuwa na fursa ya kuongea na mahujaji walioenda hija Nchi Takatifu, mjini Haifa. Wakati wa ufunguzi wa makao ya Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa mjini Haifa mwaka 2001, Mikono wawili wa Hoja waliokuwa hai Ali Mohammad Varqa na Ali Akbar Furután walikaribishwa kuhutubia umati uliokusanyika kwenye sherehe hizo. Kadiri nguvu zao za kimwili zilivyopungua, Mikono waliendelea kukaa Haifa mara nyingi kushiriki ushauriano na wajumbe wengine wa Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa na pia kutoa hotuba zenye uvuvio kwa mahujaji. Ali Akbar Furután alifariki siku ya Agano mwaka 2003 wakati anaongea na mahujaji, na wa mwisho kuondoka hapa duniani alikuwa Dkt. Ali Mohammad Varqa aliyefariki Septemba, 2007.

# 8

## SIMULIZI ZA BAADHI YA MIKONO WA HOJA

### 1. Ali Akbar Furután- Maana ya Wajibu

Siku ya Agano, 26 Novemba 2003 ilinikuta Haifa nikiwa hujaji pamoja na kundi la mahujaji wengine kutoka nchi mbalimbali duniani. Jioni ya siku hiyo ratiba yetu ilionesha kuwa tungekutana na Mkono wa Hoja ya Mungu Bw. Furután, mkutano ungekuwa saa 12 jioni kwenye Kituo cha Mapokezi kwa Mahujaji. Haikuwa mara yetu ya kwanza kukutana naye, kwa mara ya kwanza mimi nilimuona siku ya kwanza ya hija tarehe 24 Novemba. Alitoa hotuba nzuri sana na akatuahidi kuja kuzungumza nasi kila baada ya siku moja. Alisema kuwa kabla ya hapo alikuwa akija kukutana na mahujaji kila siku kwa kuwa kama ambavyo Shoghi Effendi alivyokuwa amesema kwamba, mahujaji ni wageni wa Baha'u'lláh. Lakini sasa madaktari walikuwa wameshauri kuwa asije kila siku kwa sababu ya umri wake. Alituambia tuje siku ya Jumatano pamoja na watoto kwa sababu angeongea kuhusu kufundisha Imani. Sasa unaweza kufikiria tulijisikiaje baada ya kuambiwa kuwa siku hiyo Bw. Furután asingekuja. Nakumbuka kuwa alipokuja siku ya kwanza alionekana amechoka sana na dhaifu. Ilionekana wazi kuwa nguvu zake zilikuwa zinaisha taratibu. Bila shaka kitu nilichofikiria siku hiyo ni kwamba asingekuja kwa sababu ya hali ya afya yake. Mahujaji wengi walianza kuondoka kwenda hotelini kwao, lakini baadhi yetu tukaendelea kukaa tukiwa na matumaini kuwa huenda mkutano wetu bado ungeweza kufanyika. Nilijawa na furaha tulipotaarifiwa kuwa Bw. Furután angekuja, wakati huo ilikuwa saa 12 kasoro dakika 10. Mara alipoingia ukumbini ilikuwa dhahiri kwamba alikuja kwa kujikaza tu. Alionekana amepauka sana kama vile siyo yule wa siku zote. Licha ya hali hiyo, alipoingia moja kwa moja alipanda kwenye jukwaa na kuwasha kipaza sauti. Somo lake lilihusu wajibu wa kufundisha Imani. Kwanza alisoma nukuu ya Baha'u'lláh kutoka ''Makusanyo''; ''**Sema: Fundisheni Hoja ya Mungu, Enyi watu wa Bahá, kwa kuwa Mungu ameamuru kwa kila mmoja wajibu wa kutangaza ujumbe Wake, na Hukiona kitendo hicho kama kitendo**

**bora kabisa kati ya vyote. Kitendo hicho hukubalika iwapo tu yule afundishaye Hoja, yeye mwenyewe tayari ni muumini thabiti kwa Mungu, Mlinzi Mkuu, Mwenye Neema, Mweza yote. Yeye ameamuru hata hivyo kwamba, Hoja Yake ifundishwe kwa njia ya nguvu ya matamshi ya watu na siyo kwa njia ya nguvu. Hivyo ndivyo amri Yake ilivyoteremshwa kutoka Ufalme Wake, Ambaye Ametukuka Kabisa, Mjua Yote." (Makusanyo kutoka Maandiko ya Baha'u'lláh,** uk.278)

Halafu Bw. Furután akaanza kushiriki uelewa wake wa neno "wajibu". Kama mfano, akatusimulia hadithi: "Ilitokea kule nchini Urusi wakati wa mfalme Nikolai II akiwa mtawala. Siku mmoja jioni Nikolai II alikuwa akitembeatembea kwenye viunga vya jumba lake la kifalme, akamuona mlinzi ambaye alionekana ni mgonjwa sana, uso wake ukiwa umevimba na mwekundu. Alimkaribia na kumuuliza alikuwa anaumwa nini. Mlinzi akajibu kuwa alikuwa anaumwa malaria. Mfalme akamwambia kuwa alikuwa anahitaji tiba na hivyo anamruhusu kwenda nyumbani. Lakini yule mlinzi akajibu kwamba hawezi kutoka kwenye lindo bila ruhusa ya mkubwa wake wa kazi na kwamba ulikuwa ni wajibu wake kulinda jumba la mfalme hadi pumzi yake ya mwisho. Hapo mfalme Nikolai II akachukua bunduki yake na kumwambia kuwa kama ni hivyo basi yeye atashika zamu ya lindo lake na kwamba akija mkubwa wake atamwambia kuwa yeye mwenyewe ndiye aliyemruhusu na kwamba amemshikia zamu yake." "Hiki ndicho wajibu humaanisha" alisema Bw. Furután, " sababu ya mimi kuja leo ni kwa sababu ilikuwa ni wajibu wangu kuja. Kama ni wajibu, ni lazima kuutimiza" watu wengi wanajua kwamba Bw. Furután aliishi na kusomea Urusi na kwamba hupenda kuongea Kirusi. Kwa bahati marafiki kutoka Urusi walikuwa kwenye mkutano huo, na wakati anasimulia hadithi hiyo, mara kadhaa alikuwa akitafsiri baadhi ya maneno kwa Kirusi na hasa maneno ''wajibu'' na ''jukumu''. Wakati Mkono wa Hoja Bw. Furután alipomaliza hotuba yake, mara moja aliwaendea marafiki Warusi na kuwauliza kwa Kirusi: marafiki mmeelewa nilichosema? Mmeelewa maana ya wajibu na jukumu?" Hayo yalikuwa maneno yake ya mwisho katika maisha yake hapa duniani kwani, dakika chache zilizofuata akawa amefariki dunia. Alifariki mbele yetu, kwa amani na heshima mikononi mwa mahujaji aliowapenda sana. Maisha yake na kifo chake kwangu ulikuwa mfano wa huduma ya kweli, uthabiti katika Agano, na uaminifu kwa Hoja ya Mungu. Kwa maisha yake

alituonesha wajibu ni nini na jinsi tunavyotakiwa kuutimiza hadi pumzi ya mwisho! (Ilisimuliwa na: Irina Musuc Via Dennis Chee – Malaysia)

## 2. Amatu'l-Bahá Rúhíyyih Khánum na Ufundishaji wa mtoto

Amatu'l-Bahá Rúhíyyih Khánum katika mojawapo ya kumbukumbu zake alisema kuwa siku moja alikuwa kwenye mkusanyiko wa fayasaidi na kundi la watangulizi wa Kiajemi na Kiingereza. Mmoja wa walioalikwa alikuwa ni mwanaume mtu mweusi ambaye alikuwa amekaa akisikiliza kwa makini. Ghafla mlango ulifunguliwa na binti mdogo wa mmoja wa watangulizi wa Kiingereza aliingia ndani akiwa na chupa yake ya maziwa mkononi, akawaangalia watu wote waliokuwepo halafu akaenda moja kwa moja kwa yule mwanaume mweusi na kukaa mapajani pake, akamwangalia usoni, akatabasamu na kumbusu na kisha akatulia na kuanza kunywa maziwa yake kwenye chupa. Mama mmoja wa Kiajemi akajaribu kwenda kumchukua kutoka mapajani pa yule bwana mweusi lakini Amatu'l-Bahá akamwambia kwa Kiajemi ‘’mwache hapo alipo, anafundisha Imani kwa njia yake’’. Baada ya mkutano, yule mwanaume akasogea karibu na Amatu'l-Bahá na kumwambia kuwa alitaka kuwa kama yeye na kwenda kufundisha kila alipokwenda kufundisha Imani. Amatu'l-Bahá alimwangalia na kumuuliza kama na yeye tayari alikuwa Mbahá’i. Akajibu kuwa ndiyo alikuwa tayari ni Mbahá’i; Amatu'l-Bahá akashangaa na kumuuliza, “tangu lini? kwa vipi na kwa nini?’’. Akajibu, ‘’Tangu muda mfupi uliopita wakati huyu binti mdogo alipokuja kwangu, akanibusu na kukaa mapajani pangu, akatulia na kusinzia kwa utulivu mkubwa. Kutoka wakati huo nilifikiria kuwa binti huyo alikuwa na uelewa mzuri ambao haukuwa na chembe ya ubaguzi. Wazazi wake inaonesha hawakuwa na ubaguzi wowote katika kumuelimisha, hivyo nikajisemea kimoyomoyo kuwa hii ndiyo Imani inayonifaa. Ndio maana sasa mimi ni Mbahá’i.’’

## 3. Abu’l Qasim Faizi: Nafsi ni Kisu Kikali

Rafiki mmoja alisimulia kisa kimoja kuhusu Qasim Faizi alipokuwa Bahrain. Alifikiri kama walivyo watu wengi kwamba angefurahia kupewa sifa. Baada ya muda mfupi aligundua kuwa Faizi alikuwa hapendi mazungumzo ya aina hiyo na kwa kweli alikasirika kama mtu angeanza kumsifia. Miaka kadhaa baada ya kuondoka huko, aliposikia kuwa marafiki wa Bahrain walikuwa

wametundika picha yake kwenye Bahá'i senta yao mpya alihuzunika sana. Aliwaandikia barua na kuwaomba waiondoe hiyo picha mara moja.

Faizi alikuwa akisema kuwa nafsi ni kama 'kisu kikali' na safari ya maisha ni kama 'kupanda jabali refu kwa kutumia kamba' huku ukiwa umeshika kisu kikali; muda wowote wakati ukipanda kwa kamba kisu kinaweza kugusa kamba kikaikata na ukadondoka, hata kama umekaribia kufika juu kileleni'.

## 4. Dkt. Muhajir Aliwapenda Watangulizi

Watangulizi wawili wa Ufilipino hukumbuka matembezi ya Dkt. Muhajir wakati wakiwa katika hali ya upweke na ugumu kwenye utangulizi. Katika kipindi cha miaka yote ya utangulizi wao hakuna mwingine yeyote aliyewatembelea isipokuwa yeye. Angefika akiwa amechoka sana baada ya kusafiri kwa zaidi ya saa kumi na nane kwa malori na mabasi akikaa nao siku mbili au tatu kwenye mji mdogo walipokuwa watangulizi. Angewaletea salaam za familia zao alizokuwa akizitembelea kabla hajafanya safari ya kuwatembelea, akiwapa zawadi kutoka kwa familia zao na kuwasaidia fedha ikiwa walikuwa na mahitaji. Baadaye, baada ya kuwapongeza kwa huduma waliyokuwa wanaitoa angewaaga kwa kuwaahidi kuwatembelea tena miezi michache baadaye. Kusudi lake la kuwatembelea halikuwa kujadiliana nao mafundisho ya kina au mambo magumu wala kufuatilia kama walikuwa wametekeleza maelekezo yake, bali alitaka tu kuwapongeza na kuwasaidia katika huduma waliyokuwa wanaifanya. "Kama naweza kuleta furaha katika mioyo ya Wabahá'i, nikawapa mapendekezo machache jinsi ya kufanikisha kazi yao na wakati huo huo nikafundisha watu wachache mimi mwenyewe, basi nitakuwa nimekidhi haja ya moyo wangu" alisema.

## 5. Dkt. Muhajir alihimiza Kuwa na Malengo Makubwa

Bi. Nasrin Buroumand hukumbuka changamoto ambazo **Dkt.** Muhajir alipenda marafiki wajipe: "alikuwa amekuja kukutana nasi—mabinti wawili wa Kiajemi tuliokuwa tumeenda kwenye utangulizi huko India kwa ushawishi wake........ mara zote alitushauri kutochelewa". Hakukuwa na muda wa kupoteza. Kama tulihitaji vitabu tulipaswa kuvifuata New Delhi wenyewe badala ya kuagiza na kukaa kusubiri vitumwe, hiyo ilikuwa ni kupoteza muda. Siku moja alituuliza ni kwa nini tusingefanya vijiji vyote kuwa vya Wabahá'i? Tulimjibu kwa kweli kuwa hatukuwahi kuliwaza hilo.

Kwa utaratibu alitueleza njia na jinsi ya kufanya hilo na baadaye akasema “Je, tunaweza kusaidia kuunda Mabaraza ya Mahali elfu tano? Tukashtuka, akacheka na kusema “Sawa, vipi mabaraza mia tatu?” Hili lengo lilionekana angalau linawezekana na hivyo tukatikisa vichwa kukubali. Safari yake iliyofuata tuliweza kumpa taarifa ya kuunda mabaraza mia moja na themanini, na vijiji saba vya Wabahá’i wote. Alifurahi, macho yake yaling’aa kwa furaha na kutuambia kuwa tulikuwa tumefanya miujiza na tulipaswa kumshukuru Mungu kwa baraka hii kubwa.

## 6. Dkt. Muhajir Juu ya Kuchangia Imani

Mkono wa Hoja Dkt. Muhajir, usiku mmoja akiwa na Wabahá’i ndani ya Bahá’i senta iliyojengwa kwa tope kijijini Kavivira, Zaire (sasa DRC), ambapo katika kijiji hicho nyumba zote zilikuwa za nyasi na tope. alisema: “mimi nilizaliwa katika nyumba ya tope kama hizi zenu, familia yetu haikuwa na uwezo wa kifedha lakini babu yetu alitamani sisi uzao wake tusome hadi chuo kikuu. Hivyo alimwandikia ‘Abdu’l-Bahá kupata ushauri Wake. ‘Abdu’l-Bahá alimjibu kuwa achangie mfuko wa Imani bila kukoma na tamanio lake litawezekana. Alitii, na kweli sisi sote tumepata elimu ya chuo kikuu’’.

## 7. Martha Root alizunguka Dunia mara 4

Mwaka 1918 ‘Abdu’l-Bahá alimwambia Martha ‘’unguruma kwa mwito wa Ufalme Mtakatifu’’........ “utashuhudia matokeo makubwa na mathibitisho yasiyo ya kawaida.” Hii ilikuwa katika kujibu barua Yake baada ya Martha Root kumwandikia ‘Abdu’l-Bahá akieleza kuwa alikuwa na shauku ya kusafiri dunia nzima kueneza ujumbe wa Imani ya Kibahá’i ikiwa ni kuitikia ujumbe wa ‘Nyaraka za Mpango Mtakatifu’. Akiwa amefurahishwa mno na majibu ya ‘Abdu’l-Bahá, Martha akiwa na umri wa miaka 47 mara moja akajaza vipeperushi na vitabu katika mabegi yake na akaanza safari kuelekea Amerika Kusini. Alipanda meli iliyokuwa inachukua muda wa wiki mbili kufika huko. Siku ya pili tu, akakumbuka maneno ya ‘Abdu’l-Bahá kuwa alipaswa ‘kuunguruma kwa mwito wa Ufalme kwa watu wote’, hivyo akaona fursa na kwenda kumuomba nahodha wa meli ruhusa ili jioni hiyo aongee juu ya Imani ya Kibahá’i kwa wasafiri. Nahodha akamkubalia na akaandika tangazo kuwa mama mmoja aitwaye Martha Root angeongelea juu ya Imani ya Kibahá’i jioni hiyo kwenye ukumbi mkubwa wa meli hiyo. Siku hiyo jioni akaweza kuongea juu ya Imani kwa umati mkubwa wa wasafiri kwenye meli

hiyo, ambapo wote ilikuwa mara yao ya kwanza kusikia juu ya Imani. Akiwa mwandishi wa habari mwenye tajiriba, alipofika Brazil aliendа moja kwa moja kwenye vyumba vya habari akaanza kueleza madhumuni yake kwa wanahabari na akapewa nafasi kuandika makala juu ya ujumbe wa Baha'u'lláh kupitia magazeti. Mara zote alikuwa akisema "kama mtu akiona woga kuomba fursa ya kuongea na watu, akumbuke kuwa hakuna siku inayokuja mara mbili". Alisafiri, kula na kuishi maisha rahisi na mazungumzo yake yalikuwa rahisi akiyatoa kwa upendo mkubwa. Hakuonesha kama yeye alikuwa mtu muhimu au kuwa na hadhi yoyote. Aliishi kwa kuandika makala kwenye magazeti na wakati mwingine kufundisha watu kiingereza na kupata malipo kidogo. Alizungumza na makundi ya watu wa aina zote kila sehemu duniani. Hata wafalme na watu mashuhuri aliwafikia na walivutiwa na mazungumzo yake. Mmoja wao alikuwa ni Malkia Marie wa Romania. Akitafuta njia ya kumfikia, kwanza alimtumia barua na kitabu cha Baha'u'lláh na Wakati Mpya. Malkia alikisoma usiku huo, kikamvutia na akamkaribisha Martha kumtembelea siku iliyofuata, yaani Januari 30, 1926. ''Naamini mafundisho haya ni suluhisho la matatizo ya sasa ya dunia,'' Malkia alimueleza Martha. Baadaye Malkia alihimiza watu wote kuyatafiti mafundisho ili yasisimue mioyo yao kama yalivyosisimua moyo wake. Martha alipata nafasi ya kukutana na kumshirikisha mafundisho ya Baha'u'lláh tena na tena mara nane kwa siku tofauti tofauti. Huyu Malkia Marie yasemekana ni mtu wa kwanza kutoka ukoo wa kifalme aliyeyakubali mafundisho ya Baha'u'lláh. Alikuwa ni mjukuu wa Malkia Victoria wa Uingereza. Katika safari zake za ufundishaji Imani, Martha Root alizunguka dunia kama mara nne hivi akifundisha katika mabara kadhaa, katika vyuo vikuu zaidi ya 400, na kwa viongozi na wakuu wa nchi na serikali kadhaa duniani.

### 8. Abu'l Qasim Faizi-aliambiwa kuwa 'Tofauti'

Katika kundi la mahujaji waliokuwa Nchi Takatifu wakati fulani, alikuwepo mwanamke mmoja aliyeonekana kama mshamba, aliyejulikana kama Rubabih. Rubabih alikuwa amefanya kazi za ndani kwa miaka ishirini hivi, huku akiweka akiba kidogo kidogo hadi akafikisha kiasi cha kumwezesha kwenda hija. Alikuwa na nguo moja tu ya kubadilisha na alikuwa hajasoma, na kutokana na muonekano wake na ukimya wake mwingi, bila kudhamiria hakuna aliyekuwa anamjali kwenye kundi la mahujaji wenzake. Usiku

mmoja, siku ya mwisho ya hija ya kundi hilo ghafla Rubabih aliingia kwenye Nyumba ya Mahujaji akiwa ameshikilia albamu ya picha kifuani pake huku akilia kwa kwikwi. Mahujaji wenzake aliowakuta ukumbini hapo hawakuelewa sababu ya kulia kwake kwani aliendelea kulia bila kueleza chochote na wala hawakuweza kumzuia kuendelea kulia. Mmoja wao taratibu alichukua ile albamu aliyokuwa ameishikilia kifuani na kuiangalia. Ilikuwa imejaa picha nzuri za Makaburi Matakatifu, bustani na maeneo yote matakatifu ya Kibahá'i, kila picha ikiwa na maelezo, na historia ya kila picha iliandikwa kwa mwandiko mzuri wa Mkono wa Hoja Abu'l Qasim Faizi. Alikuwa ameandaa albamu hiyo maalum kwa ajili ya Rubabih na kwa kuwa ilikuwa siku ya mwisho ya hija alimkabidhi kama zawadi kuonesha upendo wake kwake ili iwe kumbukumbu yake kwa hija yake atakaporudi nyumbani kwao Irán. Baadaye hujaji mmoja alipomueleza Abu'l Qasim Faizi kile kilichotokea kwa Rubabih baada ya kupewa hiyo zawadi, Bw. Faizi alimjibu kuwa Mlinzi alikuwa akimwambia mara zote 'kuwa tofauti', ''kuwaona watu wenye uwezo, haiba na mafanikio ni rahisi kwa kila mtu; lakini mara zote awe makini na kujitahidi kuwatambua akina Rubabih wa ulimwengu huu''.

## 9. Ukarimu wa Amelia Collins

Wakati ule ambapo Mkono wa Hoja Amelia Collins akikaa Haifa, mara nyingi alipata baraka ya kuwa karibu na Mpendwa Mlinzi, na alivutiwa sana na Shoghi Effendi, mara zote akitaka kutoa huduma yoyote. Alikuwa akiishi kwenye chumba kidogo kilicho karibu na nyumba ya Mpendwa Mlinzi. Usiku mmoja, usiku sana Amelia alishtuka kuona kuwa taa ilikuwa inawaka kwenye chumba cha Mlinzi. Akalala lakini baadaye usiku wa manane aliposhtuka tena usingizini akaona bado kulikuwa na mwanga kwenye chumba cha Mlinzi. Na tena alishtuka alfajiri ya saa kumi na moja akaona bado taa ilikuwa ikiwaka, hivyo akafikiri kuwa Mlinzi alikuwa hajalala usiku kucha. Akajiuliza, ni kitu gani kilikuwa kinamtatiza hadi kusababisha Mlinzi asilale hata kwa saa moja?

Asubuhi mapema, Amelia akaenda na kugonga kwenye mlango wa Mlinzi, akiomba ruhusa kuingia. Aliporuhusiwa aliingia mara moja, na moja kwa moja akasema ''Mpendwa Mlinzi, hukulala hata kidogo usiku kucha, kuna nini? Kuna tatizo gani?'' Mlinzi akajibu, ''Nilikuwa na shughuli nyingi na nilikuwa nasali''. Amelia akasema kwa msisitizo, "nadhani kuna jambo jingine jipya, tafadhali nishirikishe jambo hilo ili ujipunguzie uzito wa

usumbufu wa suala hilo.'' Baada ya kusisitiza sana, hatimaye Mlinzi akasema, ''Kuna sehemu ya kiwanja ambacho kilibarikiwa kwa nyayo za Baha'u'lláh, lakini ni mali ya serikali ya Israel ambayo sasa inataka kukiuza. Jumuiya ya wakristo inataka kukinunua lakini serikali ya Israel imewaambia kuwa wana viwanja vingi ambavyo hadi sasa hawajaviendeleza, lakini Wabahá'i wameendeleza kila kiwanja wanachopata, kwa hiyo hiki kiwanja wangepewa Wabahá'i kwanza isipokuwa kama Wabahá'i hawatakichukua ndiyo watauziwa Wakristo. Hivyo serikali imenitaka mimi nikinunue kwa ajili ya Wabahá'i, na ningependa kukinunua kwa ajili ya Nyumba ya Ibada lakini fedha hazipo, na nisingependa kuwaandikia tena marafiki wa Irán kuchangia fedha kwa ajili hiyo. Muda ni mfupi, tatizo langu ni kwamba tarehe ya mwisho niliyopewa ni Alhamisi ijayo, na kama hatutaweza kukinunua kwa muda huo tutakuwa tumepoteza fursa hiyo.''

Hapo hapo Amelia akaomba ruhusa ya kuondoka. Akaenda moja kwa moja kwenye ofisi ya telegrafia akatuma ujumbe nchini Argentina wa kumtaka wakala wake kuuza sehemu ya hisa zake za kwenye mgodi kwa bei yoyote ili mradi aweze kumtumia dola 50,000 (dola elfu hamsini) nchini Israel kabla ya Alhamisi. Wakala wake akauza hisa zake kwa nusu bei, akamtaarifu na akatuma kiasi cha fedha ndani ya muda. Amelia alikwenda kwa Mlinzi Jumatano akiwa na fedha zilizohitajika. Mlinzi alifurahi sana kuweza kununua kipande hicho cha ardhi kilichobarikiwa kwa nyayo za Baha'u'lláh.

Ni watu watatu ndiyo waliojua juu ya hili: Mlinzi, Rúhíyyih Khánum na Amelia.

Baadaye Mlinzi aliagiza mnara mrefu wenye pande nne zilizochongoka kusimikwa katikati ya kiwanja hicho. Mnara huo ulifika Haifa kwa bahati mbaya wakati Mlinzi amekwishafariki. Mnara huo ulihifadhiwa karibu na kiwanja hicho kwa maelekezo ya Mikono wa Hoja. Baada ya kuanzishwa kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, iliagiza mnara huo upelekwe na kusimikwa katikati ya kiwanja hicho kama yalivyokuwa matakwa ya Mlinzi. Maandalizi muhimu yalifanyika, usiku mmoja mnara ulipakiwa kwenye lori ukapelekwa kwenye kiwanja hicho. Njia ya kufika hapo ilipitia kwenye mtaa mwembamba ambao usiku huo ulizibwa na gari mbili zilizokuwa zimeegeshwa kwenye mtaa huo. Na kwa kuwa hapakuwa na njia nyingine, ililazimika magari hayo yasukumwe ili kupisha njia. Wakati winchi inaunyanyua kupita eneo hilo ghafla uliteleza na kudondoka chini na

ukapasuka vipande viwili. Kila mmoja alishtuka na kubaki kimya kwa muda bila kufanya kitu. Mkono wa Hoja aliyekuwepo alishauri watu wasogee karibu ili kuchunguza kitu gani kilitokea. Uchunguzi wa karibu ulionesha kuwa mnara huo ulikuwa umepasuka na kuacha vipande safi kama vile ulikatwa na kisu. Uchunguzi wa karibu zaidi ulionesha kwenye mpasuko wa vipande hivyo kulikuwa na maandishi ''Amelia Collins'' katikati yake. Waligundua kuwa mnara huo ulikuwa umetengenezwa kwa kuunganisha vipande viwili vyenye maandishi hayo ndani ya viungio vyake. Hakuna aliyeweza kutoa maelezo kamili na kila mmoja alifurahi kuwa ungeweza kuunganishwa tena na kuwa salama. Siku iliyofuata walimtembelea Rúhíyyih Khánum na kumuuliza kama angekuwa na maelezo juu ya maandishi hayo. Alishiriki simulizi hii ya jinsi kiwanja hiki kilivyonunuliwa na uamuzi wa Mlinzi wa kuweka mnara huo kama utambuzi wa huduma ya dhati na upendo ya Amelia Collins.

(Imesimuliwa na Bw. Zabíh)

## Mikono wa Hoja Juu ya Huduma ya Utangulizi

Mlinzi Shoghi Effendi akielezea majukukumu ya Mikono wa Hoja:

"Mojawapo ya jukumu muhimu la Mikono na Wasaidizi wao ni kuchochea watangulizi juu ya asili ya utakatifu wa huduma yao na kuwahimiza kubaki katika vituo vyao licha ya ugumu na shida, na kutunza kwa gharama yoyote ile tuzo walizozipata kwa kazi kubwa. Na hivyo hivyo kwa wale walioinuka kuimarisha vituo dhaifu au kuasisi vipya……. Wabahá'i wa mwanzoni walitoa maisha yao, mara nyingi maisha ya watoto wao na ya kwao kuisimamisha Imani''.

## Baadhi ya kauli za Mikono wa Hoja katika kutimiza jukumu hili:

''Mbali na hili kuna vitu viwili muhimu vya kuzingatia kila mara; kwanza, kila mtangulizi au anayeinuka popote kufundisha Hoja ya Mungu, lazima afanye hivyo kwa sababu ya Mungu, akitoa huduma hii kwa ajili ya Mungu pekee na akitumaini tuzo kutoka Kwake tu na si kwa mwingine yeyote, na kama ana matumaini mengine mara zote atakatishwa tamaa na kuumia. Pili, ni lazima afundishe watu akielewa kuwa wakishaukubali ujumbe wa Baha'u'lláh, uhusiano wao ni wa moja kwa moja Kwake; amekuwa Baha'u'lláh wao, Mdhihirishaji wao kutoka kwa Mungu na kwamba uhusiano wao na Yeye siyo

kupitia mtangulizi, au kamati ya ufundishaji ya eneo lingine, wanajitegemea, kupitia mtangulizi daima kutakuwa na upendo, ushauri na msaada unapohitajika lakini uhusiano waliouanzisha sasa na Hoja ya Mungu ni ule unaojitegemea. Ni kama familia ambayo inamzaa mtoto na kumlea, kadiri akuavyo mtoto huanza kudai uhuru zaidi na wazazi wanavyompenda mtoto huanza kuumia wakiona kuwa atafanya makosa ambayo kama angewasikiliza tu labda asingeyafanya. Lakini mtoto hatawasikiliza kila mara na wazazi hawawezi kuishi maisha yake. Mbahá'i mtangulizi ambaye ni mzazi wa kiroho lazima ajitoe kwa namna hiyo."

***— Mkono wa Hoja Ruhiyyih Khanum, Kitabu cha Mwongozo Kwa Watangulizi, uk. 21***

"Halafu ikafika siku.....tuliamua kuwa itakuwa bora kwa sababu ya hali iliyopo Ulaya na Ujerumani Adelbert atafanya mengi huko Ulaya kuliko ambavyo angefanya Nchi Takatifu. Nakumbuka nilikuwa nimekutana naye Ujerumani na aliniambia kuwa alikuwa na ugonjwa wa uvimbe kwenye moyo, ambao ungeweza kupasuka sekunde yoyote. Na hiyo ndiyo ilikuwa hali yake ya kiafya kutoka wakati huo (1937) hadi alipofariki hivi majuzi (1980). Nilienda Athens mwaka jana, hasa hasa kumuona. Nafikiri alikuwa kwenye miaka 90...alikuwa dhaifu kama unyoya...lakini nilishangazwa na uwezo wa akili yake, ilinigusa sana kutokana na kile alichosema kuwa 'Nimeshindwa'. Nilikuja hapa Ugiriki kufundisha na kuimarisha Wabahá'i....nahisi nimewaangusha. Siwezi kufanya kile ninachotaka kufanya. Nashindwa kuimarisha jumuiya ya Ugiriki katika Imani'. Nilimueleza kile ambacho kilikuwa wazi kwa kila mmoja kwamba katika umri wake na afya yake kwenda kuwa mtangulizi katika nchi nyingine halikuwa jambo la kawaida. Nilisema 'Adelbert uwepo wako hapa, ukweli kuwa upo hapa ukiwa bado hai katika hali yako hii, ukiwa umejawa na upendo kwa Hoja, kwa Mlinzi na kwa Wabahá'i wa Ugiriki umeweka mfano ung'aao, haya ni zaidi ya maneno yoyote ambayo ungeweza kusema' .... Halafu, kwa kweli alivisha taji tukio zima hili kwa kufia huko. Nafikiri hatujaelewa siyo tu umuhimu wa kuwa mtangulizi bali kustahimili. Moja ya jumbe za mwisho za Shoghi Effendi kwa Wabahá'i wa Ulimwengu ulikuwa kwamba alitumaini watangulizi watabakia katika vituo vyao, na sisi Mikono tunaposafiri katika nchi mbalimbali tunakutana na watangulizi ambao bado wapo kwenye vituo vyao vya huduma. Kwangu, hao ni minara imara sana.."

***

"Kitu kimoja muhimu ni kwamba Musa Banani alifia Afrika. Tulienda kwenye kituo chake cha utangulizi tukazika mifupa yake. Hili ni jambo la kustaajabisha. Alipokuwa anaumwa sana kule Tehrán, mkewe na watoto wake walisema alilia sana na kusema 'Nipeleke Afrika haraka. Sitaki kufia hapa Tihrán. Nataka kurudi nifie kwenye kituo changu cha utangulizi. Nataka kurudi kule ambako Mlinzi alinituma, nataka kurudi Afrika. Na kweli alirudishwa akafia huko. Kaburi lake ni eneo lenye umuhimu mkubwa mno kwa waumini wa Kiafrika, na sasa kando ya kaburi hilo limeongezwa la Mkono wa Hoja pekee mwafrika, Enock Olinga. Hii ni aina ya huduma na ubora wa huduma iliyotukuka…"

***

"Nilikuwa sijapata fursa ya kuongea na Rahmat. Nilimuita na kumwambia, 'Njoo tafadhali, kaa karibu na mimi. Nieleze kuhusu……' Kwa hiyo akanieleza kuhusu watu wa huko. Alikuwa daktari wa serikali huko na alizoea kutembea kwa miguu kupitia msituni, msitu mkubwa sana ili kutembelea wagonjwa wake vijijini katika kisiwa hicho kizima chenye miamba. Alisema kwamba walikuwa uchi na walikuwa na michoro mingi sana mwilini (tattoo). Ilikuwa ni sanaa katika eneo hilo la dunia. Nilisema 'Sawa, kwa hiyo ulifanya nini? Uliwaambia wavae nguo? Alisema,'Hapana, kwa nini? Sikwenda huko kuwaambia wavae nguo. Nilikwenda huko kuwaambia juu ya Baha'u'lláh. Ndiyo, hilo lilishawishi moyo wangu. Tangu wakati huo upendo wangu kwa Muhajir haukuwahi kuzimika kamwe. …Muhajir aliendelea na kuendelea kuhudumia…hadi alipodondoka chini na kufariki…

***— Mkono wa Hoja ya Mungu Ruhiyyih Khanum, kutoka hotuba katika The Gathering, Batterwood, Ontario, Canada, Agosti 2, 1980***

"Kila ushindi wa ufundishaji katika Imani kwa mtangulizi, unaweza kufuatiliwa nyuma mwanzoni,….na kumbuka alikuwa ni Baha'u'lláh, ambaye alitoa mwito kwa ajili ya utangulizi, siyo kutoka kwa Mabaraza ya Kitaifa au Mikono wa Hoja au shirika letu kuu la Nyumba ya Haki ya Ulimwengu au mpendwa Mlinzi au hata 'Abdu'l-Bahá, bali Baha'u'lláh. Huyo ndiye tunaitikia mwito Wake tunapoinuka kuwa watangulizi…. Hakuna

kinachoweza kuboresha maisha ya binadamu na kuyapa maana na kutosheka kama kitendo cha kuinuka na kuwa mtangulizi.....Ni baraka, neema itolewayo kwetu sisi katika siku hii kupitia rehema na huruma ya Baha'u'lláh ...."

***— Mkono wa Hoja William Sears, kutoka Mwito kwa ajili ya Utangulizi***

"Utangulizi unalinganishwa na kufa kishahidi na mateso. Watavuna matunda kama yale ya waumini wa mwanzoni kwa dhabihu zao"

***— Mkono wa Hoja Tarazulláh Samandari, kutoka hotuba ya 'the European International Conference' Julai, 1953, iliyochapishwa katika Bahá'í World, Vol XII, uk. 175***

"Wabahá'i wote hutamani kuona Hoja ya Baha'u'lláh ikifunika dunia nzima, lakini upanuzi haujileti wenyewe. Hatuna budi kutenda; hatuna budi kuinuka, hatuna budi kwenda. Tangu mwanzo wa Mipango, Mlinzi mara zote alituomba kuinuka na kwenda...Naamini watangulizi wana nafasi ya kipekee, daraja la juu sana, kwa sababu ni wao wanaobeba kurunzi ya mipango. Upanuzi hauletwi na watu wanaotulia sehemu moja. Ni kwa sababu hii kwamba Wabahá'i wanaombwa kwenda sehemu zote duniani. Dunia nzima inahitaji Imani ya Kibahá'i. Ulishapiga hesabu ni watu wangapi waliopo duniani wakati huu....bilioni 4. Ulishapiga hesabu ya idadi ya Wabahá'i? Kwa hiyo, ni watu wangapi hawajasikia ujumbe wa Baha'u'lláh?

"Kwenda utangulizi tunahitaji vitu viwili. Kwanza, ni uamuzi wetu kuinuka na kwenda kuwa watangulizi, na hii inakuja kutokana na upendo wetu kwa Hoja.....Na kipengele kingine hakionekani, ni mathibitisho ya Baha'u'lláh"

***— Mkono wa Hoja Dkt. Ali Mohammad Varqa, kutoka hotuba ya 'The Gathering', Batterwood, Ontario Canada, August 3, 1980***

"Shukrani zetu kwa watangulizi, Mabaraza ya Kitaifa na marafiki waliowezesha ushindi huu wote. Nina hakika ambao wamekaa vituoni mwao wanajua ukuu wa siku ya leo..... hebu tusiache fursa hizi ambazo Baha'u'lláh ametuachia. Hebu tuthamini na kutambua ukuu wa ufundishaji wetu.......

Kama mwaka mmoja hivi uliopita nilianza safari ya kutembea duniani. Kabla ya kuondoka nilikuwa na woga mwingi kuchukua jukumu hili, lakini mmoja

wa marafiki alisema ‘Nenda Amerika Kusini na uwape upendo.....kulikuwa na swali moja ambalo lilikuwa linajirudia rudia kwa kuulizwa. Nataka kulirudia hapa na jibu ambalo nilitoa. Katika maeneo mengi, marafiki baada ya kusikia taarifa za India, Afrika, Indonesia na za sehemu zingine ulimwenguni-walikuwa hasa wakivunjika moyo na kusema ‘Hivi sisi tuna tatizo gani? Tumekuwa hapa miaka mitano na kuna Wabahá’i kumi tu. Je, njia yetu haifai? Je, sisi ni wa kiroho kama walivyo watu wa India? Je, tuna matatizo gani?’ “Nataka kumhakikishia kila mmoja kwamba watangulizi hawana tatizo lolote na wala hakuna tatizo na njia wanazotumia bali kuna hiki kitu kidogo kisichoeleweka. Wanafikiri kwamba India imepata matokeo haya yote kwa mwaka huu mmoja au Afrika au Indonesia. Hapana, marafiki wapendwa, haya ni matokeo ya karibu miaka tisini ya jitihada. Baha’u’lláh, Yeye Mwenyewe alimtuma Jamal Effendi ambaye alikwenda katika majimbo yote ya India na kuongea juu ya Imani, na alirudi kwa Baha’u’lláh akionekana mikono mitupu. Baha’u’lláh alimwambia arejee akapande mbegu--‘Hili ndilo jukumu lenu’. Safari iliyofuata Jamal Effendi alikwenda katika majimbo yote ya India, alikwenda Burma, Singapore, Java, Ufilipino na katika baadhi ya visiwa vya Pasifiki, na mwalimu huyo wa Imani mwenye uwezo kabisa alifariki bila kuona matokeo ya kazi yake. Sasa baada ya kifo cha Jamal Effendi mpendwa Bwana alituma walimu wengi huko India, mpendwa Mlinzi pia alituma walimu wengi huko India. Matokeo ya taabu kwa walimu wote hawa hayakuonekana kwa haraka. Ulikuwa ni mjongeo wa polepole katika udongo wa roho za watu. Lakini tafadhali sikiliza maneno ya Bwana wakati walipokuwepo waumini kumi na tano hadi ishirini katika India nzima na waumini dhaifu sana. Aliwaandikia ‘Badiliko kubwa la dini litatokea katika India nzima, kutoka upande mmoja wa nchi hadi mwingine, itakuwa kutaniko la lulu takatifu. Marafiki wa India watainuka kuhudumia kwa kiwango ambacho watakuwa mfano wa huduma katika nchi zote jirani. India itainuka kwa kiasi kwamba wataifanya Thailand paradiso na wataihuisha Japan.’

Haya ndiyo mambo yaliyowafanya waumini kuendelea na juhudi yao. Na sasa baada ya miaka themanini au tisini, ghafla mbegu zikaanza kuota. Kitu kile kile kimetokea Afrika. Kazi ya Afrika siyo matokeo ya kazi ya mwaka huu au mwaka jana. Vile vile, Baha’u’lláh Mwenyewe alituma mwalimu Wake wa kwanza Haju kwenda Afrika....Matokeo ya dhabihu za watu wote hawa yanajidhihirisha sasa. Kwa hiyo, wale ambao wamekuwa wakifanya juhudi

katika maeneo fulani kwa miaka mitano au kumi wala wasilalamike. Haya ni matokeo ya kazi ya miaka themanini–ndiyo miaka tisini na taabu. Fanya kazi mchana na usiku, na kwa muda huo mavuno yatakuwa tayari. Baha'u'lláh amesema kwa uwazi kwa marafiki: Jukumu lenu ni kupanda mbegu. Mungu aidha atazifanya zikue au atazizika. Wajibu wenu ni kukaa katika vituo vyenu na kupanda mbegu. Hitaji kubwa kuliko yote kwa maendeleo haya ni subira. Subira ni kitu kilichoelezwa katika Qur'án kuwa kina malipo yasiyo na kikomo…. Tafadhalini kuweni na subira, Mungu atafanya kazi kupitia nyinyi hata kama haitakuwa katika kipindi cha maisha yenu-maisha ya vizazi vitakavyofuata baada yenu. Huduma zote zitapewa thawabu. Kuwa na hakika! Kuweni na hakika na kaeni kwenye vituo vyenu vya utangulizi. Hudumia na kuwa thabiti katika njia ya Mungu katika kituo ulichopewa katika kipindi cha mpendwa Mlinzi…..Kama ingekuwa rahisi kila mmoja angefanya huduma hii. Kwa hiyo, ninyi ambao ni jasiri, mkubali hilo jukumu; onesheni ujasiri wenu hadi mwisho wa maisha yenu. Hebu tusifikirie kutostahili kwetu katika njia ya huduma, marafiki wapendwa."

***— Mkono wa Hoja Abu'l Qasim Faizi kwenye Mkutano wa Dunia, Mei 2, 1963.***

"Utangulizi ni Baraka kubwa kabisa ambayo inaweza kumjia mtu-hatua moja hadi kwenye uwanja wa huduma…… mtu asimamapo katika kizingiti cha uwanja huu na kujua kwamba kuna silaha moja tu ambayo itaruhusu ushindi. Kuna silaha moja tu ambayo tunayo ambayo itahakikisha kabisa ushindi, na silaha hiyo ni kumtegemea kikamilifu Baha'u'lláh. Mtu husali katika kila hatua ya njia. Mtu huhisi ndani mwake muunganiko mpya na Mungu, hisia ya ukaribu huzaliwa kwani mtu kwa haraka hupata utambuzi wa majibu-njia ikiwa imewekwa alama kwake; mahitaji binafsi ambayo yalionekana muhimu nyumbani, ambayo yalimchukulia muda na nguvu nyingi hupotea au hutafuta kiwango kipya. Mtu hatimaye hujua kuwa hayupo pekee, huhisi viwango vipya, hutembea njia ya ajabu kwa miguu yake halisi. Kuna majaribu, mtu hawezi kuingia katika uwanja huu huku akikazia mwangaza wa kiroho kwa huduma bila kuonesha udhaifu. Hii pia ni sehemu ya baraka. Mtu huanza kujielewa mwenyewe. Kwa hiyo, ningesema kwa mtu yeyote-chukua fursa kabla hujachelewa. Kumbatia Baraka hii. Usiwe na hofu. Piga hatua kwenye uwanja. Juu ya yote, usali ili uweze kufanikiwa, usisite katikati ya uwanja. Ni Baraka kubwa iliyoje kuzaliwa katika kipindi hiki,

katika siku za mwanzo wakati utangulizi unawezekana… unapojitoa kuwa mtangulizi hauhitaji kujua kule unakoenda, huhitaji kujali unaenda wapi. Kwa sababu unaenda nje utaongozwa na Baha'u'lláh. Tumebarikiwa kwamba Mungu atawasaidia wale wote watakaoinuka kumtumikia Yeye. Tunajua kuwa tutaambatana na kundi la malaika wateule ambao watafungua milango na kutayarisha njia kwa ajili yetu…"

***— Mkono wa Hoja John Robarts, kutoka hotuba katika 'The Gathering', Batterwood, Ontario, Canada, August 3, 1980***

''……….tumaini pekee, mwanga pekee katika ulimwengu ni mwanga wa Baha'u'lláh….watangulizi wamekuwa wakituambia kwa miaka mingi kwamba umati unasubiri kupokea habari za upendo wa Mungu na ujio wa Baha'u'lláh. Tunazo njia pekee ambazo wataweza kuzipata ni kwa sisi kwenda na kuzitoa kwao…"

***— Mkono wa Hoja John Robarts, kutoka hotuba katika Konvensheni ya Kitaifa ya Vancouver, Canada, Mei 3, 1980***

"… chochote ambacho kimefanyika kupitia kazi ya watangulizi-kufungua maeneo mapya, kuunda Mabaraza ya Mahali na Kitaifa, kuandaa konvensheni, kuweka misingi-yote yalikuwa na lengo moja kuu—ukombozi wa kiroho wa moyo wa mtu, na lengo hilo bado lipo. Bado hatujafika mwisho wa safari. Lazima tuendelee….."

"Walimuuliza Mlinzi, 'Ni kipi muhimu kabisa?' Na Mlinzi alisema, 'Kwanza kutangulia katika eneo ambalo halijafunguliwa. Pili, kutangulia katika maeneo ya uimarishaji. Tatu, kutangulia katika maeneo ya nyumbani, na nne, kufundisha popote uishipo. Kwa hiyo, kusudi la maisha yetu ni kuwa watangulizi na kufundisha lakini kama unataka kujua ni lipi la kwanza, na lipi unaweza kulisahau na kufanya lililo muhimu zaidi kwanza ni kufanya utangulizi mbali zaidi. Panavyokuwa mbali zaidi ndiyo vizuri zaidi. Kwa haraka ndiyo vizuri zaidi…… huu hasa ni wakati wa kuvuna roho za watu. Kwa sababu kupitia jitihada zote hizi–tunaweza kuita miaka mia moja ya jitihada, kupitia Wana—mapambazuko, kupitia wafa kishahidi, kupitia watangulizi na watawala, sasa ulimwengu upo tayari kuja kweye Imani. Watu wapo tayari na wapokevu na inategemea tu Wabahá'i na watangulizi ambao watakwenda na kuvuna kwa ajili ya Imani. Lazima tuelewe suala hili

muhimu, mpendwa Mlinzi alisema kila mtangulizi anayekwenda nje ya jumuiya yake kwenye utangulizi siyo tu kwamba anatoa uvuvio na manufaa kwa jumuiya yake mpya ijayo, bali atakuwa chanzo cha msaada na uvuvio katika jumuiya yake anayotoka. Baraka ya Mungu itakuja kwa kila jumuiya inayotuma mtangulizi''.

"Nafikiri kwamba utangulizi wenyewe utakuimarisha…Hakuna kitakachotokea kama utakaa bila kufanya chochote na kubaki nyuma, kwa hiyo, fanya (utangulizi na kujiimarisha) vyote kwa pamoja. Kuna hadithi ya wasichana wawili waliokuwa wanaenda shule, na mmoja akamwambia mwenzie 'Tumechelewa, acha tukae na tusali ili tusichelewe' na mwenzie akamjibu, Hebu tusali huku tukikimbia…….. ''

"Kama mambo yote katika maisha huwa unapanga, kwa nini usipange kuwa mtangulizi? ….lazima tupange, kila mmoja, haraka iwezekanavyo. Na tuwaandae watoto….Wazazi wafungue akaunti ya benki ya utangulizi kwa watoto wao, hakikisha wanakwenda kuwa watangulizi, lazima wasomee katika maeneo mengine. Haiwezekani mtu afie pale alipozaliwa. Hiyo imekwisha. Lazima tuwe kwenye mwendo, mwendo uwe ule wa jinsi ambayo Mungu anataka, katika welekeo sahihi. Shughuli ya utangulizi inapaswa kuwa ya kila mmoja na inawezekana. Hitaji ni kubwa sana, hivyo kila mmoja katika wadhifa wowote anaweza kuwa mtangulizi. Baha'u'lláh Mwenyewe alitupa mfano. Wakati Alipokuwa anaanza mwendo kutoka Iraq alitangaza Imani Yake. Wakati mkuu kabisa katika Maisha Yake alikuwa katika mwendo-alipotangaza Imani Yake kwa Ulimwengu. Na 'Abdu'l-Bahá alikuwa mfano, Alikuwa na mengi ya kufanya katika Nchi Takatifu lakini aliacha kila kitu nyuma na kwenda kufundisha. Kwa hiyo, mjongeo huu wa kufundisha ni kitu cha daima. Lazima uende, uende, uende…… na uwe na hakika kuwa Baha'u'lláh yupo nawe na atakushika mkono, utafikia malengo yako na utatoa huduma kubwa kwa Imani. Sasa ulimwengu unatusubiri……. Allah-u-Abhlá."

***— Mkono wa Hoja Dr Rahmatulláh Muhajir, imenukuliwa kutoka sauti ya hotuba yake iliyorekodiwa kuhusu Utangulizi***

Kwa kuhitimisha, hakuna maneno ya kutosha kuelezea thamani ya huduma yenye dhabihu iliyotolewa na Mikono wa Hoja, labda itoshe tu kunukuu hapa

sehemu ya maneno kutoka kwenye ujumbe wa shukrani wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Mikono wa Hoja, Aprili 30, 1963:

***"Historia nzima ya dini haituoneshi kumbukumbu yoyote ya kulinganisha ya nidhamu binafsi, uaminifu mkamilifu kama huu na kujikana kwa aina hii kwa viongozi wa dini wanapojikuta ghafla wamenyang'anywa uongozi wao wenye uvuvio mtakatifu. Deni la shukrani ambalo jamii ya binadamu kwa vizazi, hapana, kwa zama zijazo ambalo inalo kwa roho hizi chache zilizopatwa na majonzi, thabiti na shujaa haliwezi kukadirika".***

## Marejeleo


1. Baha'u'lláh, akinukuliwa katika H.M. Balyuzi, *Eminent Bahá'ís in the Time of Bahá'u'lláh*, Oxford: George Ronald, 1985- 173
2. Tablets of Bahá'u'lláh Revealed after the Kitáb-i-Aqdas, Bahá'í Publishing Trust,

Wilmete -USA, 2005, 7: 83

3. Wasia na Agano la 'Abdu'l-Bahá
4. Taherzadeh, Adib, The Revelation of Baha'u'lláh; London: Bahá'i Publishing Trust, 1972 v.3 pp 313-315
5. i.'Memorials of the Faithful, (from Writtings and Utterances of 'Abdu'l-Bahá, uk 523 hadi 527; Bahá'i Publishing Trust, New Delhi, India, ii.God Passes By, uk. 130-196
   iii. The Revelation of Baha'u'lláh. vol.2,
6. i. The Revelation of Baha'u'lláh vol.3, Adib Taherzadeh, George Ronald Publishers, 1983
   ii. Windows to the Past-The Heavely Doves, by Darius Shahrokh
7. Wasia na Agano la 'Abdu'l-Bahá
8. Kama hapo juu
9. The Bahá'í World, Volume XV, pages 421 – 423
10. Waraka wa tarehe 11 Aprili, 1916; kifungu cha 6 na 9
11. Lights of Fortitude-Glimpses into the Lives of Hands of the Cause of God, Baron Harper, George Ronald Publisher, 1997.
12. *Ministry of the Custodians*, uk. 28
13. *Ministry of Custodians*, uk 321
14. *Ministry of Custodians* uk 433
15. *Nyumba ya Haki ya Ulimwengu*, *Jumbe za 1963–1986* 20.6–9.
16. *Nyumba ya Haki ya Ulimwengu*, *Jumbe za 1963–1986 131–32.1: 246*
17. Ujumbe wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu wa Aprili 30, 1963 kwa Mkutano wa Dunia wa Wabaha'i mjini London, Uingereza.
18. (Sala za Bahá'u'lláh, Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1997), uk. 83)